# Nipashe

Jumatatu Februari 17, 2020 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580156

The Guardian digital

www.ippmedia.com

nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710




## Madhila yanayobeba majonzi ulawiti wa wanafunzi shuleni

UKURASA 4




UKURASA 15

# Mwalimu mmoja aachiwa kufundisha shule nzima

**NI** shule yenye jumla ya wanafunzi 242 na madarasa...

*Endelea ukurasa wa 2*



Mwenyekiti wa Chadema, Freeman Mbowe (kushoto), akiwa na Naibu Katibu Mkuu (Zanzibar), Salum Mwalimu pamoja na wajumbe wa Kamati Kuu wa chama hicho, wakiingia katika ukumbi wa mkutano kujadili mambo mbalimbali kuelekea Uchaguzi Mkuu 2020 jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## MTOTO AUAWA AKIPORA KWA BASTOLA YA BABA

UKURASA 2

## Bashiru aonya wanaoitishia CCM

UKURASA 2







Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

Google Play App Store



**MICHEZO** SVEN ATOA MKAKATI WA UBINGWA SIMBA UK. 32

MAONI, KATUNI UK.6

## Mtoto auawa akipora kwa bastola ya baba

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

MTOTO Victor Mwasoro (17), ameuawa na wananchi wenye hasira kali baada ya kuvamia kibanda cha kutuma na kupokea fedha akiwa na bastola ya baba yake kwa lengo la kupora fedha.

Tukio hilo lilitokea mwishoni mwa wiki katika eneo la Sae jijini Mbeya na kwamba mtoto huyo alifariki kutokana na kipigo kikali alichokipokea.

Akielezea tukio hilo, Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Mbeya, Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa Polisi, Ulrich Matei, alisema mtoto huyo alivamia kibanda cha

Sauda Danda akiwa na bastola yenye namba za usajili 00098503 ikiwa na risasi saba.

Alisema baada ya wananchi kumshtukia walimvamia na kuanza kumshushia kipigo kwa kutumia silaha za jadi.

"Uchunguzi wa awali unaonyesha kuwa mtoto huyo aliichukua silaha hiyo nyumbani kwao na inamilikiwa na baba yake, wakati anaingia kwenye kibanda hicho kujaribu kuitumia kupora alikuwa ameihifadhi kwenye kifungashio," alisema Kamanda Matei na kuongeza:

"Baada ya kuokolewa mikononi mwa wananchi waliokuwa wanampiga alikimbizwa katika Hospitali ya Kanda ya Rufani ya Mbeya ambapo alifariki akiwa anaendelea kupatiwa matibabu."

Kufuatia tukio hilo, Kamanda Matei aliwataka wamiliki wa silaha mkoani humo kufuata sheria za umiliki wa silaha ili zisiingie kwenye mikono ya wahalifu.

Aidha, aliwatahadharisha majambazi wanaotumia silaha kuwa kwa sasa Mkoa wa Mbeya siyo wa kujaribu kufanya matukio ya aina hiyo kwa kuwa jeshi hilo liko makini na liko tayari kukabiliana nao wakati wowote.

# Mwalimu mmoja afundisha wanafunzi 242

**Na Jaliwason Jasson,** MANYARA

SHULE Shikizi ya Maweni, Halmashauri ya Babati mkoani Manyara, yenye wanafunzi 242 na madarasa manne ina mwalimu mmoja pekee.

Mwalimu wa Mkuu wa shule hiyo, Jacob Mwenda, alitoa taarifa hiyo wakati akizungumza na Kamati ya Siasa ya Wilaya ya Babati na wananchi.

Mwalimu Mwenda alisema shule hiyo ina madarasa ya awali hadi darasa la tatu huku masomo yote akifundisha peke yake.

Alisema darasa moja anaweza kufundisha masomo mawili ili kila mwanafunzi aweze kuambulia kitu.

"Naiomba serikali inisaidie kuongeza walimu angalau tuwe wanne ili tuweze kufundisha wanafunzi hawa," alisema Mwalimu Mwenda.

Mmoja wa wananchi akizungumza na Nipashe kuhusu uhaba wa walimu kwenye shule hiyo, Rukia Kemo, alisema kwa hali hiyo uwezekano wa watoto kufanya vizuri ni mgumu.

Aliiomba serikali kuongeza walimu kwenye shule hiyo kwa kuwa wanahitaji watoto wao wafanye vizuri kwenye masomo na kufaulu.

Katibu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Filbert Mpwepwe, akizungumza na wananchi hao aliwataka viongozi wa Kijiji cha Endadosh na Kata ya Qash kuongeza jitihada ili shule hiyo ikamilike haraka.

Naye Mwenyekiti wa Halmashauri ya Babati, Nicodemus Tarimo, alisema wananchi wa kijiji hicho hawajitumi licha ya halmashauri kuwachangia Sh. milioni tano.

Tarimo alisema ili shule iweze kupata usajili ni lazima iwe imekamilisha ujenzi wa miundombinu kwa asilimia 75.

Alimtaka diwani wa kata hiyo kuwachukulia hatua wenyeviti wa vitongoji wanaokula fedha ya michango ya wananchi badala ya kulalamika.

Diwani wa Kata ya Qash, John Kanda, alidai kinachokwamisha ujenzi wa shule hiyo ni fedha kutafunwa.



Waziri Mkuu Kassim Majaliwa (katikati), akipokea zawadi kutoka kwa Mwenyekiti wa Bodi ya Kiwanda cha kutengeneza nguo cha Nida Textile Mills, Haji Mohammed Rafiq (kulia), wakati wa Maulid ya Mazazi ya Mtume Muhammad (S AW) jijini Dar es Salaam jana. Kushoto ni Sheikh Al Sayyid Afeefuddin Al Jailaani kutoka Iraq. Wa pili kulia ni Sheikh Mkuu, Mufti Abubakar Zuber Bin Ali. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Bashiru aonya wanaoitishia CCM mitandaoni

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

KATIBU Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Dk. Bashiru Ally, amesema chama hicho hakitasita kumfukuza mwanachama wake bila kujali, umri, cheo au wadhifa kwa kukitishia chama na kuzungumza matatizo katika mitandao ya kijamii badala ya kuwasilisha kwenye vikao vya chama.

Alisema CCM ni chama kikubwa nje na ndani ya nchi na kinaheshimu demokrasia kwa wanachama wake hivyo matatizo yanapotokea kati ya viongozi wa chama na wanachama yanapaswa kufikishwa katika vikao halali vya chama badala ya kukimbilia kuandika katika mitandao ya kijamii.

Dk. Bashiru alitoa onyo hilo kwenye Mkutano Mkuu Maalumu wa CCM, Manispaa ya Morogoro wakati wa kupokea taarifa ya utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya chama hicho uliofanywa na Mbunge wa jimbo hilo, AbdulAziz Abood, katika kipindi cha mwaka 2015-2020.

Dk. Bashiru, alisema amelazimika kutoa agizo hilo baada ya siku za hivi karibuni baadhi ya wanachama na wengine waliowahi kuwa viongozi na kushika nyadhifa mbalimbali kukimbilia katika mitandao ya kijamii kueleza matatizo au tofauti zinazotokea ndani ya chama hicho, na kuonya kamwe matatizo hayo hayawezi kujibiwa na yeye katika mitandao ya kijamii.

"Kama kuna tatizo ndani ya chama kwa kiongozi na mwanachama, utaratibu umewekwa mzuri katika chama chetu, peleka tatizo katika vikao kuna ngazi ya tawi, wilaya na mkoa, ukishindwa peleka kwa Katibu Mkuu, lakini sio kukimbilia katika mitandao ya kijamii, hatuwezi kukujibu huko zaidi tutakuchukulia hatua kali ikiwamo ya kukufukuza uanachama," alionya Dk. Bashiru.

Alimpongeza, Mbunge wa Jimbo la Morogoro Mjini, Abood kwa kutekeleza ilani ya chama hicho kwa vitendo na kukubarika kwa wananchi wake.

"Nimekuwa nikisikia mengi unayofanya kwa wananchi wako, lakini leo nimeshuhudia mwenyewe mwendelezo huo wa utekelezaji wa Ilani ya chama baada ya kutoa gari la wagonjwa kusaidia wananchi kukimbizwa hospitali ndio tunataka wabunge kama nyinyi inatufanya CCM kutembea kifua mbele," alisema.

Awali akiwasilisha utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi, Abood alimshukuru Rais John Magufuli kwa kuleta fedha za utekelezaji wa miradi mikubwa katika jimbo hilo, ikiwamo ujenzi wa stendi ya kisasa, soko kuu, miundombinu ya barabara, huduma za afya, mradi mkubwa wa maji na huduma nyingine za kijamii.

Alisema ahadi zote alizoahidi wakati wa uchaguzi kwa sasa ametekeleza kwa asilimia 90 na asilimia 10 iliyobaki kwa kushirikiana na wananchi katika maeneo mbalimbali ya jimbo hilo na uongozi wa CCM katika wilaya hiyo.

Katika hatua nyingine Dk. Bashiru amewapokea na kuwakaribisha katika chama madiwani wawili wa Chadema, akiwamo wa kata ya Kilakala, Mabura Lusewa na Gabriel

INAENDELEA UK. 8

# HABARI KITAIFA




Watendaji wa Mauzo wa Mikoa wa Kampuni ya The Guardian Ltd wakiwa pamoja na wakuu wa idara katika ofisi za kampuni hiyo, baada ya kumaliza mafunzo ya siku nne. Kutoka kushoto Meneja Usambazaji, Emanuel Lyimo, Mkurugenzi wa Biashara, Ajay Goyal na Mkurugenzi wa Fedha, Samuel Orgeness. Mstari wa mbele kutoka kulia ni Baraghash Hassan, Heavens Mrema, Stephen Rwechungura, Calvin Lyimo, Esther Mwakalobo na Siangicha Ngowi. Mstari wa nyuma kutoka kulia ni Elia Elisha, Jackson Paulo na Maurine Mrema. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Watanzania waondolewa hofu corona

**Na Woinde Shizza,** ARUSHA

NAIBU Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Faustine Ndugulile, amewahakikisha Watanzania kuwa nchi bado iko salama na hakuna mgonjwa yeyote mwenye ugonjwa wa virusi vya corona.

Dk. Ndugulile alitoa kauli hiyo kwa waandishi wa habari akiwa jijini Arusha katika ziara zake za kikazi.

Katika maswali yao waandishi walitaka kujua kuhusu tetesi za kuwapo kwa ugonjwa huo nchini, pamoja na kufahamu ukweli wa taarifa za mtu anayedai kuwa na dawa za ugonjwa huo.

"Niseme tu kuwa Tanzania mpaka sasa hivi bado tuko salama na hakuna mgonjwa yeyote ambaye ameripotiwa na amethibitika kuwa na ugonjwa," alisema Dk. Ndugulile.

Alisema serikali inafuatilia taarifa mbalimbali za washukiwa na watu wote ambao wanawahisi kuwa na ugonjwa huo na kuwapima na kubaini kuwa hawana ugonjwa.

"Tumeendelea kuchukua tahadhari mbalimbali na mimi niko katika mkoa huu wa Arusha na nitaenda Kilimanjaro kwenda kuangalia utayari," alisema Dk. Ndugulile na kuongeza kuwa ameridhika na maandalizi ya mkoa huo katika kudhibiti ugonjwa huo.

Akijibu kuhusu mtu aliyedai kuwa na dawa ya kutibu ugonjwa huo ambaye anajulikana kwa jina la Mosses Mollel, maarufu kwa jina la 'Nabii namba saba', Dk. Ndugulile alisema ana taarifa za mtu huyo ambazo zimesambaa kwenye mitandao ya kijamii na vyombo vya habari akijitangaza kuwa anayodawa ya kutibu ugonjwa huo na kumtaka athibitishe kauli yake.

"Kimsingi nimeiona hiyo taarifa ya huyo mtu anayejiita Nabii Saba kuwa anayo dawa ya kutibu ugonjwa wa corona, ila hapa kwetu Tanzania hatuna maambukizi yoyote ya ugonjwa huyo, tunachotaka huyo mtu atuthibitishie uwezo wake wa kutibu huo ugonjwa wa corona," alisema Ndugulile.

Alisema kama atashindwa kuthibitisha atachukuliwa hatua kali za kisheria.

Dk. Ndugulile alisema serikali imetuma wataalamu wake kwenda kumsaka na kumhoji kama ana vibali vya kutoa huduma ya tiba na kujitangaza kuwa anatoa huduma ya kutibu ugonjwa huo hatari ambao hadi sasa mataifa bado yanahaha kusaka tiba.

Mollel mkazi wa Ngaramtoni wilayani

INAENDELEA UK. 8

## Dereva gari lililoua wanafunzi 5 Songea atiwa mbaroni Dar

**Na Gideon Mwakanosya,** SONGEA

JESHI la Polisi mkoani Ruvuma, linamshikilia dereva wa gari lililosababisha vifo vya wanafunzi watano wa Shule ya Msingi Ndelenyuma, Wilaya ya Madaba na kujeruhi mmoja.

Deveva huyo Salum Mohamed, alikamatiwa Manispaa ya Ilala jijini Dar es Salaam, alikokimbilia baada ya tukio hilo kutokea wiki iliyopita.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Ruvuma, Simon Maigwa, alisema dereva huyo alikamatwa mchana wa Februari 15, mwaka huu kwa ushirikiano kati ya polisi na jamii.

Aidha, alisema askari kutoka Songea ametumwa kwenda kumfuata na kumleta Ruvuma kwa ajili ya kuhojiwa na hatua za kisheria kuchukuliwa dhidi yake.

Ajali hiyo ilitoke Februari 12, majira ya saa nane mchana katika kijiji cha Ndelenyuma kwa gari lenye namba za usajili T 443 AQT aina ya Toyota Land Cruiser mali ya kampuni ya CAMUST likitoka Songea kuelekea Njombe kuacha njia na kuwagonga wanafunzi sita wenye umri wa miaka 10 hadi 13 wa darasa la pili hadi nne.

Baada ya kuwagonga gari hiyo ilipinduka na dereva alitoka na kutorokea kusikojulikana.

Mwanafunzi Hilda Kilasi (12) mwanafunzi wa darasa la nne, anaendelea na matibabu katika Hospitali ya Mkoa Songea na hali yake inaendelea vizuri.

Kwa mujibu wa Kamanda Maigwa, chanzo cha ajali hiyo ni mwendo kasi wa dereva ambaye inadaiwa hakujali hali ya mvua kubwa iliyokuwa ikinyesha kwenye eneo la kijiji hicho na utelezi kwenye barabara hiyo hatimaye gari lilimshinda na kuwagonga wanafunzi hao ambao walikuwa pembeni mwa barabara wakitembea kwa miguu kuelekea nyumbani wakitokea shuleni na kudondokea mtaroni ambapo watatu walisombwa na maji na miili yao kuokotwa takribani mita 100 kutoka eneo la tukio na wengine wawili walikutwa mtaroni jirani na eneo la ajali.


**KUMBUKUMBU**

**DIONISIA SIMON IVAMBI**



**DIONISIA UMETIMIZA MIAKA 17** TANGU UTUTOKE GHAFLA TAREHE 17/02/2003. NA KUTUACHIA MAJONZI YASIYOFUTIKA KATIKA FAMILIA YETU. INGAWA HAUPO NASI KIMWILI MDOGO WETU LAKINI KIROHO TUKO PAMOJA NAWE SIKU ZOTE. BADO TUNAKUMBUKA UCHESHI, UPENDO NA MOYO WAKO WA KUJITOA.

DIONISIA UNAKUMBUKWA SANA NA WANAO: NANCY SENIOR NA DIANA

DADA ZAKO VERONICA, OLIVA, JANETH, FRIDA, KAKA YAKO. SEBASTIAN, SHEMEJI ZAKO, MARAFIKI ZAKO PAMOJA NA WANAFAMILIA WOTE.

DAIMA TUNAFARIJIKA KWA MANENO HAYA: SISI TULIKUPENDA SANA MDOGO WETU LAKINI MUUMBA WAKO ALIKUPENDA ZAIDI.

*BWANA ALITOA NA BWANA AMETWAA JINA LA BWANA LIHIMIDIWE*

115631002



selcom

**TAARIFA KWA UMMA**



**JINA: VENANCE JOHN MWANSASU**
**MAHALI: DAR ES SALAAM**

Uongozi wa kampuni ya **SELCOM PAYTECH LIMITED** unapenda kuufahamisha umma kuwa mtajwa hapo juu kama anavyoonekana pichani si mfanyakazi tena wa kampuni hiyo tangu tarehe 6.1.2020. Kwamba kampuni haitawajibika kwa namna yoyote ile kwenye makubaliano au mkataba alioingiwa ama utakaoingiwa na mtajwa kwa niaba ya kampuni kuanzia tarehe tajwa hapo juu.

**Kwa maelezo zaidi tafadhali piga simu namba +255 68 616 2417**

# Madhila yanayobeba majonzi ulawiti wa wanafunzi shuleni

## ■Wabuni mfumo, maficho 'kuharibiana'
## ■Malalamiko ya bibi, butwaa kwa walimu

**Na Elizabeth Zaya**

Ni habari na simulizi iliyojaa ukakasi kuanzia kuisikia au kuifahamu kwa namna yoyote, haina kokote inakoweza kusimama zaidi ya neno mbaya, wanafunzi kulawitiana. Sasa hata jina na hadhi ya Mkuranga nayo inaangukia kwenye ubaya.

Mamlaka za kiuongozi wilayani humo, kuanzia Ofisi ya Mkuu wa Kamati ya Ulinzi na Usalama wilayani na nyenzo zake za usalama, Ustawi wa Jamii na walimu wa watoto hao, kila mmoja kwa nafasi yake anakiri kulifahamu na ama hatua zinazochukuliwa au kinachostahili kufanyika kukomesha hilo.

"Wanafunzi wenzangu walikuwa wananivizia wakati natoka shuleni kurudi nyumbani, mmoja ananishika mkono wa kulia na mwingine wa kushoto, halafu wananivua nguo na kuniinamisha chini...

"Wanafanya hivyo kwa zamu, mmoja akimaliza, anaanza mwingine na baada ya hapo, huwa wananitishia nisiseme kwa mtu yeyote, kwamba nikifanya hivyo wataniua."

Ni kauli ya mwanafunzi wa darasa la tano (jina tunalo) katika shule iliyoko kilomita chache kutoka makao makuu ya Wilaya ya Mkuranga mkoani Pwani.

Mwanafunzi huyo alikuwa akitoa ufafanuzi kwa Nipashe iliyomfuata kupata uhalisia wa tetesi hizo, ikiwa ni sehemu ya uchunguzi iliyoendesha wilayani humo kuhusu tuhuma za ulawiti miongoni mwa wanafunzi wenyewe.

Huku akiwataja kwa majina, alifafanua baadhi ya waliomtenda hivyo wanasoma naye shule moja na wengine si wanafunzi wenzake.

Aliendelea: "Siyo peke yangu wanayenifanyia hivi, tuko wengi (anawataja kwa majina), wanaotufanyia hivi, wengi ni wa darasa la saba (anawataja kwa majina). Wakati mwingine huwa wanatudanganya kwamba watatununulia chipsi."

Ni mazingira yapi hayo yanafanyika?

Mwanafunzi huyo ana simulizi ya ziada kwa Nipashe akisema: "Walikuwa wanatufanyia vitendo hivyo kila siku tunapotoka shuleni au tunapokuja (shuleni) asubuhi na kuna siku walinifanyia hivyo nikawa naumia sana! Nilishindwa kujizuia siku hiyo kwa sababu maumivu yalikuwa makali, nililia mpaka nyumbani na bibi aliniponiuliza, nilimwambia wamenifanyia vibaya.

"Bibi alinipeleka chooni kuniangalia, ndiyo akaanza kuniuliza, tena nilipojisaidia kilitoka 'kinyama'... alinishika na kunisafisha halafu akasema anipeleke shuleni akawaulize walimu.

"Nilimwambia bibi kwamba walionifanyia ni wanafunzi wa la saba, akasema 'twende akawatafute shuleni' na tulipofika na walimu nao walianza kuniuliza na nikawataja walionifanyia hivyo."

Mwanafunzi huyo aliendelea kusimulia kwamba hatua iliyofuata, alipelekwa hospitali alikopatiwa dawa, aliyofafanua matumizi yake kuwa: "Mpaka sasa bibi ananiwekea na sasa hivi sisikii maumivu tena. Tangu bibi alivyokuja kushitaki shuleni na nikawataja wale waliokuwa wananifanyia, sasa hivi wanawafanyia wengine, mimi wameniacha."



Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu.

**KULIKONI SHULENI?**

Nyayo za udadisi wa Nipashe zilifika hadi katika shule za msingi zinazohusika na kashfa hiyo kupata ufafanuzi na katika shule ya kwanza ilibahatika kukutana na Victoria Msuya na Rahim Mbululu, ambao ni walimu wakuu wasaidizi wa shule ambayo mtoto huyo anasoma.

Kwa kauli ya pamoja, walianza kwa kukiri uwapo wa kashfa hiyo katika maeneo yao ya kazi na baada ya kuwadadisi, kila mmoja kwa maelezo yake, aliangukia kuwa na taarifa ya vitendo hivyo vya ulawiti kufanyika kati ya wanafunzi wenyewe katika vipindi vya mapumziko na muda wa kwenda nyumbani.

Mwalimu Victoria alisema wanafunzi wengi waliowabainika kufanyiwa ukatili huo, ni wa madarasa ya tatu, nne na tano, kashfa hiyo ikifanyika zaidi eneo ambalo wanafunzi hao wamelibatiza jina la 'Chimbo'.

"Ukishamaliza eneo hili la shule, kuna sehemu ambayo walikuwa wanachimba mchanga, huko ndiko tuliwabaini wakiwa wanaenda kufanyia hivyo vitendo," alisema, huku akielekeza kwa kidole kwamba:

"Kama unavyoona shule yetu haina uzio... inapofika wakati wa mapumziko, watoto wengine huwa wanapata mwanya wa kwenda hata huko mtaani kutafuta vyakula vidogo vidogo.

"Wengine ndiyo huenda huko kwenye machimbo na huwezi kujua, na ndiyo huo muda huwa wanautumia kushawishiana."

Mwalimu huyo alisimulia njia zingine wanazotumia wanafunzi kutekeleza mabaya hayo, ni kwa wanaosoma kwa kubadilishana, baadhi yao hufanya hivyo kabla ya muda wa kuripoti shuleni.

Victoria alitoa mfano wa namna mojawapo njama hizo zinavyofanyika, kwamba kuna baadhi ya wanafunzi wanaoingia masomoni saa nne asubuhi, lakini wanaaga kutoka nyumbani mapema, kumbe safari yao inaanzia kwenye uasi huo na kisha inakamilishwa shuleni.

"Kwetu walimu, inakuwa si rahisi kujua kwa sababu unamwona mtoto amewahi darasani kama kawaida, kumbe kabla ya hapo kuna mahali alipitia," alieleza.

**WALIMU WALIJUAJE?**

Mkasa wa bibi kuwasilisha rasmi ukatili dhidi ya mjukuu wake, ndiyo Mwalimu Victoria aliutaja kusaidia kuwafumbua macho na masikio ya kuwapo utovu huo wa nidhamu, akiwa na ufafanuzi kwamba: "Jambo hilo lilitushtua sana na tukaamua kuwaita wanafunzi wote kuwahoji."

Alieleza hatua za haraka walizochukua kwamba ni: "Watoto walianza kutajana, tulibaini kwamba watoto wengi waliokuwa wanafanyiwa, ni wa darasa la tatu, nne na tano na waliwataja waliokuwa wanawafanyia na wengine tayari wazazi wao wameshawaondoa shuleni."

Naye Mwalimu Mbululu alisema wameanzisha utaratibu wa kufanya operesheni ya kufuatilia katika maeneo yote (likiwamo 'Chimbo') wanakobaini wanafunzi hao kufanyia vitendo hivyo.

"Kwa sababu tumeshafahamu mtandao wao, hata tukiona kuna mwanafunzi haonekani darasani, huwa tunawabana wenzake watuambie alipo na wakati mwingine wanatupeleka huko machimboni na tukienda tunamkuta.

"Kinachotushangaza ni kwamba hata hao wanaowaona huko mtaani wanashindwa kutoa ushirikiano kwa walimu. Kwa hatua hii waliyofikia hawa watoto, tunahitaji kushirikiana na jamii kuwasaidia hata kama siyo mwanao. Tabia hii ikienea, itaharibu watoto wengi," alibainisha.

Safari ya Nipashe ndani ya uwanda wa Wilaya ya Mkuranga, ilitinga kwenye shule nyingine ya msingi yenye wasifu wa kipekee kuwa na jumla ya wanafunzi 2,284 ikiwa na vyumba vya madarasa 10 tu.

Mwalimu Mkuu wa Shule hiyo, Adrian Tete, ambako ni umbali mrefu zaidi kutoka makao makuu ya wilaya, alianza kutambulisha ugumu wa mazingira ya utendaji wake katika kuwamudu wanafunzi akitamka:

"Kwa picha hiyo unayoiona hapa, hata kama kuna mtoto ametoroka, huwezi kujua mpaka umalize kufundisha halafu uwaite majina, na wakati huo tayari kama ameenda huko porini kufanya mambo yao hayo, hata ukienda kumtafuta unakuwa umechelewa.

"Tungekuwa na madarasa ya kutosha, wanafunzi wote wakawa wanasoma kwa wakati mmoja bila 'shift', halafu kukawa na uzio, ingesaidia, hata namna ya kuwadhibiti ingekuwa rahisi kwa sababu wakati wa mapumziko wasingekuwa wanatoka nje."

Nipashe ilipomdadisi zaidi kutaka kujua nafasi yake katika kashfa inayowakabili walimu wenzake kuhusiana na nidhamu mbaya ya vitendo vigeni visivyokubalika katika jamii kuvamia shule za Mkuranga, naye alikiri kwamba hajanusurika.

Katika picha ile ile inayowakabili walimu wenzake, Mwalimu Tete alisema tatizo kwa wanafunzi wake wamekuwa 'wakiharibiana' wenyewe kwa wenyewe, wahusika wakuu wa madhila hayo wakiwa ni wa madarasa ya pili, tatu na nne.

"Ni kweli katika shule yetu tulibaini watoto wetu wakifanyiana vitendo vibaya... hasa katika nyakati za mapumziko au wanapotoka majumbani kwao kuja shuleni na wanapotoka shuleni kurudi majumbani," alisema.

*ITAENDELEA KESHO

# SBL yafadhili masomo wanafunzi 10 Chuo Kilimo

**Na Mwandishi Wetu**

WANAFUNZI 10 wanaosomea kilimo katika Chuo cha Kilacha Agriculture and Livestock Training Center, kilichoko Moshi mkoani Kilimanjaro, wamekuwa wa pili kunufaika na ufadhili wa msomo unaotolewa na Kampuni ya Bia ya Serengeti (SBL) kwa wanafunzi wa kilimo nchini.

Chini ya mpango unaojulikana kama Kilimo-Viwanda, SBL inatoa ufadhili wa masomo kwa wanafunzi 50 kutoka katika jamii za wakulima kila mwaka kwa kuwalipia ada kwenye vyuo vya kilimo kwa kipindi chote cha masomo yao.

Mkurugenzi Mtendaji wa SBL, Mark Ocitti, akizungumza wakati wa hafla ya kutiliana saini katika Chuo cha Kilacha, alisema mpango huo unawalenga wanafunzi wanaotoka katika familia za wakulima ambazo hazina uwezo wa kuwalipia ada watoto wao na kuongeza kuwa itasaidia kuongeza wataalamu wa kilimo.

"Tunaamini kuwa mpango huu utawasaidia wanafunzi wanaotoka katika familia za wakulima zenye kipato cha chini kupata elimu ya juu huku pia ikichangia kuongeza wataalamu wa kilimo ambao watasaidia kuongeza uzalishaji," alisema.

Kwa mujibu wa Ocitti, mpango huo ni sehemu ya mkakati wa SBL wa kuongeza kiasi cha nafaka ambacho kampuni hiyo inanunua kwa ajili ya uzalishaji wa bia ambazo ni pamoja na mahindi, shayiri na mtama.

Alisema, mwaka jana SBL ilinunua zaidi ya tani za ujazo 17,000 za nafaka kutoka kwa wakulima wa ndani sawa na asilimia 70 ya mahitaji yake yote ya malighafi kwa mwaka.

"Kampuni ya SBL inalengo la kuongeza kiasi cha malighafi inayonunua kutoka kwa wakulima wa ndani hadi asilimia 85 kufikia mwaka 2020 na ndiyo maana tumeona umuhimu wa kusaidia kusomesha wataalamu wa kilimo ili wakafanye kazi ya kuboresha kilimo chetu. Kwa sasa kampuni inanunua malighafi kutoka kwenye mtandao wenye wakulima 400 hapa nchini," alisema.

Kwa upande wa mkuu wa kituo hicho, Benito Mwenda, aliishukuru SBL kwa ufadhili alioutoa na kuzitaka taasisi binafsi kujitokeza na kusaidia sekta ya kilimo ambayo ni sekta mama.

Mwezi Januari, Chuo cha Kaole Wazazi College of Agriculture kilichopo Bagamoyo mkoani Pwani, kilikuwa ni cha kwanza kunufaika na mpango huo wa ufadhili wa masomo unaolenga kuongeza wataalamu katika sekta ya kilimo nchini.



Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mhandisi Hamad Masauni, akiangalia kiatu kinachotengenezwa katika kiwanda cha Gereza la Karanga mkoani Kilimanjaro, mwishoni mwa wiki wakati wa ziara ya ukaguzi wa shughuli zinazofanywa kiwandani hapo. **PICHA: WMN**

# Afariki dunia kwa kutumbukia mgodini

**Na Mohab Dominick,** KAHAMA

MKAZI wa Kijiji cha Marito Kata ya Shilela Halmashauri ya Msalala wilayani Kahama, Amos Lucas (28), amefariki dunia baada ya kutumbukia kwenye shimo wakati akifanya uchimbaji wa dhahabu katika mgodi wa Bushimangila uliopo Kijiji cha Mhandu Kata ya Chela.

Vyanzo vya habari vilidai kuwa katika tukio hilo watu wawili walifariki dunia akiwamo Lucas aliyefariki papo hapo na mwingine ambaye hajafahamika jina lake, alifariki wakati akipatiwa matibabu.

Katibu wa Mgodi wa Bushimangila, Mwaje Doto, akizungumza jana na waandishi wa habari ofisini kwake alithibitisha kutokea kwa ajali hiyo na kumtaja aliyefariki kuwa ni Amos Lucas.

Alidai kuwa tukio hilo lilitokea Februari 12, mwaka huu saa 12:00 alfajiri na kuwa duara lililosababisha maafa hayo lilikuwa limezuiwa uchimbaji kwa sababu za kiusalama. Alisema kifo cha Lucas kilisababishwa na kuteleza na kutumbukia kwenye duara alilovamia.

Alisema alifanya hivyo baada ya walinzi kuondoka na kwamba hakuna mtu aliyejeruhiwa na kukimbizwa hospitalini.

Ofisa Mtendaji wa Kata ya Chela, Patrick Mahona alipotakiwa kuzungumzia tukio hilo alikiri kupokea taarifa ya watu watatu waliopata ajali katika mgodi huo kwamba kati ya hao mmoja amepoteza maisha.

TANZAM 2000

BUCKREEF GOLD COMPANY LIMITED

**Announces 4,291,000 ounces of gold contained in unclassified resources at the conclusion of its Phases I & 2 Resource Upgrade drilling along the 1.2km Buckreef Shear Zone**

TORONTO, February 14, 2020, Tanzanian Gold Corporation's, (TSX:TNX) (NYSE American:TRX) Board of Directors is pleased to announce Unclassified Mineral Resources for the 1.2km long Buckreef Shear Zone that amount up to 4,291,000 ounces contained in 242.4 million tons grading at 0.57 g/t Au at a block cutoff grade of 0.1 g/t Au. The Unclassified Mineral Resources are from an unconstrained block model using all the drilling results to date. Results at higher cut-off grades are shown in the table below.

As a consequence of the drilling program the Company completed in 2019, the largest drilling campaign in the Company's history amounting to over 17,650m in 60 holes during which a significant number of exploration targets were identified which require further drilling to upgrade the gold mineralization encountered in these exploration areas to the Inferred category.

Further, as the gold mineralization in the Buckreef Shear Zone is still open along strike to the northeast and down dip a Phase III drilling program has been started to further test the continuity of the mineralization at ultra-deep levels below mineralization encountered in Phase II.

And finally, the new global estimate of Mineral Resources in the Buckreef Shear Zone was derived from a new resource model developed for the Company that combines geological information such as major rock units, structures, alteration styles and assay data from over 1,000 holes that amounted to approximately 140,000m that were drilled along the Buckreef Shear Zone.

The new model includes holes drilled by previous owners of Buckreef as well as holes drilled by the Company since it acquired Buckreef in 2011; and includes the results from the drilling campaign in 2019.

In view of these considerations, the Company has elected to, in the first instance, give these unconstrained Resource estimates the designation of Unclassified – Exploration Targets. A NI 43- 101 Technical Report will be released in 45 days by Virimai Projects as part of the continuation of the results reported in the Pre-Feasibility Report published in June 2018.

This estimate will culminate Estimated Mineral Resources categorized into Measured, Indicated and Inferred Resources.

| Cut off Grade | Tonnage | Grade Au (g/t) | Tonnes Au | Oz ('000) |
|---|---|---|---|---|
| 0.1 | 242,403,762 | 0.57 | 137.8 | 4,291 |
| 0.4 | 85,394,995 | 1.25 | 106.9 | 3,330 |
| 0.5 | 70,207,693 | 1.43 | 100.1 | 3,119 |
| 0.6 | 60,214,862 | 1.57 | 94.7 | 2,949 |

Source : Virimai Projects
Mineral Resources that are not Mineral Reserves do not have demonstrated economic viability
Mineral Resources reported inclusive of Mineral Reserves (although no Mineral Reserves are reported)
Cut-off Grades of 0.1g/t Au to 0.5g/t Au
Estimates in 10m (X) by 10m (Y) by 10m (Z) blocks constrained by topography only
Specific Gravity ranges 2.0 to 2.8
Inconsistencies in totals are due to rounding
55% attributable to TRX

**Sample Protocol and QA/QC**
The sample chain of custody is managed by the Buckreef technical team under the supervision of Anthony Minde. Gold analyses reported in this release were performed by standard fire assay using a 50-gram charge with atomic absorption finish (0.01ppm LLD) and a gravimetric finish for assays greater than 10 grams per tonne. All assays were performed by Nesch Mintech Laboratory in Mwanza. Sampling and analytical procedures are subject to a comprehensive quality assurance and quality control program. The QAQC program includes duplication to the samples, blanks and analytical standards.

Intervals of core to be analyzed are split in half with a mechanized core cutter, with one half sent to the Laboratory for geochemical analysis and the remaining half kept in storage for future reference and uses.

Nesch Mintech Laboratory is ISO 90001 and 17025 accredited and employs a Laboratory Information Management System for sample tracking, quality control and reporting.

**Qualified Person**
The Company's Qualified Person, Mr. Peter Zizhou, has reviewed and approved the contents of this news release. Mr. Zizhou has a Master of Science (Exploration Geology) degree from the University of Zimbabwe (2000) and is a registered professional natural scientist with SACNASP (Reg. No. 400028/08).

Virimai Projects have read and approved the contents of this press release and do hereby confirm that they are now actively engaged as the Qualified Person (QP) undertaking the NI43-101 Mineral Resource Update Technical Report following the completion of the two phases of resource upgrade drilling conducted as per their recommendations in the Pre-Feasibility report of June 2018.

Tanzanian Gold Corporation, Executive Chairman, James Sinclair, commented "The numbers presented here today speak for themselves, and offer a first glimpse of some of the results of our year-long exploration and development program at Buckreef. This extensive and comprehensive program has been conducted with the most scientific of methods and at the highest of industry standards. This program would not be in place without critical, value added, financing completed in a year which has been fully transformational for our company. As we have said in the past, mines are not simply discovered – they are built. We will continue to build the Buckreef Mine toward the goal of world class status."

**James E. Sinclair**
**Chairman of Buckreef Gold Company Ltd.**

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Soka letu bado linahitaji wachezaji wa kigeni zaidi

**MWISHONI** mwa wiki kwa mara nyingine tena Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Dk. Harrison Mwakyembe, aliibua hoja ya kupunguzwa kwa idadi ya wachezaji wa kigeni Ligi Kuu Bara.

Kwa mujibu wa kanuni za Ligi Kuu Bara, kila klabu inaruhusiwa kusajili wachezaji wa kigeni wasiozidi 10, jambo ambalo Dk. Mwakyembe anataka mjadala mpana akipendekeza wapungue hadi watano.

Hii si mara ya kwanza kwa Waziri Mwakyembe kutoa pendekezo hilo, na safari hii ameweka hoja hiyo mezani akitaka viongozi na wadau wa soka, kuijadili kwa mapana zaidi.

Hoja ya Mwakyembe, yeye anaona klabu kuruhusiwa kusajili wachezaji 10, kunapunguza nafasi ya wazawa kucheza na kuibuliwa kwa vipaji. Hata hivyo, Nipashe tunaona hoja hiyo haina mashiko kwa maendeleo ya soka kwa sasa kwani soka letu linawahitaji wachezaji wa kigeni zaidi.

Tunasema hivyo kutokana na ukweli kwamba Ligi Kuu kwa sasa ina klabu 20, na zenye uwezo wa kusajili wachezaji hao 10 wa kigeni hazizidi tatu. Kwa ujumla kila klabu inaruhusiwa kusajili wachezaji wasiozidi 30, hivyo kwa msimu mzima kwa klabu 20, jumla ya wachezaji 600 hucheza ligi hiyo.

Kama klabu zinazoweza kusajili wachezaji wote 10 wa kigeni hazizidi tatu, hiyo ina maana watakuwa 30, hata hivyo tufanye jumla ya nyota wote wa kigeni kwa msimu Ligi Kuu ni 50.

Hiyo inamaana kwa msimu mzima kuna wazawa 550 watakaoonekana wakicheza Ligi Kuu, tunashindwa kuelewa ni vipi wageni 50 wanaweza kuzuia vipaji hivyo kuonekana.

Lakini pia, tunashindwa kuielewa hoja ya Waziri Mwakyembe kuwa wachezaji wa kigeni eti wenyewe wanalipwa mishahara mikubwa kuliko wazawa. Ikumbukwe tunaelekea katika soka la kulipwa, hivyo suala la mchezaji wa kigeni kulipwa zaidi ya mzawa, hilo haliwezi kuepukika kwa vyovyote vile.

Leo hii Muargentina Lionel Messi, ndiye mchezaji anayelipwa zaidi Ligi Kuu, Hispania huku Mjerumani Metus Ozil akiongoza kwa kulipwa zaidi Ligi Kuu England kama ilivyo kwa Mreno Cristiano Ronaldo pale Juventus kwenye Ligi Kuu Italia.


Lakini Waziri Mwakyembe pamoja na wadau wengine wanaotaka wageni kupunguzwa kutoka 10 hadi watano, watambue kwamba uwapo wao Ligi Kuu Bara unaboresha viwango vya wachezaji wetu.

Wachezaji wetu wengi wanacheza soka la ndani jambo ambalo tumekuwa tukipiga kelele tukiwataka kwenda kucheza soka la kulipwa ili waweze kuwa msaada kwa timu ya Taifa, Taifa Stars, kama hilo limeshindikana tuvutie wageni wenye viwango kuja nchini kucheza nao.

Hivyo, kinachotakiwa ni Shirikisho la Soka nchini (TFF) kusimamia kanuni yake ya wageni wanaosajili nchini kuwa na viwango vya hali ya juu ili kutoa changamoto ipasavyo kwa wazawa.

Mwisho pamoja na kuwapo wageni bado tunaona wazawa kama Hassan Dilunga, Erasto Nyoni, Jonas Mkude pale Simba huku Yanga, Kelvin Yondan, Metacha Mnata, Juma Makapu na Azam FC wachezaji kama Agrey Moris na wengine wengi wakiwa katika vikosi vya kwanza.

Na hao ndio wamekuwa tegemeo wanapoitwa kuitumikia Taifa Stars, hiyo inaonyesha ni kwa namna gani wanapambana kuwania namba klabuni jambo linaloboresha viwango vyao kila uchao.






## Muungwana Lazima Nilonge

# Ruvu kuweni wapole, kanuni mlipitisha wenyewe

Na Adam Fungamwango

MATUKIO haya mara nyingi hutokea kwenye Ligi Daraja la Kwanza Tanzania Bara, lakini safari hii limetokea kwenye Ligi Kuu na ndiyo maana mashabiki wengi wameonekana kushangaa.

Msimu huu kwenye Ligi Daraja la Kwanza kuna timu imepokwa pointi baada ya kutokuwa na gari la wagonjwa kwenye uwanja wake wa nyumbani na wageni kupewa pointi.

Halikuzungumzwa kwa sababu mashabiki wengi hawafuatilii. Sasa limetokea kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara. Jumatano iliyopita Prisons ya Mbeya ilipewa pointi tatu na magoli matatu baada ya gari la wagonjwa kukosekana kwenye Uwanja wa Mabatini, Mlandizi mkoani Pwani.

Nilisema kukosekana siyo kwamba halikuja kabisa, ila liliwasili dakika mbili baada ya muda wa nusu saa wa kusubiri uliowekwa kumalizika.

Ina maana liliwasili nje ya muda, hivyo Prisons wakaondoka uwanjani.

Hali hii ilizua sintofahamu, kila mmoja akiongea lake, lakini Kamati ya Uendeshaji na Usimamizi wa Ligi ya Bodi ya Ligi Kuu Tanzania, katika kikao chao wiki hii, kiliizawadia Prisons pointi tatu na magoli mawili kutokana na Ruvu Shooting kuvunja kanuni hiyo.

Ni kanuni iliyopitishwa msimu huu wa ligi. Ni kwamba timu yoyote mwenyeji ndiyo ina wajibu wa kuleta gari la wagonjwa na vijana waokota mpira viwanjani.

Klabu yoyote ile ikikiuka maagizo haya, basi mwamuzi hatakiwi kuchezesha mechi hiyo, na timu ngeni itapewa ushindi wa pointi tatu na magoli matatu.

Na ndicho kilichotokea. Nimeona viongozi wa Ruvu Shooting wakilalamika sana juu ya hili.

Lakini ukisikiliza malalamiko yao yanalenga sana kwenye ubinadamu na si kanuni.

Wanadai gari la wagonjwa halikuwapo kwa wakati kwa sababu lilipeleka mgonjwa kwenye Hospitali ya Tumbi. Ni kweli, lakini hili haliwezi kufanya kanuni ya soka ibadilishwe.

Kanuni inamtaka mwamuzi asubiri gari hilo kwa muda wa nusu saa baada ya muda ambao mpira ulitakiwa kuanza.

Dakika moja baada ya nusu saa mwamuzi anatakiwa kuvunja pambano. Vyovyote itakavyokuwa ni kwamba kanuni imevunjwa na Ruvu Shooting hawana cha kujitetea na inabidi tu wakubali, waangalie mbele na kujifunza kutokana na hili lililotokea.

Ni kwamba kanuni hizi zilipitishwa kabla ya Ligi Kuu kuanza na viongozi wa klabu zote, hivyo kwao hapo hakukuwa na kipya wasichokijua. Na kama walikuwa hawajui, basi hilo ni tatizo lao.

Mara nyingi kanuni hizi hutungwa na kupitishwa kabla ya msimu mpya wa ligi kuanza.

Shirikisho la Soka Nchini (TFF) huwataka viongozi wa klabu kupeleka mapendekezo yao, lakini baadaye hupewa kuyapitia na kuyafanyia marekebisho yale ambayo wanaona yanaweza kuleta matatizo, au hayatekelezeki.

Lakini mara nyingi viongozi wa baadhi ya klabu hupuuza kupeleka maendekezo au kuyapitia na matokeo yake, kanuni hizi zinapokuja kutumika ndipo wanaposhtuka na kushangaa.

Vile vile wapo baadhi ya viongozi wanapopitisha mapendekezo haya hawadhani kama yatawakuta wao, badala yake wanaona kuwa wenzao ndiyo wanaweza kuathirika, sasa linapowakuta wanaanza kulalamika kana kwamba ndiyo wanaziona kwa mara ya kwanza kanuni hizo.

Kwa kuwasaidia tu viongozi wa Ruvu Shooting kama wanaona kanuni hiyo haina tija basi msimu ujao wapambane kuiondoa na kuleta kanuni mbadala, lakini kwa sasa hawakwepi mkono wa adhabu, ili iwakumbushe na klabu zingine kuwa kuna aina hiyo ya kanuni ambayo waliipitisha wenyewe na inafanya kazi.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji:** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com

MJADALA

# Waarabu wanataka wageni, Wabongo tunawajadili

**Na Adam Fungamwango**

WIKI hii kumezuka kwa mara nyingine tena mjadala wa wachezaji wa kigeni wanaocheza Ligi Kuu Tanzania Bara nchini, ibaki idadi ya wachezaji 10 au wapunguzwe hadi kufikia watano.

Mjadala huu huwa unakuja kwa kupotea, halafu unaibuka tena kutokana na kuwa baadhi ya mashabiki wa soka wanataka idadi ya wachezaji wa kigeni iwe ndogo kwa ajili ya kuwapa fursa wachezaji wa Kitanzania.

Kwenye vipindi vya redio, televisheni na hata kwenye mitandao ya kijamii, imekuwa ndiyo mada na kila mmoja anayechangia amekuwa na mitazamo yake tofauti.

Kwa muda mrefu kuna watu wamekuwa akitamani Ligi Kuu iwe na wachezaji wengi wa Kitanzania, lakini wapo wanaotaka wachezaji wa kigeni kwa ajili ya kuipa nguvu, na kuifanya ligi iwe bora.

Wanaotaka wachezaji wa kigeni wapunguzwe ukiwasikiliza wana mitazamo ya kizalendo zaidi, yaani wao wanachotaka wachezaji wa Kibongo wacheze ili kupatikana kwa wachezaji wengi kwenye kikosi cha timu ya taifa.

Wako sana, lakini kama wakienda mbali zaidi watagundua kuwa pamoja na uzalendo wao, lakini hata wanaotaka wageni wawe wengi kwenye ligi ambao wanaonekana kama hawana uzalendo, lakini nao pia wanalitakia mema soka la nchi hii.

Binafsi mimi naona kuwa kuwapunguza wachezaji wa kigeni kwenye ligi ni sawa na wakazi wa kijiji fulani kutaka kuwaondoa wanafunzi wa kijiji kingine kwa sababu tu wana akili darasani kwa kuhofia watoto zao wasifaulu.

Hapo hata kama wataondolewa na watoto wa kijiji hicho watafaulu, lakini hataenda mbali kwa sababu wamefaulu katikati ya wanafunzi wasio na uwezo. Yaani wao ndiyo wana afadhali.

Cha muhimu hapo ni kuwaambia watoto wao wapambane nao, ili hata wakipasi japo mawili tu, watakuwa ni watoto wenye uwezo wa hali ya juu.

Binfasi huwa nashangaa kusikia wachezaji wa kigeni wanawabana wachezaji wa Kitanzania kupata namba.

Yaani ili wachezaji wa Kitanzania wawe bora ni kwamba wageni wapunguzwe.

Cha ajabu ni kwamba timu zisizokuwa na wachezaji wa kigeni kama Mtibwa Sugar, JKT Tanzania, Polisi Tanzania, Ruvu Shooting ambako wachezaji wote 30 wa timu nzima ni Wabongo, lakini hakuna hata mchezaji mmoja wa Taifa Stars, au mmoja ama mawili tu.

Na huko kwenye wachezaji wengi wa kigeni ambako tunasema kuwa wanawabana wazawa kama Simba, Yanga na Azam, ndiko kuna wachezaji wengi wa timu ya taifa.

Sasa unajiulizwa wanabanwa vipi? Lakini ukweli ni kwamba wanapokuwa kunapokuwa na wachezaji wa kigeni, kunawafanya wachezaji wa Kibongo kufanya bidii ya mazoezi kupambania namba na hapo ndipo wanapopatikana wachezaji bora wa kuichezea Stars na si bora wachezaji.

Ukimuona Mbongo anapata namba mbele ya wachezaji wa kigeni, ujue huyo ana sifa zote wa kuichezea timu ya Taifa ya Tanzania.

Kingine ni kwamba tusijidanganye, Tanzania kuna idadi kubwa ya wachezaji wa kigeni kama tunavyofikiria, ila tatizo letu tunaziangalia timu za Simba, Yanga na Azam tu.

Timu zinazobaki hazifiki hata sita zenye wachezaji wa kigeni na hazisajili idadi hiyo ya wachezaji 10, hivyo hakuna ulazima wa kuwapunguza.

Ina maana tunataka Ligi ya Tanzania kuwe na wachezaji 25 au 30 wa kigeni mbele ya wachezaji zaidi ya 500 wa Kibongo?

Lazima tujiulize, timu 20 za Ligi Kuu, zinaruhusiwa kusajili wachezaji 30, hivyo jumla ya wachezaji wote idadi yao ni 600.

Mfano kila timu kati ya hizo 20, isajili wachezaji 10 wa kigeni ingawa si kweli, kunakuwa na wachezaji 200 kutoka nje.

Wachezaji 600, ukitoa 200 wa kigeni hapo Wabongo wanabaki 400, hivi nchi inashindwa kupata kikosi cha timu ya Taifa, Taifa Stars kwa idadi hiyo ya wachezaji 400?

Tukirudi kwenye takwimu ni kwamba Simba iliingia Robo Fainali ya Ligi ya Mabingwa, idadi ya magoli 18 yaliyofunga, 15 yalifungwa na wachezaji wa kigeni.

Hata msimu uliopita, Yanga na Azam zilipocheza michuano ya kimataifa, magoli yao yalifungwa na wachezaji wa kigeni kina Richard Djodi, Sadney Urhkob, Juma Balinya na Papy Tshishimbi.

Hapa inaonyesha kuwa ili kufanya vema kwenye michuano ya kimataifa, ni lazima klabu za Tanzania ziwe na wachezaji wa kutosha wa kigeni, na kuchanganya na wa Kitanzania wenye uwezo, wala hakuna siasa katika hili.

Kwa soka la kisasa, hakuna klabu yoyote duniani inayoweza kufanya vizuri ikiwa na wachezaji wa nchini mwao tu.

Hata klabu za Afrika Kaskazini maarufu kama Waarabu ambao zamani walikuwa na idadi kubwa ya wachezaji wa nchini mwao wamebadilika.

Vyama za soka vya nchi za Misri, Morocco, Algeria, Tunisia na Libya wameanzisha mpango wa kutowahesabu wachezaji wanaotoka kwenye nchi hizo kama wa kigeni.

Ina maana Al Ahly ya Misri ikiwa na wachezaji kutoka Morocco na Tunisia, hawahesabiki kama wa kigeni, hivyo nchi hizo kwa sasa zina uwanja mpana sana wa kuchukua wachezaji kutoka nje ya nchi kwa sababu tu klabu zao zifanye vema na kukuza soka nchini mwao, lakini kuwafanya wachezaji wa nchi zao kupata changamoto kutoka kwa wachezaji wengine ili kuimarika.


SHIRIKA LA NYUMBA LA TAIFA

NHC
SHIRIKA LA NYUMBA LA TAIFA
TUNAJENGA TAIFA LETU

## TANGAZO KWA WAPANGAJI WA NYUMBA ZA SHIRIKA LA NYUMBA LA TAIFA

Shirika la Nyumba la Taifa (NHC) linapenda kuwatangazia Wapangaji na umma kwa ujumla kuwa limeanza zoezi la kuhakiki Wapangaji wake wote nchi nzima. Zoezi hili limeanza wiki hii na litaendelea muda wote hata siku za mwisho wa wiki na sikukuu ili liweze kukamilika mapema mwezi Machi 2020.

Ili kulifanya zoezi hili kuwa na mafanikio makubwa, Wapangaji wote wanatakiwa kutoa ushirikiano kwa Maafisa wa Shirika ambao muda wote watakuwa wamevaa vitambulisho vya kazi. Maafisa hao wa Shirika watapita majumbani au sehemu za biashara ili kuhakiki wapangaji hao kwa lengo la kuboresha taarifa zao.

Wakati wa uhakiki huu, wapangaji wanatakiwa kuwa na nyaraka za utambulisho ambazo ni:-

1. Mkataba wa Upangaji ulio hai
2. Stakabadhi ya malipo ya kodi ya pango ya mwezi husika
3. Nakala ya kitambulisho cha NIDA au kitambulisho cha Mpiga Kura, Hati ya kusafiria na au leseni ya Udereva iliyo hai kwa wapangaji wasiokuwa na vitambulisho vya NIDA.
4. Nyaraka za utambulisho na uthibitisho wa uhai wa kampuni ama taasisi husika kama vile leseni, memorandum and articles of association, and Cerificate of Incorporation.)
5. Stakabadhi ya malipo ya 'nominal rent" ya mwezi husika, Hati ya Upangaji ya muda mrefu "long term lease" ama sub title na nyaraka nyingine yoyote inayothibitisha umiliki binafsi (ex-owners na tenant purchasers).

Shirika linatoa rai kwa kila mpangaji ahakikishe amehakikiwa ili kuepuka usumbufu utakaoweza kujitokeza baada ya zoezi la uhakiki kukamilika. Ni matumaini yetu kuwa wapangaji wote watashiriki zoezi hili kikamilifu.

IMETOLEWA NA:
KITENGO CHA MAWASILIANO NA HUDUMA KWA JAMII NHC MAKAO MAKUU



SHIRIKA LA NYUMBA LA TAIFA

NHC
SHIRIKA LA NYUMBA LA TAIFA
TUNAJENGA TAIFA LETU

## TAARIFA KWA UMMA

Shirika la Nyumba la Taifa linawashukuru wapangaji wake waliokamilisha kulipa kodi na malimbikizo waliokuwa wakidaiwa na Shirika. Aidha, Shirika linawapongeza wapangaji wengine waliokuwa wakidaiwa ambao wamefika katika Ofisi mbalimbali za Mikoa ya Shirika kuomba muda wa kukamilisha kulipa kodi na malimbikizo yao wanayodaiwa.

Hata hivyo, Shirika linapenda kuwatangazia wapangaji wake wote ambao bado wana malimbikizo na wale wote waliohama na madeni wakiwamo watu binafsi, taasisi za umma, wakala za serikali na kampuni binafsi kuwa majina ya wadaiwa hao sugu yataanza kutolewa kwenye vyombo vya habari kuanzia Februari 17, 2020. Baada ya majina ya wadaiwa sugu kutangazwa kwenye vyombo vya habari, Shirika litaanza mara moja kuchukua hatua za kisheria dhidi yao.

Kwa wale wanaofahamu kwamba upangaji wao ulipatikana kwa njia zisizo sahihi wanapaswa kutoa taarifa Makao Makuu ya Shirika ili waweze kuhalalishwa kwa kupewa upangaji.

Epuka usumbufu lipa kodi kwa wakati

**Imetolewa na:**

OFISI YA MAWASILIANO KWA UMMA NA HUDUMA KWA JAMII NHC- MAKAO MAKUU

# Walimu waonywa rushwa uchaguzi

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WAKATI Chama cha Walimu Tanzania (CWT) kikianza kufanya uchaguzi Februari 15 hadi Mei mwaka huu, wagombea katika nafasi mbalimbali wameonywa kutojihusisha na vitendo vya rushwa au kugombea kwa misingi ya kisiasa.

Onyo hilo lilitolewa jana na Katibu Mkuu wa chama hicho Taifa, Mwalimu Deus Seif, alipokuwa akitoa taarifa ya uchaguzi huo katika ngazi zote kwa waandishi wa habari jijini Dodoma.

"Kwa mujibu wa katiba ya CWT, kufanya chaguzi zetu kila baada ya miaka mitano, hivyo mwaka huu ni mwaka wa uchaguzi wa chama chetu na leo tumekuja hapa kuwahamasisha walimu na kutoa utaratibu unaohitajika kwa wanachama wetu," alieleza Seif.

Vilevile, alisema kuwa pamoja na kuwa kila mwanachama ana haki ya kugombea, kuchagua na kuchaguliwa, lakini ni lazima kufuata misingi na maadili ambayo yanatambuliwa kikatiba.

Alisema kuwa wanachama wanatahadharishwa kuwa makini katika kipindi chote cha uchaguzi na kuepuka kabisa kutumia njia ya rushwa au kutoa ahadi zisizotekelezeka ili kupata kura.

"Yeyote atakayekiuka maadili ya chama kuhusu uchaguzi atachukuliwa hatua za kinidhamu ikiwa ni pamoja na kunyang'anywa ushindi ikiwa ameshinda," alisema katibu huyo.

Akielezea ratiba ya uchaguzi huo Seif, alisema kuwa kwa ngazi ya tawi utafanyika kuanzia tarehe 15 hadi 27 mwezi huu ambapo itahusisha shule, vyuo vya ualimu (TTC) na vyuo vya maendeleo ya jamii (FDCs).

Pia alisema uchaguzi huo utafanyika katika wizara na taasisi mbalimbali zenye wanachama pamoja na zilizopo ngazi ya wilaya zinazojumuisha ofisi za elimu za wilaya na waratibu wa elimu ngazi za kata.

Akizungumzia uchaguzi huo katika ngazi ya wilaya, alisema uchaguzi utafanyika kuanzia Machi 16 hadi 27, 2020, ambapo uchukuaji fomu na urejeshaji utapangwa na kamati ya uendeshaji ya wilaya husika.

Alisema kwa ngazi ya Mkoa itakuwa ni kuanzia Aprili 20 hadi 30, 2020, na uchukuaji fomu na urejeshaji utapangwa na kamati ya uendeshaji ya mkoa husika.

Kwa ngazi ya Taifa, Seif, alisema kuwa uchaguzi utafanyika Mei 28, mwaka huu na kueleza kuwa wagombea wote watajulishwa mahali pa mkutano mkuu kabla ya mkutano wa uchaguzi.

Aidha, alisema kuwa vitengo vya walimu wanawake na wenye ulemavu vitafanya chaguzi zao tarehe 27 Mei 2020, na mwisho wa kurudisha fomu kwa wagombea nafasi za kitaifa ni tarehe 24 Aprili mwaka huu saa 10:00 jioni makao makuu ya chama hicho, Taifa jijini Dodoma.

Akizungumzia juu ya hali ya chama Rais wa CWT, Leah Ulaya, alisema kuwa chama kimekuwa na mafanikio ikiwa ni pamoja na ujenzi wa ofisi 50 za wilaya kwa Tanzania Bara.

Mafanikio mengine alisema ni walimu kupandishwa madaraja na serikali kulipa madeni na malimbikizo huku kilio cha kukosekana kikiwa kimepungua.




Mkurugenzi wa Masoko wa Benki ya Biashara ya DCB, James Ngaluko (katikati), Mkurugenzi Mtendaji wa benki hiyo, Godfrey Ndalahwa na Mkurugenzi wa Masoko, Rahma Ngassa (kulia), wakati wa uzinduzi wa DCB Skonga jijini Dar es Salaam. Habari Uk. 24.
**PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Bashiru aonya wanaoitishia CCM

**INATOKA UK. 2**

Temba, wa Kata ya Kihonda Maghorofani.

Madiwani hao wameeleza wameamua kujiunga na CCM ili kumuunga mkono Rais Magufuli kutokana na kuwaletea maendeleo wananchi.

**WANAOANZA KAMPENI MAPEMA KUFYEKWA**

Chama hicho pia kimeonya wagombea wa viti vya udiwani na ubunge watakaoanza kampeni kabla ya muda na kutoa zawadi kuwa majina yao yatakatwa.

Makamu Mwenyekiti wa chama hicho Tanzania Bara, Philip Mangula, alitoa tahadhari hiyo jana wakati akizungumza na wajumbe wa Halmashauri Kuu na Kamati za Siasa za CCM Mkoa wa Shinyanga, kuwa wagombea wote wanapaswa kufuata kanuni na maadili ya chama.

Alisema chama hicho kina kanuni na taratibu zake na kuonya wagombea wote ambao wana nia ya kugombea nafasi za uongozi kwenye uchaguzi mkuu wa mwaka huu, watakaoanza kampeni kabla ya muda watafyeka majina yao.

"Kwenye uchaguzi mkuu wa mwaka huu, tunataka taratibu, kanuni na maadili yafuatwe kwenye kugombea nafasi za udiwani na ubunge, wale ambao wataanza kampeni kabla ya muda pamoja na kutoa vizawadi tutafyeka majina yao, msubiri muda ukifika ndipo muanze kujinadi," alisema Mangula.

"Tunataka nidhamu ndani ya chama na hakuna jamii ambayo haina taratibu namna ya kuishi, hivyo kamati za siasa chungeni sana wagombea ambao wataanza kufanya kampeni kabla ya muda wachukulieni hatua na mkishindwa sisi tutaiwajibisha kamati nzima," aliongeza.

Pia aliwataka wana-CCM kuendelea kushikamana na kuwa wamoja hasa kwenye kipindi cha kuelekea kwenye uchaguzi mkuu, pamoja na kuhamasisha wananchi wajitokeze kupiga kura ili chama kipate ushindi wa kishindo kuliko wa mwaka 2015 wakati chama kilivurugika.

Naye Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Shinyanga, Mabala Mlolwa, alimhakikishia Mangula kuwa chama kimejipanga vizuri na hakuna hata kiti kimoja watakachokipoteza kuanzia nafasi ya udiwani na ubunge, huku akiahidi kutekeleza maagizo ambayo ameyatoa ikiwamo wagombea kutoanza kampeni kabla ya muda.

Baadhi ya wabunge mkoani Shinyanga akiwamo Ahmed Salum wa Jimbo la Solwa, alimpongeza Rais John Magufuli kwa kazi nzuri ya kutekeleza ahadi nyingi za wananchi kwa asilimia kubwa na wananchi kuendelea kuwa na imani na CCM.

**■Taarifa imeandikwa na Ashton Balaigwa (Morogoro) na Marco Maduhu (Shinyanga)**

## Watanzania waondolewa hofu corona

**INATOKA UK. 3**

Arumeru, amekuwa akijitangaza kuwa ana dawa ya kutibu ugonjwa huo wa virusi vya corona na kuweka mawasiliano yake kwenye mitandao.

Dk. Ndugulile alitahadharisha kuwa mtu yeyote anayetoa tiba asili na mbadala lazima asajiliwe na mamlaka husika ambayo ni Wizara ya Afya, lazima dawa zake ziwe zimesajiliwa na Wizara ya Afya na kusisitiza kuwa nabii huyo pia anapaswa kuthibitisha amesajiliwa wapi na lini.

"Tuepuke kutoa kauli ambazo zinakwenda kuchanganya jamii, na endapo tutabaini mtu huyu hana sifa ambazo anasema kuwa nazo tutamchukulia hatua za kisheria," alisema.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Arusha, Jonathan Shana, alisema kuwa jeshi hilo lilimkamata na kumpeleka kwa Mganga Mkuu kwa ajili ya kumuhoji kama kweli ana dawa hizo.

"Sisi tulimkamata na kumpeleka kwa Mganga Mkuu ili amuhoji na kumwangalia kama ana vibali vya kugawa hiyo dawa na nifafanue sisi tulimchukua na kumpeleka kwa Mganga Mkuu hatumshikilii," alisema Shanna.

HABARI KITAIFA

# Mkurugenzi aona shida matumizi ya kondomu

**Na Elisabeth Zaya**

MKURUGENZI wa Biashara na Huduma za Kijamii kutoka Shirika la T-MARC Tanzania, Flavian Ngole, amewahimiza Watanzania juu ya umuhimu wa matumizi sahihi ya mipira ya kuzuia maambukizo ya Virusi vya Ukimwi (VVU) ili kupambana na maambukizo hayo.

Pia, amewashauri wanawake kutumia ushawishi walionao katika kuhamasisha jamii juu ya matumizi sahihi ya mipira hiyo.

Ngole alisema hayo mwishoni mwa wiki katika maadhimisho ya kimataifa ya kukuza uelewa juu ya kondomu na kuelimisha jamii kuhusu umuhimu wa ngono salama muda wote.

Alisema shirika hilo limekuwa likitumia njia za kibunifu kuwafikia Watanzania hususani wale ambao wahajafikiwa na huduma muhimu kupitia njia za utolewaji wa huduma na bidhaa za kijamii na mawasiliano.

Alisema matumizi ya mipira hiyo yanatakiwa kuwa kwa makundi yote ikiwamo watu wenye ulemavu, lengo likiwa ni kuwalinda wenza wao katika kupata maambukizo ya magonjwa mbalimbali.

Kuhusu mwanamke kuwa chachu ya matumizi ya kondomu, Meneja Utawala na Logistiki wa taasisi hiyo, Geraldine Duwe, alisema ipo haja ya kuondoa taswira katika jamii kwamba watu wanaonunua mipira hiyo wana tabia za kihuni.

"Watu wawe na uelewa sahihi wa matumizi ya kondomu, ipo haja kuhamasisha juu ya uhusiano mzuri na salama na kuwakumbusha watu juu ya hatari ya magonjwa yanayoambukizwa kwa ngono na mimba zisizopangiliwa," alisema.



Baadhi ya wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Bajeti pamoja na maofisa wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) wakimsikiliza Ofisa wa Kampuni ya Sigara Tanzania (TCC Plc.), Phibert Fidel (wa tatu kulia), alipokuwa akifafanua kuhusu moja ya bidhaa za sigara zinazozalishwa na kampuni hiyo wajumbe hao walipofanya ziara hivi karibuni ili kufahamu ufanisi wa mfumo wa stempu za kodi za kielektroniki unaotumiwa na kampuni hiyo. **MPIGAPICHA WETU**

# TIC yatoa neno kwa wawekezaji

**Na Mwandishi Wetu,** MBOZI

KITUO cha Uwekezaji Tanzania (TIC), kimesema kimejipanga kuhakikisha kuwa wawekezaji wote wanajisajili kwenye kituo hicho ili kupata fursa na taarifa mbalimbali za kiuwekezaji, kisheria na msaada wa huduma za kikodi sambamba na kupata cheti.

Akizungumza mkoani Songwe kwenye kongamano kubwa la siku tatu la uwekezaji linalofanyika viwanja vya michezo vya CCM katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbozi-jana, Mratibu wa Idara ya

Huduma za Uwekezaji wa TIC, Aboubakar Ndwata, alisema kuna umuhimu na faida kubwa kwa wawekezaji kujisajili kwenye kituo kicho.

"TIC ni chombo pekee cha kuratibu uwekezaji nchini hivyo tuna kazi kubwa kuhakikisha elimu inawafikia wawekezaji wa ndani, nje na wananchi kiujumla juu ya mazingira ya uwekezaji na faida watakaozipata wanapojisajili TIC," alisema Ndwata.

Alisema katika Mkoa wa Songwe, TIC itajikita zaidi kuwaelimisha wananchi pamoja na wawekezaji juu ya mazingira ya uwekezaji nchini na umuhimu wa kuzingatia kanuni na sheria na taratibu za uwekezaji.

Ndwata alisema kongamano la uwekezaji Songwe lina umuhimu mkubwa katika kuvitangaza vivutio mbalimbali vilivyopo mkoani hapo kwenye sekta mbalimbali muhimu za kiuchumi na kijamiii.

"TIC kwa kushirikiana na Serikali ya Mkoa wa Songwe pamoja na wadau wengine kutoka sekta binafsi tulihakikisha tunawakutanisha wawekezaji kwa pamoja, wajasiriamali wadogo na wananchi wa mikoa ya karibu lengo likiwa kutangaza vivutio vya uwekezaji fursa zilizopo katika sekta mbalimbali za kiuchumi," alisema Ndwata.

Alisema Mkoa wa Songwe ni tajiri sana kwa fursa za kiuwekezaji, hivyo TIC kwa kushirikiana na serikali ya mkoa na wadau kutoka sekta binafsi watashirikiana kuzitangaza fursa hizo.

"Niwaombe wawekezaji, wafanyabiashara na wananchi wote wa Mkoa wa Songwe kuchangamkia fursa lukuki zilizopo katika mkoa huu zikiwamo kwenye sekta za kilimo, ufugaji, utalii, ufugaji, madini na viwanda ili kujikwamua kiuchumi," alisema.

Mkuu wa Mkoa wa Songwe Brigedia Generali mstaafu Nicodemus Mwangela, aliwashukuru wawekezaji, wafanyabiashara, wajasiriamali na wananchi kwa kujitokeza kwa wingi kwenye kongamano hilo na kuwataka kuendelea kufika kwa wingi kutangaza biashara zao na kuona bidhaa zingine zinazoonyeshwa ili waweze kukuza biashara zao.

"Uwekezaji mzuri unaanzia nyumbani kwa hiyo wawekezaji wa kwanza ni sisi wananchi wa Mkoa wa Songwe, hivyo tujitokeze kwa wingi tuje tutumie fursa hii kuona nini tunazalisha na nini tunauza," alisema Mwangela.

Aliwaomba pia wafanyabiashara, wawekezaji wa kitaifa na kimataifa wafike kwa wingi katika kongamano hilo ili kufahamu undani mazingira rafiki yaliyopo kwa ajili ya uwekezaji katika mkoa wa Songwe, ukizingatia ni lango la biashara kwa nchi za SADC.

Alisema kwa zaidi ya asilimia 70 ya mizigo kwenda Bandari ya Dar es Salaam hupita katika mpaka wa Tunduma kuingia nchini, hivyo soko la bidhaa zitakazozalishwa mkoani Songwe litakua pana zaidi.

# Repoa yang'ara kimataifa

**Na Elizabeth Zaya**

TAASISI inayoshughulika na masuala ya utafiti (Repoa), imeng'ara kwa kushika nafasi ya 11 kati ya taasisi 612 zinazofanya kazi hiyo barani Afrika.

Repoa imeendelea kushikiria nafasi hiyo ya juu kwa miaka sita mfululizo kwa Tanzania na kuzipita taasisi nyingine zinazofanya shughuli hizo.

Ripoti hiyo ilitolewa mwishoni mwa Januari mwaka huu jijini Washington DC, Marekani na Taasisi ya Kitafiti ya Kimataifa ya Global Think Tanks (TTCSP).

Akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam, Mkurugenzi Mtendaji wa Repoa, Dk. Donald Mmari, alisema taasisi yao imefanikiwa kushikilia nafasi hiyo ya 11 tangu mwaka 2017, kati ya taasisi hizo 612 barani Afrika.

"Mafanikio haya katika taasisi yetu yametokana na kuaminiwa na kutumika kwa kazi ambazo tumekuwa tukizifanya na kuleta manufaa katika taifa letu," alisema Dk. Mmari na kuongeza:

"Tunaishukuru sana serikali yetu kwa kutuamini na kwa kuona kwamba kazi zetu ni bora za kuaminika na kuendelea kuzitumia kwa kuona umuhimu wake."

Pia alisema mpango kazi mpya wa miaka mitano ijayo wamepanga kuboresha zaidi kazi zao hususani kwa kutilia mkazo katika mambo makuu matatu.

Aliyataja ni katika ukuaji wa uchumi, katika maendeleo ya jamii na matakwa ya kidunia katika kutekeleza malengo endelevu (STGs).

Eneo jingine watakaloliangalia ni jinsia na maendeleo ya binadamu hususani katika afya na mifuko mbalimbali ya kusaidia jamii.

"Tunaangalia kwa kina na namna ya kutoa ushauri wa kisera ili tofauti za kijinsia zisiwe kikwazo kwa kukua kwa maendeleo," alisema Dk. Mmari.

Eneo la tatu alisema wataangalia utawala, uwajibikaji na ushirikishwaji wa wananchi katika shughuli za kiuchumi.

# Samia awaonya viongozi CCM, serikali Pwani

**Na Khadija Kalili,** KIBAHA

MAKAMU wa Rais, Samia Suluhu Hassan, amewapa karipio kali viongozi wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) na wa Serikali mkoani Pwani baada ya kupata taarifa kwamba wamekuwa wakisigana na kujengeana chuki.

Samia ambaye ni Mjumbe wa Kamati Kuu ya CCM, amewataka kuacha tabia ya chuki na kuwa kitu kimoja, huku akiwataka kuunganisha nguvu moja katika kipindi hiki cha kuelekea uchaguzi mkuu wa baadaye mwaka huu.

"Ninazo taarifa kuwa kuna msuguano ndani kwa ndani kati ya viongozi wa chama na viongozi wa serikali, sasa nawaomba kila mmoja ajipime mwenyewe misuguano hii haina tija zaidi ya kutugawa," alisema na kuongeza:


"Mna maugomvi pia, wapo watu ambao wameanza kujipitisha pitisha mapema, leo nawaapia kuwa tutawakata majina yenu mapema... anayejipitisha mapema tunakuona, tutakushughulikia mapema na pesa yako utakayotoa ya kuchukulia fomu utakuwa umechangia chama kutunisha mfuko wake." Aliyasema hayo alipokuwa mgeni rasmi kwenye sherehe za miaka 43 ya kuzaliwa kwa CCM Kibaha mkoani Pwani.

"Tusizushiane majungu, pia nipende kusema kuwa kamati za siasa wamepewa onyo kali kutowaogopa wale watu ambao wanaonekana kuwa ni tishio kwa kuwawekea alama nyingi, acheni chuki nasisitiza acheni chuki miongoni mwenu," alisema.

Aliatoa wito kwa wakazi wa mkoa wa Pwani kujipanga kibiashara ilikujinasua katika dimbwi la umaskini, pia amewahimiza kusoma kwa bidii.

Alisema kuwa ifikapo Aprili mwaka huu changamoto ya usafiri ya muda mrefu kwa wakazi wa Wilaya ya Mafia itatatuliwa na kubaki historia.

Akizungumza kuhusu mgogoro wa eneo la soko la Mlandizi, alisema kuwa wamekuta kuna pande mbili zinazovutana jambo linalokwamisha maendeleo, hivyo ili kila mmoja aweze kupata haki yake, aliagiza Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru) walifanyie kazi.



Naibu Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania (BoT), Dk. Bernard Kibesse (kushoto), akilakiwa na Mwenyekiti wa Bodi ya Absa Tanzania, Simon katika hafla iliyoandaliwa na benki hiyo kwa wateja wake jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. Kulia ni Mkurugenzi Mtendaji wa Absa wa Kanda, Saviour Chibiya na Mkurugenzi Mtendaji wa Absa Tanzania, Abdi Mohamed. **PICHA: MPIGA PICHA WETU**

# Viongozi watakiwa kuwa mfano uchumi wa kati

**Na Elizabeth Zaya**

KATIBU Mkuu, Ofisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Zanzibar, Yakout Hassan Yakout, amesema viongozi wanatakiwa kuwa mfano bora kwa kufanya kazi kwa bidii na kutimiza azma ya serikali ya kufikia uchumi wa kati.

Alitoa kauli hiyo jijini Dar es Salaam wakati akifunga kozi fupi ya nane ya uongozi ya mwaka 2020 kwa viongozi kutoka Tanzania Bara na Zanzibar inayotolewa na Chuo cha Taifa cha Ulinzi Tanzania (NDC).

Alisema ni wajibu wa kiongozi kujitathmini kila mara juu ya utendaji wake wa kazi ikiwamo kufanya maamuzi sahihi na chanya kwa jamii na kwa taifa.

"Naomba mafunzo mnayopata yatatue changamoto zinazokabili taifa na zitakazojitokeza hususani zinazohatarisha usta- wi wake, usalama wa taifa, wa watu na mali zao, na kuzingatia kufanya maamuzi sahihi yanayogusa maslahi ya jamii," alisema Hassan Yakout. "Serikali zetu zinataka kuona viongozi wenye mashiko katika nchi na ndiyo maana viongozi wakuu wanasisitiza kila siku tuchape kazi, mnatakiwa mkawe mafuta ambayo yakichanganywa na maji yanajitenga, tunataka muwe chachu ya maendeleo."

Akizungumza katika hafla hiyo, Mkuu wa NDC, Luteni Jenerali Peter Massao, alisema mafunzo hayo yameshirikisha viongozi wa ngazi za juu wa serikalini na taasisi zake kutoka Tanzania Bara na Zanzibar.

Alisema lengo la mafunzo hayo ni kuwajengea uwezo wa misingi bora ya kiutendaji, namna ya kukabiliana na changamoto za uongozi, kufanya maamuzi kwa usahihi na weledi kwa mambo yanayohusu serikali na usalama wa taifa na kusimamia maadili na uzalendo katika taifa.

Pia alisema mafunzo hayo yamekuwa yakifanyika kwa viongozi mbalimbali na yamesaidia kwa kiwango kikubwa kuleta ufanisi kwa viongozi hao.

# Wananchi wa vijiji 11 wamlilia Waziri Lukuvi

**Na Mwandishi Wetu,** MBARALI

WANANCHI wa vijiji 11 wa Wilaya ya Mbarali mkoani Mbeya wenye mgogoro wa muda mrefu na mbunge wao, Pirmohamed Mulla, wamemwomba Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, William Lukuvi kuwatembelea ili kupata undani wa sakata hilo.

Wakizungumza na Nipashe, viongozi wa wananchi hao, Patrick Mnyota na Oswald Mndeva, walidai Waziri Lukuvi amepewa ripoti potofu na watendaji wake ngazi ya wilaya na mkoa wanaompendelea Mulla ambaye kampuni yake, Highland Estate Limited ndiyo mhusika mkuu wa mgogoro huo.

"Kwa niaba ya wananchi wa vijiji vyote 11 vilivyoathirika na mgogoro huu, tunamwomba Waziri Lukuvi aje atutembelee ili tumpe ushahidi wa nyaraka kuhusu madai yetu," alisema mwenyekiti wa kamati ya waathirika hao.

Alidai mgogoro huo ambao wameshaufikisha mpaka Ikulu kwa Rais John Magufuli, umeshindwa kutatuliwa kwa sababu viongozi wa Wilaya ya Mbarali na Mkoa wa Mbeya wanasikiliza watendaji wao ambao ni washirika wa karibu wa Mulla.

"Kilio chetu sisi ni kurudishiwa ardhi yetu ambayo Highland Estate Limited imechukua kama sehemu ya ardhi ya Nafco baada ya ubinafsishaji," alisema Katibu wa Kamati hiyo Mndeva.

Hivi karibuni Waziri Lukuvi aliliambia gazeti dada la Nipashe, The Guardian kwamba wananchi hao hawahusiki na ardhi aliotwaa Rais Magufuli kutoka kwa mwekezaji mwezi Mei mwaka jana alipofanya ziara wilayani Mbarali, lakini alikiri kwamba suala lao analielewa.

"Hao wananchi suala lao linashughulikiwa na uongozi wa wilaya na mkoa na siyo wanufaika wa ardhi iliyotwaliwa na Rais Magufuli," Lukuvi alisema na kusisitiza kwamba wananchi hao waendelee kushirikiana na viongozi wa wilaya na mkoa kumaliza mgogoro huo uliodumu tangu mwaka 2014.

Mbunge Mulla, alikanusha kuhusika na uporaji wa ardhi hiyo akidai ni sehemu halali ya Nafco iliyonunuliwa na Highland Estates Limited wakati wa ubinafsishaji mwaka 2014.

"Kampuni inakujulisha kuwa, mipaka kwenye shamba la Highland Estates Limited-Mbarali haikuwekwa na mwekezaji isipokuwa imewekwa na serikali," alisema Mulla ambaye ni Mkurugenzi wa HEL kwenye barua yake ya Desemba 6, 2017, akiwajibu wananchi hao.

Vijiji 11 vilivyoathirika na mgogoro huo ni Nyeregete, Ibohola, Mbarali, Ubaruku, Utyego, Mayota, Warumba, Urinda, Ibumila, Imalilosongwe na Mwanavala.

# CCM yaagiza kijiji ujenzi ofisi ya walimu Babati

**Na Jaliwason Jasson,**
MANYARA

KAMATI ya Siasa ya Wilaya ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) Babati mkoani Manyara, imeagiza Serikali ya Kijiji cha Minjingu kujenga ofisi ya walimu katika Shule ya Msingi Minjingu, ili walimu wasitumie darasa.

Kujengwa kwa ofisi hiyo, pia kutasaidia walimu wa shule hiyo kutokufanyia shughuli zao chini ya miti.

Agizo hilo lilitolewa mwishoni mwa wiki na kamati hiyo, wakati wa ziara ya kukagua miradi ya maendeleo wilayani humo.

Katibu wa CCM wa Wilaya ya Babati, Filbert Mapwepwe, alimtaka mwenyekiti wa kijiji hicho kukaa na serikali yake na kuangalia namna ya kuwajengea walimu ofisi ili wasitumie darasa kama ofisi ya kufanyia kazi. "Nitakuja hapa tena Aprili kuangali kama mmeshaanza ujenzi wa ofisi hiyo, maana wanafunzi hawawezi kuteseka kwa kukaa chini kutokana na walimu wanatumia darasa lao kama ofisi," alisema Mapwepwe.

Baada ya kutoa maagizo hayo, walikagua madarasa matatu na matundu ya vyoo 24, ambayo wamejengewa na Jumuiya ya Hifadhi ya Wanyamapori (JUHIBU).

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Babati, Nicodemus Tarimo, alishangazwa na walimu kuligeuza darasa kuwa ofisi yao.

Tarimo alisema kilichokwamisha ujenzi ni wananchi kukaidi kuchangia.

Alisema Juhibu watoe fedha za ujenzi, wananchi wa Minjingu hawakuridhika na walikataa kutoa fedha za ujenzi bila sababu maalumu.

Mjumbe mwingine wa kamati hiyo, Michael Tsaxara, alisema walimu kutumia darasa kama ofisi hawawatendei haki kwa wanafunzi.

Mapema akisoma taarifa ya ujenzi huo, Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Minjingu, Veronica Kweka, alisema mradi huo una thamani ya Sh. milioni.249.6 na fedha zilizotumika hadi sasa ni Sh. milioni. 234.

Kweka alisema shule hiyo ina walimu 17 na wanafunzi 1,000, kuanzia darasa la awali mpaka darasa la saba.

Mwalimu Idrisa Msemo, alisema shule hiyo, ina upungufu wa majengo ya utawala ndio maana wametumia darasa kama ofisi ya kufanyia shughuli zao. Naye Mwenyekiti wa Kijiji hicho, Samuel Melam, alikiri walifanya makosa kwa kutumia darasa kama ofisi ya walimu wakati wanafunzi wana uhaba wa madarasa. Aliahidi kamati hiyo, kuwa watatafuta fedha haraka ili wajenge ofisi ya walimu.



Mbunge wa Uturuki ambaye ni Mjumbe wa Bodi ya Wadhamini wa Mfuko wa Turkish Maarif Foundation (TMF), Profesa Cihad Demirli (katikati), akiwa na Mbunge mwenzake Huseyin Sanverd (kushoto) pamoja na Balozi wa Uturuki nchini, Ali Davutoglu, wakipanda mti jana kwenye eneo la shule ya watoto yatima na wanaoishi kwenye mazingira magumu ya Turkish Maarif inayoendeshwa na shirika hilo, jijini Arusha jana. **PICHA: DANIEL SABUNI**

# Watakaofaulu vizuri kupewa vifaa umeme

**Na Cynthia Mwilolezi,**
ARUSHA

KAMPUNI ya kuzalisha vifaa vya umeme wa jua ya Zola, imeahidi kuwazawadia vifaa vya nishati ya umeme wa jua, wanafunzi wa kidato cha nne watakaofaulu vizuri mwaka huu, ili kuwaongezea chachu ya kujisomea zaidi.

Akitoa ahadi hiyo wakati wa uzinduzi wa ofisi ya Zola mkoani Arusha, Mkurugenzi wa Kampuni ya Zola Afrika Mashariki, Yusuph Nassor, alisema serikali imejitolea kuwasaidia watoto kielimu kwa kutoa elimu bure, hivyo wameunga mkono jitihada hizo.

"Sisi tunaamini elimu ndio urithi mzuri hakuna urithi mwingine kama huu, hivyo tumeona ni vema tuwape zawadi ya vifaa vyetu vya Zola kwa kila atakayefaulu vizuri kwa kidato cha nne, vifaa hivyo ni taa, feni na kompyuta na vifaa hivi vitawasaidia katika masomo yao," alisema.

Nassor alisema mbali kampuni hiyo, kusaidia sekta ya elimu, pia watatoa gawio la faida kwa ajili ya kusaidia sekta ya afya na nyingine.

Naye Mkuu wa Wilaya ya Longido, Frack Mwaisumbe, akizungumza kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa wa Arusha, Mrisho Gambo, aliipongeza kampuni hiyo, kwa kuamua kuisaidia serikali katika sekta ya elimu. "Kwa kutoa zawadi hizi kutachangia kuinua kiwango cha elimu na watoto watasoma kwa ushindani na kuinua mkoa wetu kielimu," alisema.

Mwaisumbe alisema baada ya zawadi hizo, kutolewa matarajio yake Mkoa utafanya vizuri kitaifa zaidi ya mwaka jana 2019, uliposhika nafasi ya tatu katika matokeo ya kidato cha nne.

Pia ameipongeza kampuni hiyo kwa kuajiri vijana wengi wa kitanzania kwa kufanya hivyo, wameonyesha moyo wa kizalendo.

Balozi wa Kampuni ya Zola, Idris Sultan, aliahidi kuitangaza zaidi kampuni hiyo, kwa wananchi hususan wale wanaoishi vijijini, ili wapate fursa ya kutumia nishati ya umeme wa shirika hilo.

"Wengi hawajui umeme huu wa jua, lakini nitatangaza popote niendapo ili watu wauelewe umeme huu, na vijana nitawahamasisha wanapojenga nyumba zao, wawe na miundombinu ya Zola, kwa kuwa hata wakiwa na umeme wa Tanesco haizuii kutumia umeme huu kwa faida zao," alisema.

# Mzumbe kujengea kijiji shule

**Na Allan Isack,** ARUSHA

CHUO Kikuu cha Mzumbe, kimeingia makubaliano na wananchi wa Kijiji cha Kiseriani Kata ya Mlangarini Halmashauri ya Arusha DC, wilayani Arumeru, kuanzisha ujenzi wa shule mpya ya sekondari Kiseriani.

Katika makubaliano hayo, Chuo Kikuu cha Mzumbe kitajenga vyumba vinne vya madarasa, ofisi za walimu, na vyoo.

Wadau hao wa elimu wamejitokeza kuchangia sekta ya elimu katika Halmashauri ya Arusha DC, kwa lengo la kuboresha na kuweka mazingira rafiki ya walimu kufundishia na wanafunzi kusomea darasani.

Ujenzi wa shule hiyo unakwenda sambamba sera ya serikali ya kuboresha sekta ya elimu na kutoa elimu bila malipo.

Ujenzi wa miundombinu hiyo, utagharimu kiasi cha Sh. milioni 150 hadi kukamilika.

Fedha za ujenzi huo zimetolewa na Chuo Kikuu cha Mzumbe kama fidia ya shamba lililotolewa na kijiji cha Kiseriani kwa chuo kikuu hicho.

Ofisa Elimu ya Sekondari Halmashauri ya Arusha DC, Medad Lupenza, alipongeza uongozi wa Chuo Kikuu cha Mzumbe na Kijiji cha Kiseriani, kwa kufanya makubaliano hayo muhimu kwa ajili ya sekta ya elimu.

Alisema makubaliano hayo yameleta mapinduzi kielimu katika eneo ambalo, awali halikuwahi kuwa na shule ya sekondari.

Alisema watoto wa Kijiji cha Kiseriani walikuwa wakitembea zaidi ya kilomita 10 kufuata huduma ya shule ya sekondari.

Ujenzi wa shule hiyo umeondoa adha kwa wanafunzi kwa wanafunzi wa kijiji hicho.

Aidha, alisema halmashauri hiyo imeanza mchakato wa awali wa kusajili shule hiyo, na baada ya mchakato kukamilika, wanafunzi wataingia shuleni hapo.

Wananchi wa kijiji hicho, wameanza ujenzi wa maabara ya masomo ya sayansi ili kukidhi vigezo vya shule kusajiliwa.





# Mkwamo zahanati wamkera Ndugulile

**Na Godfrey Mushi,** MWANGA

KUSUASUA kwa miradi ya ujenzi ya zahanati za Kileo na Lembeni katika Wilaya ya Mwanga, kumemkera Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Faustine Ndugulile, na kuagiza Mganga Mkuu wa Mkoa na Wilaya hiyo kuzungumza lugha moja ili kutafuta ufumbuzi wa tatizo hilo.

Alisema viongozi hao wanapaswa kukaa pamoja na kujadili namna ya kutatua mkwamo huo wa zahanati mbili ambazo kama zingekamilika kwa wakati zingewapunguzia adha wakazi wa kata hizo mbili kufuata huduma ya afya katika Hospitali ya Usangi iliyopo zaidi ya kilomita 20.

Dk. Naibu Waziri Ndugulile aliyasema hayo mwishoni mwa wiki, baada ya kukagua miradi hiyo ya ujenzi na kupokea malalamiko ya wananchi wa Lembeni na Kileo kuhusu kusuasua kukamilika kwa zahanati hiyo kwa miaka kadhaa sasa.

Kutokana na hali hiyo, aliagiza Mganga Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro na Mganga Mkuu wa Wilaya ya Mwanga kuhakikisha ujenzi wa zahanati za Lembeni na Kileo unakamilika mara moja ili wananchi waendelee kunufaika na huduma nzuri za matibabu zitakazokuwa zinatolewa katika zahanati hizo.

"Inawezekana hamzungumzi lugha moja, ndio maana mambo hayaendi, haiwezekani wananchi wanalalamika kwamba ujenzi wa miradi hii umechukua muda mrefu kukamilika na wala hawaelezwi sababu za msingi. Naagiza kaeni tena pamoja na mtatue tatizo hili haraka," alisema.

Akiwa katika zahanati ya Lembeni, Naibu Waziri Ndugulile alichangia mifuko 50 ya saruji kwa ajili ya kuunga mkono juhudi za wananchi katika umaliziaji wa jengo jipya la zahanati hiyo.

Wakati katika zahanati ya Kileo, Dk. Ndugulile aliagiza Ofisi ya Mganga Mkuu wa Wilaya na Mkoa wakae na kuweka mikakati mizuri ya namna ya kuendeleza mradi mpya wa jengo la zahanati ya Kileo.

# Wataka matumizi ya Tehama kwenye Saccos

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

MKURUGENZI Mtendaji wa Shirikisho la Vyama vya Ushirika vya Akiba na Mikopo Afrika (Accosca), George Ombado, ameungana na mameneja zaidi ya 50 wanaoendesha vyama vikubwa vya akiba na mikopo Tanzania (Saccos), kutaka kuanza kutumika mfumo wa matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (Tehama) katika sekta hiyo.

Mkurugenzi hiyo alisema mapinduzi ya Tehama duniani yamesaidia sekta nyingi na hasa ushirika kuongeza uwazi, ufanisi, uwajibikaji na tija katika utoaji wa huduma kwa wananchi.

Alikuwa akizungumza na mameneja hao jijini Arusha, baada ya kumalizika kwa kikao kazi cha siku tatu kilichowakutanisha kwa mara ya kwanza mameneja wa Saccos za Tanzania kilichoandaliwa na Chama Kikuu cha Ushirika wa Akiba na Mikopo Tanzania (SCCULT Ltd-1992).

Awali, Mkurugenzi Mtendaji wa SCCULT Ltd-1992, Hassani Mnyone, alisema maendeleo ya teknolojia duniani hususani eneo la Tehama yameleta mapinduzi makubwa katika upashanaji wa habari na utoaji wa huduma kwa umma.

Taarifa iliyotolewa jana na Mnyone, inaeleza kuwa mameneja hao waliridhia uamuzi huo katika kikao kazi cha pamoja kilichofanyika jijini Arusha kujadili na kubadilishana uzoefu wa masuala mbalimbali yanayohusu sekta ya ushirika.

"Azma ya kuanzisha mtandao wa mameneja wa Saccos Tanzania inalenga zaidi kuendelea kuboresha mahusiano na ushirikiano baina ya mameneja na kufanya kazi pamoja na mtandao wa wanawake kwenye ushirika wa akiba na mikopo na mtandao wa vijana," alisema mkurugenzi huyo.

Sera ya taifa ya Tehama ya mwaka 2003 pamoja na mambo mengine, inasisitiza juu ya matumizi ya fursa za Tehama katika utendaji kazi wa kila siku na utoaji huduma kwa wananchi.

Kikao hicho cha siku tatu kilifunguliwa na Mwenyekiti wa SCCULT Taifa, Dk. Gervas Machimu, ambaye alisisitizia suala la maadili na weledi kwa mameneja ambao ndio injini ya shughuli zote za Saccos.

Akizungumzia mfumo huo, Meneja wa Chama cha Akiba na Mikopo cha Wafanyakazi wa Kampuni ya TICTS (DCTW Saccos), Mary Lyimo, alisema: "Hii ni fursa ya kujifunza, kujipima na kubadilishana uzoefu na imekuja wakati muafaka, ambapo sekta ya ushirika wa akiba na mikopo inapokea mabadiliko na uelekeo mpya kutokana na mabadiliko ya sheria, sera na mazingira ya kibiashara.

"SCCULT (1992) Ltd imefanya jambo kubwa na muhimu kutukutanisha hapa kwa siku tatu."

Mambo yaliyojadiliwa kwenye kikao hicho na kutolewa maazimio ni mbinu za ufanyaji maamuzi na mahusiano kazini, matumizi na ulinzi wa mifumo ya Tehama, mahusiano ya taasisi, mabadiliko ya sheria na kanuni za huduma ndogo za fedha na uanzishwaji wa mtandao wa mameneja wa Sacoss Tanzania.

Watoa mada wakuu walikuwa ni Hassani Mnyone, Emmanuel Masaga, Prof. Frank Neumann na Josephat Kisamalala.



Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Hai mkoani Kilimanjaro, Yohana Sintoo, akitoa maelekezo juzi kwa wakuu wa idara, madiwani na wananchi wa wilaya hiyo (hawapo pichani) kutumia kituo cha redio cha Boma Fm kueleza kero zilizopo kwenye maeneo yao, badala ya kulalamika katika mitandao ya kijamii. **PICHA: GODFREY MUSHI**

# Wazazi 375 kukamatwa kisa wanafunzi kutoripoti shuleni

**Na Mary Mosha,** ROMBO

SERIKALI imetoa amri ya kukamatwa wazazi 375 katika Wilaya ya Rombo, ambao watashindwa kuhakikisha watoto wao waliochaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza, wanaripoti shuleni hadi kufikia Machi 30, mwaka huu.

Mkuu wa Wilaya ya Rombo, Agness Hokororo, aliyasema hayo wakati akitoa taarifa kuhusu hatua zinazochukuliwa na serikali kuhakikisha waliochaguliwa kujiunga na elimu ya sekondari wanatimiza ndoto zao.

"Unajua watu wanacheza na elimu na katika hali kama hiyo ili kuikomesha, nimeagiza wazazi na walezi wote ambao watoto wao hawajaenda shule walizopangiwa mpaka sasa, wakamatwe na kufikishwa mahakamani kama watakuwa hawajaripoti shuleni ifikapo Machi 30, mwaka huu," alisema.

Aidha, Hokororo alisisitiza kuwa operesheni hiyo itakwenda pamoja na kukamata wanaume wakware watakaobainika kuwapa mimba wanafunzi walioshindwa kuripoti shuleni.

Kwa upande wake, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hiyo, Godwin Chacha, alisema kati ya wanafunzi 5,080 waliochaguliwa kujiunga kidato cha kwanza, hadi sasa ambao hawajaripoti ni nusu ya wanafunzi hao.

Idadi hiyo ya waliofaulu katika Wilaya ya Rombo ni sawa na ongezeko la wanafunzi 1,080.

Kwa mujibu wa Chacha, Wilaya ya Rombo mpaka sasa inakabiliwa na upungufu wa madarasa 27.


Awali, Ofisa Elimu Sekondari wa Wilaya hiyo, Petronila Wakurila, alisema serikali imesambaza vitabu vya kutosha vya masomo mbalimbali ikiwamo sayansi katika shule zote ili kuwapunguzia wazazi mzigo wa kuwanunulia vitabu watoto wao.

Mwalimu Mkuu wa Shule ya Sekondari ya Urauri, Justice Kika, aliishukuru serikali kwa kusaidia ujenzi wa madarasa na vitabu vya masomo mbalimbali na wananchi katika ushiriki wao wa hali na mali katika ujenzi huo.

NIPASHE JUMATATU FEBRUARI 17, 2020

Nipashe

# Spotika



SABABU 3 UNITED KUMTAKA GREALISH UK. 20




## ISIKUPITE

KAMA Cristiano Ronaldo atatwaa Kiatu cha Dhahabu Ligi Kuu Italia, Serie A msimu huu, atakuwa mchezaji wa kwanza kutwaa tuzo hiyo katika Ligi Kuu tatu kubwa za nchi tofauti. Tayari ameshatwaa kiatu hicho akiwa Ligi Kuu England na Hispania, hadi sasa ana mabao 20 Serie A, matano pungufu kwa kinara Ciro Immobile wa Lazio.

# BAO LANGU LA 100

Sadio Mane akipiga shuti kuunganisha pasi ya Jordan Henderson na kufunga bao lake la 100 kwenye soka la Uingereza wakati Liverpool ikiifunga Norwich 1-0, Jumamosi.




# TAKWIMU ZA ZIYECH AKITUA CHELSEA

**LONDON, England**

HAKIM Ziyech hatahitaji utambulisho kwa mashabiki wa Chelsea baada ya raia huyo wa Morocco kukamilisha usajili wake wa kuhamia Stamford Bridge akitokea Ajax.

Ziyech alikuwa mmoja wa wachezaji bora uwanjani wakati wakitoka sare ya kufungana 4-4 na Chelsea Novemba mwaka jana kwenye mchezo wa Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Kepa Arrizabalaga anaweza kuonekana alijifunga, lakini shuti la Ziyech lilimshinda na kujikuta Chelsea wakiwa nyuma kwa mabao 3-1 kipindi cha mapumziko.

Msimu ujao mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 26 atakuwa kwenye viunga vya Stamford Bridge, baada ya kukamilisha usajili wa pauni milioni 38 kwa kiungo huyo mshambuliaji.

**Makala hii inamchambua Ziyech kwa Takwimu.**

**Masta wa kutengeneza nafasi**

Ziyech amekuwa na kiwango cha kuvutia zaidi kwenye Ligi Kuu ya Uholanzi, Eredivisie, tangu alipoanza kucheza kikosi cha kwanza pale Heerenveen mwaka 2012 akitokea timu ya vijana.

Baada ya miaka miwili, Ziyech akahamia Ajax Agosti mwaka 2016 ambako kiwango chake kiling'ara kwenye Ligi ya nyumbani na Ligi ya mabingwa Ulaya.

Tangu kutua pale uwanja wa Johan Cruijff, ni wachezaji wanne tu walioweza kufikisha magoli zaidi ya 38 ambayo yeye amefunga na kumfanya kuwa jumla ya mabao 51 ya kwenye Ligi Kuu.

Amehusika katika mabao 89 ya Ligi, saba zaidi ya Berghuis, huku Bryan Linssen akimfuatia kwa kuhusika na mabao 66.

Ziyech ametengeneza nafasi 421 tangu Septemba 2016 akimzidi 134 Berghuis anayeshika nafasi ya pili.

Ajax walikuwa wanacheza soka la kuvutia msimu wa 2018-19 kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya, lakini bao la Lucas Moura wa Tottenham la dakika za majeruhi likawazuia vijana hao wa Erik Hag kutinga fainali.

Ziyech alikuwa na mhamu kubwa zaidi ya kufuzu hatua ya robo fainali, kwani alitoa asisti saba kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Akimzidi mchezaji mwenzake Dusan Tadic na akipitwa moja na Kylian Mbappe na Riyad Mahrez na moja zaidi na nyota wa Barcelona, Lionel Messi.

Mabao yake matano ni 13 machache zaidi ya 18 aliyofunga mshambuliaji wa Bayern Munich, Robert Lewandowski, huku Messi akifunga 14.

Messi anaongoza orodha kwa kuhusika katika mabao 20, Lewandowski (18), Mbappe (17), Raheem Sterling (14), Tadic na Mohamed Salah (wote 13) na Ziyech 12 kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Kwa upande wa nafasi alizotengeneza Ziyech zimefika 39 sawa na Christian Eriksen na amezidiwa na Toni Kroos (51), Tadic (47) na Messi (41).

**Takwimu**

Tangu msimu wa 2012-13, Ziyech amecheza mechi 217 za Ligi Kuu ya Uholanzi, Eredivisie, amefunga mabao 79 na kutoa asisti 87.

Ziyech ana asisti 10 katika mechi sita za Eredivisie msimu huu, hakuna mchezaji mwingine.

Hakuna mchezaji mwenye asisti nyingi (51), mashuti (528), nafasi alizotengeneza (421), chenga (288) kama Ziyech kwenye Ligi Kuu ya Uholanzi tangu ajiunge na Ajax.

**JE, WAJUA?**




LIVERPOOL imecheza bila kuruhusu bao (clean sheet) katika mechi 10 kati ya 11 za Ligi Kuu msimu huu.

## MICHEZO

# YANGA NA REKODI MBAYA YA KUJIFUNGA

**Na Adam Fungamwango**

ACHANA na sare ya bila kufungana dhidi ya Prisons iliyoipata Yanga Jumamosi iliyopita, Jumanne iliyopita pia ilipata sare ya bao 1-1 dhidi ya Mbeya City na lilikuwa bao la kujifunga la Lamine Moro kwenye Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam, limeifanya timu ya Yanga iongoze kwa wachezaji wake kujifunga kwenye mechi za Ligi Kuu msimu huu.

Ni goli lililoinyima Yanga ushindi kwani ingeweza kuondoka na ushindi wa bao 1-0, lakini beki huyo raia wa Ghana alitangulia kujifunga, kabla ya Benald Morrison kusawazisha dakika ya 78 na kuifanya mechi hiyo iishe kwa sare ya bao 1-1.

Hii ni mara ya pili kwa Yanga kujifunga kwani, beki mwingine wa timu hiyo Ally Sonso alijifunga katika harakati za kuokoa kwenye mechi ya Ligi Kuu dhidi ya Azam FC, na bao hilo lilidumu hadi mwisho, Azam FC ikitoka na ushindi wa bao 1-0.

Kwa mujibu wa rekodi zetu ni tayari wachezaji 11 wameshajifunga wenyewe kwa bahati mbaya kwenye mechi za Ligi Kuu, huku Yanga ikiwa na wachezaji wawili ambao ni Sonso na Lamine.

Wachezaji wengine ambao wametumbukiza mpira kwenye kamba za timu wanazochezea ni Ibrahim Said wa Mbao FC, George Chota wa Mbeya City, Yassin Mustapha wa Polisi Tanzania, Dickson Daudi wa Mtibwa Sugar na Mtenje Juma wa Coastal Union.

Wengine ni Geofrey Luseke wa Alliance, Juma Nyosso wa Kagera Sugar na Michael Ismail wa Prisons.

Kwa misimu ya hivi karibuni mabeki wa Yanga wamekuwa na bahati mbaya sana ya kujifunga magoli kwenye mechi mbalimbali za Ligi Kuu na michuano mingine.

Mwandishi wa makala haya anakutelea rekodi ya wachezaji wa timu hiyo kujifunga kwenye misimu ya hivi karibuni.

**Juma Abdul-Yanga vs Azam (Ligi Kuu)**

Rekodi zinaanzia mwaka 2016, ikiwa ni kwenye Ligi Kuu msimu wa 2015/16, Yanga ilipotoka sare ya mabao 2-2 dhidi ya Azam FC.

Katika mechi hiyo beki wa Yanga, Juma Abdul alijifunga katika harakati za kuokoa mpira.

Hata hivyo, mchezaji huyo huyo baadaye alisawazisha makosa yake na kuipatia Yanga bao.

Mabao mengine kwenye mechi hiyo iliyochezwa Machi 5, 2016 yalifunga na John Bocco wakati huo akiwa Azam na Donald Ngoma wakati huo akiwa Yanga.

**Abdallah Shaibu 'Ninja'**

Ilikuwa ni Agosti 12, 2017, mechi ya kirafiki dhidi ya Ruvu Shooting, ikijiandaa na mechi ya Ngao ya Jamii dhidi ya Simba, msimu wa 2017/18, beki wa Yanga, Abdallah Shaibu 'Ninja' akiwa ndiyo kwanza amesajiliwa na klabu hiyo, alijifunga bao dakika ya 22 kwenye mechi hiyo na kusababisha timu yake kufungwa bao 1-0, mechi ikipigwa Uwanja wa Azam Complex, Chamazi jijini Dar es Salaam.



Beki wa Yanga Lamine Moro aliyevaa jezi namba 25 akiwa na wachezaji wenzake kwenye moja ya mechi za Ligi Kuu.

Ni goli lililomweka kwenye wakati mgumu mno na kushindwa kuaminiwa kwenye maisha yake ya mwanzo klabuni hapo, lakini baadaye akageuka kuwa beki wa kutegemewa hadi alipohama.

**Andrew Vicent-Yanga vs Mbao (Kombe la FA)**

Ilikuwa ni 2017 wakati beki wa Yanga, Andrew Vicent 'Dante' alipojifunga kwenye mechi ya nusu fainali ya Kombe la FA kwenye Uwanja wa CCM Kirumba Mjini Mwanza.

Dante aliuweka mwenyewe mpira wavuni akiwa katika harakati za kutaka kuokoa krosi ya Pius Buswita ambaye baada ya msimu huo akasajiliwa na Yanga.

Ni bao hilo pekee ndilo lililopatikana kwenye mechi hiyo, Mbao FC ikiifunga Yanga bao 1-0 na kuipeleka fainali ambayo ilicheza dhidi ya Simba mjini Dodoma na kufungwa mabao 2-1, Simba ikitwaa kombe hilo.

**Abdulaziz Makame-Yanga vs Zesco (Ligi ya Mabingwa)**

Kiungo Abdulaziz Makame alijifunga bao kwenye dakika ya 78 katika harakati za kuokoa krosi kali iliyopigwa na Quadri Aladeokum za Zesco kwenye mechi ya Ligi ya Mabingwa Afrika mwishoni mwa mwezi Oktoba 2019 nchini Zambia na kuifanya timu hiyo kufungwa mabao 3-2 na kuondolewa kwenye michuano hiyo.

"Nilikwenda kuuzuia mpira baada ya kuona nyuma yangu kuna mchezaji wa Zesco. Nikiwa na uhakika kuwa nitautoa nje, kwa bahati mbaya nikajifunga." Alisema kiungo hiyo.

**Ally Sonso-Yanga vs Azam (Ligi Kuu)**

Hii ni Ligi Kuu ya msimu huu, mechi ikichezwa Januari 28 mwaka huu kwenye Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam kati ya Yanga dhidi ya Azam FC.

Beki wa kati, Ally Sonso, alijifunga mwenyewe dakika ya 25 ya mchezo na kuwa bao pekee, timu yake ya Yanga ikilala bao 1-0 dhidi ya Wanalambalamba.

Goli hilo lilitokana na mpira wa kona ambao kipa Farouk Shikalo aliupangia, lakini ulimgonga beki huyo na kurejea tena golini, ukatinga wavuni.

**Lamine Moro-Yanga vs Mbeya City (Ligi Kuu)**


Kama ukiangalia mabeki wote wa Yanga waliojifunga ni Wabongo, lakini huyu sasa ni raia wa Ghana.

Beki huyu wa kati Lamine Moro alijifunga goli Februari 11 kwenye mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara ulichezwa Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam. Yalikuwa ni mawasiliano hafifu kati yake na kipa Metacha Mnata na beki huyo akaupiga ili kuutoa nje, lakini akajikuta akiutumbukiza wavuni dakika ya 40.

Kwenye mechi hiyo, Yanga ilitoka sare ya bao 1-1 dhidi ya Mbeya City.

**NJE YA UWANJA**

Wachezaji wa Manchester City waliitwa katika mkutano na mkuu wa klabu hiyo Ferran Soriano, Jumamosi, saa moja baada ya klabu hiyo kupigwa marufuku ya kushiriki kombe la Ligi ya Mabingwa kwa misimu miwili.



Extra Time




# REKODI ZINAZOSUBIRIWA KUVUNJWA NA LIVERPOOL MSIMU 2019/20 EPL

**LONDON, England**

INAONEKANA ni suala la muda tu kwa Liverpool kutwaa taji la Ligi Kuu ya England msimu huu na wanaweza kuvunja rekodi nyingi tu kwa kutwaa taji hilo.

Kikosi hicho cha kocha, Jurgen Klopp kimekuwa na msimu wenye mafanikio makubwa zaidi huku kikiongoza msimamo kwa tofauti ya pointi 22 (kabla ya mechi za juzi na jana).

Liverpool pia bado wapo kwenye mashindano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya na kombe la FA, na hadi sasa imebakia kuwa timu pekee ambayo haijafungwa kwenye Ligi Kuu ya England msimu huu.

Makala hii inakuchambulia rekodi ambazo zinasubiriwa kuvunjwa na timu hiyo itakapobeba taji la Ligi Kuu ya England.

**Ushindi mfululizo**

Kwa sasa rekodi ya kushinda mechi nyingi mfululizo inashikiliwa na Manchester City wakati iliposhinda mechi 18 mfululizo msimu wa 2017/18. Liverpool wana nafasi ya kuifikia na kuivunja rekodi hiyo wakati watakapolibeba taji hilo.

Mechi nyingi bila kufungwa

Arsenal ina rekodi ya kucheza mechi 49 bila kufungwa kwa msimu wa 2002/03-2004/05.

Na wakati Arsenal ikiweka rekodi hiyo kuliwa na maswali kwamba nani ataweza kuja kuivunja wakati washikabunduki hao walipokuwa chini ya kocha Arsene Wenger.

Liverpool haijaonja machungu ya kufungwa msimu huu na wekundu hao wanaweza kufikisha mechi 50 kama hawatafungwa kwenye mechi zote za ligi zilizobaki.

Mchezo wa 50 utakuwa ni ule wa nyumbani dhidi ya Aston Villa Aprili 11.

Ushindi mechi nyingi

Manchester City wanashikilia rekodi ya kushinda mechi 32 katika msimu wa 2017/18 na 2018/19.

Man City iliweka rekodi wakati klabu hiyo ya Pep Guardiola alipotwaa taji lake la kwanza la Ligi Kuu mwaka 2018.

Kama wataendelea kushinda mechi zao zikiwamo zile dhidi ya City na Everton, watavunja rekodi kwa kushinda mechi 37.

**Pointi nyingi**

Timu ya Manchester City ilifikisha pointi 100 wakati ikitwaa ubingwa wake msimu wa 2017/18.

Bao la dakika za mwisho la Gabriel Jesus liliipa Manchester City ushindi dhidi ya Southampton kwenye mchezo wa mwisho wa ligi msimu wa 2017/18 na kukifanya kikosi hicho kutwaa ubingwa kwa kuwa na pointi 100.

Liverpool wana nafasi ya kufanya hivyo msimu huu kwani wanaweza kuzifikia pointi hizo.

**Ushindi mechi nyingine ugenini**

Manchester City ilishinda mechi 16 ugenini msimu wa 2017/18, lakini Liverpool wana nafasi kubwa ya kuifikia rekodi hiyo. Wanaweza kuweka historia hiyo kwenye mchezo wao dhidi ya Arsenal pale kwenye dimba la Emirates - sehemu ambayo walibeba pointi tatu mara moja tu kwenye mechi zao sita za mwisho kwenda pale.

Ushindi mechi nyingi nyumbani

Chelsea ilishinda mechi 18 nyumbani msimu wa 2005/06, huku Manchester United ikiweka rekodi hiyo msimu wa 2010/11 na Manchester City msimu wa 2011/12 na ule wa 2018/19.

Liverpool inakabiriwa na mechi sita za nyumbani kuweza kuivunja rekodi ya kushinda mechi nyingi ugenini.

Kati ya hizo sita, mechi tano zitakuwa dhidi ya timu ambazo kwa sasa zipo chini ya katikati ya msimamo huku Chelsea pekee ikiwa kwenye nne bora katika mchezo wake wa mwisho pale Anfield.

Liverpool haijapoteza mchezo wowote wa ligi nyumbani tangu Crystal Palace ilipowafunga Aprili 2017, na wameshinda mechi 43 na kutoka sare 10 huku wakikaribia mwaka wa tatu bila kufungwa.

**Siku nyingi bila kufungwa**

Arsenal ilicheza mechi siku 537 bila kufungwa msimu wa 2002/03 na 2004/05, rekodi ambayo haijavunjwa hadi sasa.

Kama Liverpool itamaliza Ligi Kuu bila kufungwa watakuwa na nafasi ya kuizima rekodi hiyo ya Arsenal ambapo ilikuwa ni sawa na kucheza miezi 18 bila kufungwa.

Rekodi hii inaweza kuwa na changamoto kubwa zaidi kwa kikosi cha Klopp hasa kutokana na ukweli kwamba bado wapo kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya na kombe la FA. Itakuwa kazi ya ziada kwa kikosi hicho kuweza kuongeza siku 46 zaidi kwenye rekodi ya Arsenal.

**Tofauti ya pointi nyingi**

Manchester City walishinda taji la Ligi Kuu kwa tofauti ya pointi 19 msimu wa 2017/18.

Liverpool kwasasa wanaongoza msimamo kwa tofauti ya pointi 22 na pengine wanaweza kuvunja rekodi hiyo.


Liverpool wanaweza kubeba taji la Ligi Kuu ya England wakati watakaposafiri kwenda kucheza na Manchester City pale kwenye dimba la Etihad mwanzoni mwa Aprili.

## Nukuu

"Liverpool inapaa, na hainishangazi, tayari tulishaliona hilo mwaka jana wakati walipotwaa Ligi ya Mabingwa, lakini sishangazwi kwa sababu ya kikosi chao kizuri na kocha. Ni mwenye furaha sana, kwa sababu nina marafiki wengi sana pale, wachezaji wenzangu wa zamani, hivyo ni mwenye furaha sana kwao. Lakini hivyo ndivyo ilivyo, siwezi kutazama nyuma, ninatazama njia nyingine," **Kiungo wa zamani wa timu hiyo, kwa sasa Bayern Munichi, Philippe Coutinho.**



"Leo [Messi] alisema Barca ni kila kitu kwake yeye, kwamba anataka kuendelea kuwa hapa, lakini kuna masharti. Tunazungumza kuhusu mchezaji bora duniani na kuongeza mkataba kwa mchezaji kama huyo haijawahi kuwa rahisi," **Mkurugenzi wa Ufundi wa klabu hiyo, Eric Abidal.**



"Kiukweli kabisa, ningependa kufanya kazi kwenye Ligi Kuu England, itakuwa ngumu, najua na kwa sasa ni wakati wa kusubiri na kuona nini kitatokea. Ni wakati wa kujirekebisha, kufikiria kuhusu wewe mwenyewe kidogo, na kuwa tayari kwa sababu kwenye soka kitu chochote kinaweza kutokea na unatakiwa kuwa tayari. Niko tayari na nasubiria changamoto mpya. Nina imani na najiamini kwamba changamoto ijayo itakuwa nzuri zaidi," **kocha wa zamani wa Tottenham, Mauricio Pochettino.**



# DILUNGA WA SIMBA SASA YUKO JUU MAWINGUNI

**Na Adam Fungamwango**

BAADA ya kumalizika mechi yao dhidi ya Mtibwa Sugar kwenye Uwanja wa Jamhuri mjini Morogoro, mshabiki wa Simba walimbeba juu juu, kiungo mshambuliaji wa timu hiyo, Hassan Dilunga na kuzunguka naye uwanjani, baadhi wakipiga naye picha kutokana na kiwango kikubwa alichoonyesha kwenye mechi hiyo.

Mbali na kusakata kandanda safi na la kuvutia, alifunga bao la tatu lililoipa Simba ushindi wa mabao 3-0 Jumanne iliyopita.

"Mtibwa wanisamehe kwa hili, maana nimeshangilia sana hili bao. Unajua wakati mwingine unaweza kufanya kitu ukajishangaa hata wewe mwenyewe. Mtibwa ni timu yangu na ndiko nilikotokea, mazingira yenyewe ya mechi ndiyo yaliyonifanya nishangilie sana. Wanisamehe sana." Alisema mara baada ya mechi hiyo.

Tangu kuanza kwa mzunguko wa pili, Dilunga amekuwa kwenye kiwango cha hali ya juu na kuiwezesha klabu yake ya Simba kushinda mechi kadhaa za Ligi Kuu Tanzania Bara inayoendelea.

Kwa sasa amefikisha mabao sita kwenye Ligi Kuu, akiwa amemkuta kiungo mshambuliaji mwenzake wa Simba aliye kwenye majeruhi ya muda mrefu kwa sasa, Miraji Athumani.

Mbali na mchezaji huyo, wachezaji wengine wenye magoli sita ni Adam Adam wa JKT Tanzania, Ayoub Lyanga wa Coastal Union, na Waziri Junior wa Mbao FC.

Mechi ya kwanza 'iliyomtoa' Dilunga ilikuwa ni sikukuu ya Krismasi alipofunga mabao mawili, Simba ilipocheza mechi ya Ligi Kuu dhidi ya Lipuli ya Iringa jijini Dar es Salaam kwenye mechi ya mzunguko wa kwanza, Desemba 25 mwaka jana.

Alifunga goli lake la kwanza kwa mkwaju wa penalti dakika ya 56, na baadaye dakika ya 64, Simba ikishinda mabao 4-0, mengine yakifungwa na Meddie Kagere na Francis Kahata.

Goli lake la tatu alilifunga Januari 16 mwaka huu, Simba ilipoichapa Mbao FC mabao 2-1 kwenye Uwanja wa CCM Kirumba mjini Mwanza.

Lilikuwa ni bao la kwanza kwenye mechi hiyo, akilifunga dakika ya 41, kabla ya Jonas Mkude kupachika la pili dakika ya 46.

Siku tatu baadaye, Simba ilicheza mechi ya Ligi Kuu kwenye uwanja huo huo dhidi ya Alliance FC na kushinda mabao 4-1.

Dilunga kwa mara nyingine tena alifunga bao moja, akiandikisha bao lake la tatu kwenye Ligi Kuu, mengine yakifungwa na Mkude, Kagere na Cleotus Chama, Januari 19 mwaka huu na kuwa bao lake la nne.

Januari 22 mwaka huu, aliandikisha bao la tano kwenye Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam, Simba ikiichapa Namungo FC mabao 3-2.

Mbali na Kahata na Kagere kufunga mabao, Dilunga alifunga bao la pili kwenye mechi hiyo dakika ya 38.

Jumanne iliyopita kwenye Uwanja wa Jamhuri mjini Morogoro, alipachika bao lake la sita msimu huu, likiwa ni la tatu kwenye mechi hiyo, Simba ikishinda mabao 3-0.

Mchezaji huyo aliyezaliwa Oktoba 10, 1993, kwa nyakati tofauti amezichezea klabu za Ruvu Shooting, Yanga, JKT Ruvu, Mtibwa Sugar, kabla ya kujiunga na Simba, na huu ni msimu wa pili kwake.

Ikumbukwe kuwa msimu wa kwanza kujiunga na Simba, aliifungia timu hiyo bao la pili na la ushindi kwenye Uwanja wa CCM Kirumba kwenye mechi ya Ngao ya Jamii dhidi ya timu yake ya zamani, Mtibwa Sugar, Simba ikitwaa ngao, kabla ya kuanza kwa msimu wa Ligi Kuu Tanzania Bara 2018/19.


Alimaliza ligi msimu uliopita akiwa ameifungua Simba mabao mawili tu.



Hassan Dilunga (kushoto), akiwa na mmoja wa wachezaji wa Lipuli baada ya mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara msimu uliopita.

## NAJUA WAJUA

HADI sasa Jordan Henderson ametoa pasi za mwisho tano kwenye Ligi Kuu England, ni katika msimu wa 2014/15 (9) na 2013/14 (7) alitoa pasi zaidi kwa msimu mmoja.



# KWA NINI ARSENAL ITAMALIZA 4-BORA




**LONDON, England**

WAKATI Arsène Wenger mara moja aliposema kumaliza kwenye nne bora sawa na kutwaa taji, kauli yake hiyo ilionekana kama vile isiyoeleweka kwa wengi.

Lakini sasa kauli ya Mfaransa huyo inaonekana kuwa kweli kwani timu nyingi sasa zinaona thamani ya kuipata nafasi hiyo ni kama vile kubeba kombe la FA na lile la Carabao.

Mapato ambayo yanapatikana kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya kunazifanya timu kuwa na 'njaa' kubwa ya kutaka kumaliza kwenye nne bora.

Arsenal haijacheza Ligi ya Mabingwa Ulaya kwa misimu mitatu, maana yake kwamba wamekosa kuingiza fedha nyingi kwa miaka mitatu. Ligi ya Mabingwa Ulaya siyo tu inaingiza fedha nyingi, bali pia inavutia usajili wa wachezaji wapya.

Kwa msimamo ulivyo sasa, Arsenal wamepitwa pointi 10 kutoka kwenye nne bora. Lakini tayari wameonyesha kuimarika na kwa sasa kuna uwezekano mkubwa wa kujikuta wakimaliza kwenye nne bora.

Hapa tunaangalia sababu 3 kwanini Arsenal itaweza kumaliza kwenye 4 bora msimu huu.

**3. Kiwango cha wapinzani**

Msimu huu, kuna timu nyingi zinazopigania kufuzu Ligi ya Mabingwa Ulaya, ikiwamo Leicester City, Chelsea, Manchester United, Tottenham Hotspur na Arsenal. Tuchukulie kwamba nafasi mbili za juu zinachukuliwa na Liverpool na Manchester City, na klabu tano zilizotajwa hapo juu inamaana zinapigania nafasi mbili zilizobaki.

Msimu huu Chelsea imepoteza mechi 8, Leicester 6, Manchester United 8, Tottenham 8 na Arsenal 6. Hakuna timu iliyoonyesha uimara wa kushinda mechi mfululizo na hiyo maana yake ni kwamba Arsenal ina nafasi nzuri zaidi ya kumaliza kwenye nne bora nyuma ya Manchester City na Liverpool.

Kama Arsenal itaweza kuwa na matokeo mazuri mfululizo kwa kushinda angalau nusu ya mechi zake zilizobaki, nafasi ya kumaliza kwenye nne bora ni kubwa zaidi kwao. Arsenal itakutana na timu hizo zinazowania nne bora mara nne katika kipindi chote cha msimu kilichobakia na kuwaacha wao wakiwa na mechi nyingi za kuweza kushinda.

**2. Kuimarika safu ya ulinzi**

Kwa miaka mingi, mashabiki wa Arsenal wamekuwa wakilia kuhusu ubovu wa safu yao ya ulinzi. Ukiacha Laurent Koscielny, hakuna beki mwenye ubora aliyesajiliwa kwa miaka ya hivi karibuni.

Kipindi cha majira ya joto, klabu hiyo iliamua kumsajili David Luiz ili kumaliza tatizo lao la ulinzi, lakini alionekana siyo suluhisho la kumaliza matatizo ya ulinzi ya Arsenal. Na matokeo yake klabu ikaamua kutumia busara kwa kuimarisha safu ya ulinzi wakati wa dirisha dogo la Januari kwa kusajili wachezaji wawili.

Ujio wa Pablo Mari na Cedric Soares umeipa Arsenal nafasi ya kuimarisha safu yao hiyo chini ya kocha, Mikel Arteta.

Kwa mechi chache ambazo Arteta ameiongoza klabu hiyo, safu ya ulinzi ya Arsenal imeanza kuimarika na kwa sasa alichobakiwa ni kuimarisha safu ya ushambuliaji.

**1. Falsafa ya Arteta**

Tangu Mikel Arteta alipoichukua Arsenal, kumekuwa na mtazamo tofauti kwa timu.

Ghafla washikabunduki hao wanaonekana kuimarika kwa safu ya ulinzi na kuwa timu iliyounganika zaidi kutoka mbele hadi nyuma. Arteta amesisita kwamba timu inalinda kwa umoja. Raia huyo wa Hispania amekuwa kwenye timu hiyo kwa wiki saba pekee, lakini timu hiyo imeonesha ishara nzuri zaidi kwa kipindi kifupi kuliko muda wa miezi 18 waliokuwa chini ya Unai Emery.

Kocha huyo alibainisha kwenye mkutano wake wa kwanza na waandishi wa habari akisema anatarajia kiwango cha wachezaji kuwa cha asilimia 100 na yule ambaye hataendana na falsafa hiyo hataichezea timu kwa siku za usoni.

Wachezaji wanaelewa kwamba wanatakiwa kucheza kwa kujituma kwa dakika zote 90 wakiwa dimbani ili kupata nafasi ya kucheza mara kwa mara.

NDANI YA 18



BAO alilofunga Sadio Mane wakati wakishinda 1-0 dhidi ya Norwich juzi linamfanya kufikisha jumla ya mabao 100 kwenye Ligi Kuu England, 75 akiifungia Liverpool na 25 alifunga akiwa na Southampton.



INAONEKANA ni suala la muda tu kwa Liverpool kutwaa taji la Ligi Kuu ya England msimu huu na wanaweza kuvunja rekodi nyingi tu kwa kutwaa taji hilo. Kikosi hicho cha kocha, Jurgen Klopp kimekuwa na msimu wenye...
**Uk. 16-17**



# SABABU 3 UNITED KUMTAKA GREALISH

**MANCHESTER, England**

LICHA ya kumsajili Bruno Fernandes wakati wa dirisha dogo la usajili la Januari, Manchester United bado inahitaji usajili wa wachezaji wengine kabla ya kutoa ushindani Ulaya. Lakini ujio wa raia huyo wa Ureno umeonyesha ishara nzuri ya kuimarisha safu yao ya ulinzi.

Safu ya ulinzi ya Manchester United imekuwa haina ubora msimu huu kutokana na kukabiliwa ma majeruhi wengi. Kuumia kwa Scott McTominay na Paul Pogba kumeifanya timu hiyo kuwa kwenye wakati mgumu.

Mashetani wekundu hao walitakiwa kuimarisha safu yao ya ulinzi tangu kipindi cha majira ya joto kilichopita wakati Ander Herrera aliporuhusiwa kuondoka bila kupata mrithi wake.

Kipindi cha majira ya joto kinachokuja cha mwaka huu United itatakiwa kuimarisha safu yao ya ushambuliaji na sasa ni wazi kwamba anayehitaji zaidi pale kwa sasa si mwingine zaidi ya Jack Grealish.

Kiungo huyu wa Aston Villa amekuwa na kiwango cha kuvutia katika klabu yake hiyo ya utotoni kwa miaka kadhaa na aliwasaidia kupanda Ligi Kuu msimu huu. Tangu kupanda daraja kwa timu hiyo, Grealish kiwango chake kimezidi kuimarika. Makala hii inachambua sababu 3 kwanini United wanatakiwa kumsajili Muingereza huyo kipindi kinachokuja cha majira ya joto.

**3. Urahisi wa kumpata**

Manchester United awali walikuwa wanataka kumsajili James Maddison, mchezaji ambaye mashetani wekundu hao wamemfuatilia kwa kipindi kirefu. Hata hivyo, Muingereza huyo anakaribia kukubali kusaini mkataba mpya na Leicester City na hilo litafanya uwezekano wa kumpata ni mdogo.

Na inaonekana wazi kwamba, United watashindwa kumsajili Maddison, sasa ni muda mwingine kwa United kuangalia sehemu nyingine.

Na hapo ndio Grealish anapokuja. Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 24 ameichezea Aston Villa kwa kipindi chote cha maisha yake na sasa yupo tayari kuondoka kwenye klabu yake hiyo ya utotoni. Ameripotiwa kwamba anawaniwa na Barcelona, huku pia Pep Guardiola amethibitisha kuwa anavutiwa zaidi na mchezaji huyo.

Ushindani unaweza kuwa mkubwa, lakini United lazima ifanye kila kinachowezekana kupata saini ya Grealish.

Muingereza huyo atafikisha umri wa miaka 25 Septemba na huku akiwa amepita umri wa miaka 23 waliouweka United kwenye soko la usajili, Grealish ana ubora utakaomwezesha kuisaidia United.

**2. Kiraka**

Solskjaer ameonesha kupenda zaidi kutumia mfumo wa 4-2-3-1 msimu huu, lakini anaweza kurudisha mfumo wa 4-3-3 kwenye timu hiyo. kwa kuongezea wachezaji waliopo wanaweza kucheza mifumo yote miwili. Sasa kwenye hali hiyo uwepo wa Grealish utaipa faida kubwa zaidi mashetaji wekundu hao.

Muingereza kama James Maddison ni namba 10 ambaye anaweza kucheza pia namba 8. Grealish anacheza namba 8 katika timu ya Aston Villa, sehemu ambapo viungo wanacheza watatu, lakini anaweza kucheza namba 10 kwenye kikosi cha Solskjaer katika mfumo wa 4-2-3-1. Kwa nyongeza, Muingereza huyo anaweza kucheza kama fowadi wa kushoto mbele ya watatu na amefanya hivyo akiwa Villa.


Ukilinganisha na Maddison, Grealish anatengeneza nafasi nyingi zaidi kwa mchezo. Grealish ana mabao 9 na asisti 5 katika mechi 26 hadi sasa msimu huu.

**1. Kiongozi**

Kama United wataweza kumsajili Grealish pale Old Trafford, watakuwa na mchezaji mzuri zaidi ambaye ni kiongozi wa timu. Mashetani wekundu hao wamekuwa hawana kiongozi uwanjani na kwenye vyumba vya kubadilishia nguo na hivyo kuwaumiza mchezoni.

Grealish, ambaye anavaa kitambaa cha unahodha kwa klabu yake hiyo ya utotoni, ni kiongozi kwa asili na kwa mfano. Ujio wake kwa mfano utakifanya kikosi hicho cha Solskjaer kuwa na mtu ambaye ataweza kuwaunganisha wachezaji uwanjani.

**USILOLIJUA**



LIONEL Messi hajafunga katika mechi nne mfululizo kwenye La Liga hiyo ikiwa ni mara ya kwanza kwake kukumbwa na ukame kama huo, tangu kipindi cha Oktoba 2013 hadi Januari 2014.





Ofisa Mkuu wa Wateja Binafsi, Biashara Ndogo na za Kati wa NMB Filbert Mponzi, akimpa maelezo kuhusu benki hiyo, Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu Uwekezaji, Angela Kairuki, alipotembelea katika banda la NMB kwenye kongamano la uwekezaji mkoani Songwe katika Viwanja vya Vwawa. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mbaroni tuhuma za kukutwa na dhahabu bandia

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

JESHI la Polisi mkoani Mbeya, linawashikilia watu wawili akiwamo mwalimu wa Shule ya Msingi Kangamo wilayani Momba, Mkoa wa Songwe, Jacob Mwangosi, kwa tuhuma za kukutwa na dhahabu bandia yenye uzito wa gramu 600.

Akizungumza na waandishi wa habari ofisini kwake juzi, Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Mbeya, Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa Polisi, Ulrich Matei, alisema mwalimu huyo pamoja na mwenzake, Joseph Singogo ambaye ni Mkazi wa Kangamo walikamatwa Februari 11, mwaka huu saa 10:30 jioni katika Soko Kuu la Dhahabu, wilayani Chunya.

Alisema watuhumiwa walinaswa wakati wakitaka kuuza dhahabu hiyo bandia katika soko hilo na kwamba endapo watuhumiwa wangefanikiwa kuuza kipande hicho cha dhahabu feki, wangepata zaidi ya Sh. milioni 70.

Alisema watuhumiwa walikuwa tayari wameshampata mteja wa kununua dhahabu hiyo ambaye anajulikana kwa jina la Paulo Gagala, mmoja wa wanunuzi wa dhahabu katika soko hilo.

"Wataalamu wa madini katika Soko Kuu la Dhahabu la Chunya, walibaini kuwa dhahabu ile ilikuwa bandia na hivyo watuhumiwa wakakamatwa na mpaka sasa wanashikiliwa katika Kituo cha Polisi Chunya wakati tukiendelea na taratibu za kuwafikisha mahakamani," alisema Kamanda Matei. Kamanda Matei aliwataka wanunuzi wa dhahabu katika Mkoa wa Mbeya, kuepuka kununua dhahabu nje ya masoko yaliyoanzishwa na serikali kwa maelezo kuwa ndio mazingira ambayo matapeli wanayatumia.

Vilevile aliwaomba wataalamu wa madini nchini kutoa elimu kwa wananchi ili wawe na ujuzi wa kutofautisha dhahabu sahihi na bandia ili wasiingie kirahisi kwenye mikono ya matapeli.

Katika hatua nyingine Kamanda Matei alisema, wakazi wa Sae jijini Mbeya, walimuua kwa kipigo, Victor Mwasoro (17), ambaye alivamia moja ya vibanda vya M-Pesa katika eneo hilo akiwa na bastola kwa ajili ya kupora fedha.

Alisema mtoto huyo alivamia kibanda cha Sauda Danda akiwa na bastola yenye namba za usajili 00098503 ikiwa na risasi saba na baada ya wananchi kumshtukia walimvamia na kuanza kumshushia kipigo wakitumia silaha za jadi. "Uchunguzi wa awali unaonyesha kuwa mtoto huyo aliichukua silaha hiyo nyumbani kwao na inamilikiwa na baba yake, wakati anaingia kwenye kibanda hicho kujaribu kuitumia kupora alikuwa ameihifadhi kwenye kifungashio," alisema Kamanda Matei na kuongeza.

"Baada ya kuokolewa mikononi mwa wananchi waliokuwa wanampiga alikimbizwa katika Hospitali ya Kanda ya Rufani ya Mbeya na alifariki akiwa anaendelea kupatiwa matibabu," aliongeza. Kufuatia tukio hilo, Kamanda Matei aliwataka wamiliki wa silaha mkoani humo kufuata sheria za umiliki wa silaha ili zisiingie kwenye mikono ya wahalifu.

# Mahakamani wakidaiwa kupokea 120,000/-

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru) Mkoa wa Mbeya, imewafikisha mahakamani watumishi wawili wa Mahakama ya Mwanzo Iyunga jijini Mbeya, kwa tuhuma za kuomba na kupokea rushwa ya Sh. 120,000.

Watumishi waliofikishwa mahakamani ni Hakimu wa Mahakama ya Mwanzo Iyunga, Evangeline Ager, na Mzee wa Baraza, Elizabeth Kibona, ambao wanadaiwa kuomba na kupokea rushwa hiyo kutoka kwa Eva Mahuve, ili wawaachie ndugu zake wawili ambao walikuwa wamewekwa mahabusu katika Gereza la Ruanda.

Watuhumiwa hao walipandishwa kizimbani katika Mahakama ya Hakimu Mkazi wa Mkoa wa Mbeya, Andrew Sauti mwishoni mwa wiki na kusomewa mashtaka yao na Mwendesha Mashtaka wa Takukuru, Maria Mwakatobe.

Akiwasomea mashtaka hayo, Mwendesha Mashtaka wa Takukuru, Mwakatobe, alisema watuhumiwa walitenda kosa hilo Januari 24 na walimshawishi Mahuve awapatie fedha hizo ili wamsaidie kuwatoa ndugu zake.

"Kosa hilo ni kinyume na kifungu cha 15 cha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Namba 11 ya mwaka 2007, hivyo tunaomba sheria ichukuwe mkondo wake dhidi ya hawa watu," alisema Mwakatobe.

Mwakatobe alisema upande wa mashtaka upelelezi wa kesi hiyo umeshakamilika na kuiomba mahakama iendelee kusikiliza ili haki ipatikane mapema.

Watuhumiwa wote wawili walikana kufanya makosa hayo huku wakili anayewatetea, Ladislaus Rwekaza, aliiomba mahakama hiyo kuuamuru upande wa mashtaka kuwaleta mashahidi mahakamani hapo ili waanze kutoa ushahidi wao. "Kwa kuwa upande wa mashtaka wanasema tayari wamemaliza uchunguzi wa shauri hili, ni vema wawalete mashahidi wao ili kesi hii iishe haraka," aliomba Rwekaza.

Watuhumiwa wote waliachiwa kwa dhamana baada ya kukidhi vigezo kwa kila mmoja kutakiwa kujidhamini kwa Sh. 3,000,000 ya maneno na kila mmoja akitakiwa kuwa na mdhamini mmoja.

Awali, akizungumza na waandishi wa habari ofisini kwake, Mkuu wa Takukuru Mkoa wa Mbeya, Julieth Matechi, alisema mbali na watuhumiwa hao pia ofisi yake ilikuwa inakusudia kuwafikisha mahakamani watuhumiwa wengine wawili. Alisema watuhumiwa hao ni Andrew Ndingo na Nesia Mwelangu, ambao alisema walikamatwa wakifanya biashara ya kubadilisha fedha za kigeni jijini Mbeya bila kuwa na vibali vya kufanya biashara hiyo.

Pia alisema watuhumiwa hao walikamatwa kati ya Februari 7 na 8 mwaka huu, wakifanya biashara hiyo kinyume cha kanuni ya 4 (I), 2 ya kanuni za ubadilishaji wa fedha za kigeni (Foreign exchange Act) ya Sheria namba 271 ya mwaka 2002. Kadhalika wanatuhumiwa kwa kosa la kukwepa kodi kwa madai kuwa kwa kufanya biashara hiyo bila kuwa na leseni, serikali ilikuwa haikusanyi mapato.

Alisema kibali cha kuwafikisha mahakamani watuhumiwa hao, tayari kimeshatolewa na Ofisi ya Mwendesha Mashtaka Mkuu wa Serikali (DPP).

Aliwataka wananchi kuendelea kutoa ushirikiano kwa taasisi hiyo kwa kuwafichua watu wanaoomba na kupokea rushwa kwa kupiga simu ya bure namba 113.

# Wahimizwa ujenzi sekondari kukomboa watoto

**Na Nebart Msokwa,** CHUNYA

WANANCHI wa Kata ya Sangambi wilayani Chunya katika Mkoa wa Mbeya, wametakiwa kuendelea kujitoa kuchangia ujenzi wa shule ya sekondari unaoendelea katika kata hiyo, ili kuwapunguzia wanafunzi adha ya kutembea umbali mrefu kwenda kusoma katika Shule ya Sekondari Chalangwa.

Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo, Bosco Mwanginde, alisema hayo wakati alipoiongoza Kamati ya Fedha, Utawala na Mipango ya Madiwani wa Halmashauri hiyo kukagua mradi wa ujenzi wa shule hiyo.

Mwanginde alisema wananchi wakiendelea kujitoa kuchangiaji nguvu na fedha mradi huo utakamilika kwa wakati na wanafunzi wanaosoma Sekondari ya Chalangwa watakuwa wamepunguziwa adha ya kutembea umbali wa zaidi ya kilomita 40.

Alisema licha ya wananchi hao kuonyesha nia ya kujitoa kuhakikisha wanatatua tatizo hilo wanatakiwa waendelee kumalizia majengo yaliyobakia ili waishawishi serikali kutoa kibali cha kusajili.

"Ili shule hii ifunguliwe ni lazima majengo yakamilike, hivyo watendaji hakikisheni mnawafuatilia wananchi wachangie michango yao tukamilishe na tuombe kibali cha kufunguliwa," alisema Mwanginde.

Akisoma taarifa ya utekelezaji wa mradi huo, Ofisa Mtendaji wa Kata ya Sangambi, Ndutu Chapa, alisema mradi huo utagharimu Sh. milioni 900 mpaka kukamilika.

Alisema walipokea michango kutoka Halmashauri na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Mbeya yenye thamani ya Sh. milioni 17, michango ya wananchi Sh. milioni 71 na michango ya wadau mbalimbali ambao walichangia vifaa kwa ajili ya kubeba mawe, mchanga na maji.

"Wananchi wameonyesha moyo wa ajabu wa kujitolea, wamejitoa kwa nguvu sana na matarajio yetu ni kukamilisha majengo haya kabla ya mwezi Aprili," alisema Chapa.

Mratibu Elimu Kata ya Sangambi, Crementino Hongoli, alisema kama shule hiyo itafunguliwa, itasaidia kupunguza matatizo ya wanafunzi kupata mimba.

Alisema shule hiyo ikikamilika itakuwa imepunguza idadi ya wanafunzi 170 ambao kwa sasa wanasoma katika Shule ya Sekondari ya Chalangwa, ambayo ipo kata nyingine.



# NDC kusambaza dawa ya viuadudu

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

SHIRIKA la Taifa la Maendeleo (NDC), limeanza mchakato wa kutafuta mawakala nchi nzima kwa ajili ya kuanza kusambaza dawa ya viuadudu kwa wananchi ili kutokomeza mazalia ya mbu wa malaria kwenye nyumba zao.

Kadhalika Watanzania wameshauriwa kutumia dawa hiyo inayozalishwa ndani ya nchi kwa kuwa haina madhara na kuacha kutumia dawa zenye kemikali kutoka nje ya nchi.

Wito huo ulitolewa jijini hapa na Mkurugenzi Mwendeshaji wa Shirika la Taifa la Maendeleo (NDC), Prof. Damian Gabagambi, alipokuwa akizungumza na gazeti hili.

Alisema viuadudu vinavyozalishwa nchini vimethibitishwa na mamlaka husika. Alilitaka Baraza la Mazingira nchini (NEMC), kuitangaza dawa hiyo kwa wadau wake kama katika migodi, hoteli, baa kwa kuwa tatizo la mbu wanaoeneza ugonjwa wa malaria limekuwa sugu.

"Niwatake NEMC watumie dawa yetu ya viuadudu kuitangaza kwa watu wa migodini, kule kuna mbu wengi sana kwa kuwa wanapochimba mashimo maji yanatuama humo, hivyo mazalia ya mbu yanakuwa mengi, lakini hata katika hoteli na baa pia wanatakiwa kupulizia hiyo dawa," alisema.

Mkurugenzi huyo alisema kuwa, dawa nyingi kutoka nje za kuua mbu zinamchanganyiko wa kemikali mbalimbali na kuhatarisha afya za watu. Prof. Gabagambi alisema wananchi wanatakiwa kupambana na mazalia ya mbu, siyo kuua mbu anayeruka, kwa kuwa kuua mbu baada ya siku tatu mbu mmoja anatoa mayai 200 hivyo kusababisha ugumu wa kuwaangamiza.

"Kuna haja ya serikali na taasisi zake kutumia dawa hii katika kuua mazalia ya mbu, ili kutokomeza kabisa mbu wanaoeneza ugonjwa wa malaria ambao bado tishio hapa nchini," alisema.

Akizungumzia kuhusu kiwanda cha kutengeneza dawa hizo kilichopo Kibaha mkoa wa Pwani, alisema wazo la kujenga kiwanda hicho lilikuwa ni agizo la Mawaziri wa Viwanda nchi za Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) waliokaa mwaka 2007 na kukubaliana ifikapo mwaka 2030 malaria iwe imetokomezwa kwenye nchi zao. Alifafanua kuwa Rais Jakaya Kikwete alipokuwa madarakani mwaka 2009, alianzisha Umoja wa Maraisi wa Afrika kwa ajili ya kutokomeza malaria na alifanikiwa kwenda nchini Cuba na kujionea jinsi walivyotokomeza ugonjwa huo. "Nakuambia Cuba hakuna malaria, wenzetu walifanikiwa kutokomeza malaria kwa kutumia dawa hii, tunayozalisha sisi hapa nchini, kwanini Tanzania tushindwe kumaliza ugonjwa huu?" Alihoji.

Alieleza kuwa kiwanda kina uwezo wa kuzalisha dawa lita milioni sita kwa mwaka.

"Kwa mfano hiyo dawa ya milimita 30, unaweka kwenye maji ya ujazo wa lita 1,500 za maji na inauzwa kwa Sh. 1,000 tu, hivyo unaweza kupulizia maeneo yanayozunguka nyumba yako na kuua mazalia ya mbu," alisema.

Pia alisema kuwa hivi sasa wako katika mchakato wa kutafuta cheti cha uthibitisho wa ubora kutoka Shirika la Afya Duniani (WHO), ili dawa hiyo iwe katika ubora wa kimataifa.



Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu Kazi, Ajira na Vijana, Anthony Mavunde (kushoto), akikata utepe kuashiria uzinduzi rasmi wa duka kubwa la viatu la kampuni ya GSM jijini Dodoma mwisho wa wiki, katikati ni Meneja Msaidizi wa kampuni hiyo, Ahmed Eriba na kulia ni Inam Soudagar mmoja wa wafanyakazi wa kampuni hiyo. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# 'Usafi wahimizwa machinjio ya kuku'

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

WAFANYABIASHARA wa kuuza na kuchinja kuku kwenye masoko ya Jiji la Dodoma wametakiwa kujiepusha na magonjwa ya mlipuko kwa kuzingatia kanuni na sheria za usafi ili kulinda afya za walaji.

Kauli hiyo ilitolewa jana na Ofisa Masoko wa jiji hilo, James Yuna, alipokuwa akikagua eneo la kuchinja kuku katika Soko Kuu la Majengo.

Alisema kuwa jukumu la usafi wa mazingira ni la kila siku kutokana na biashara wanayoifanya na kuwataka kuzingatia usafi ili kuwa na usalama wa chakula.

Yuna alisema kuwa katika kipindi hiki cha mvua ni muhimu wafanyabiashara hao kuzingatia zaidi usafi katika maeneo hayo ya biashara ya kuuza na kuchinja. Aliwataka kuheshimu miundombinu ya mifereji ya maji kwa kuisafisha ili kupitisha maji badala ya kuacha uchafu unaotoa harufu mbaya kwenye eneo hilo. Alisema miundombinu ya jiji ipo katika mpangilio mzuri wa kupitisha maji hivyo hakuna sababu ya kufanya biashara kwenye mazingira yenye uchafu.

Aliwasisitiza kuheshimu sheria na kanuni zilizopo ikiwamo kutovamia maeneo yasiyo rasmi na kufanyia biashara. Alisema ndani ya kata 41 zilizopo Jiji la Dodoma kuna masoko yanayojitosheleza kutokana na mpango uliopo wa ujenzi wake, hivyo ni wajibu wao kufuata kanuni na sheria.

# Ataja sababu kukwama kesi ukatili wa kijinsia

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MKUU wa Wilaya ya Dodoma, Patrobas Katambi, ametaja sababu zinazosababisha kuwapo na ugumu wa kushughulikia kesi za ukatili wa kijinsia na mimba za utotoni kuwa ni pamoja na kukithiri kwa vitendo vya rushwa na kukosa ushirikiano kati ya wazazi, viongozi na vyombo vya dola nchini.

Katambi alitoa kauli hiyo jijini hapa katika mkutano wa kutoa elimu dhidi ya vitendo vya ukatili kwa watoto kwa wananchi wa Kata ya Chang'ombe ulioratibiwa na Shirika lisilo la kiserikali linaloshughulika na masuala ya wanawake na watoto (WOWAP).

Alisema kesi zinafutwa kutokana na wazazi kuharibu ushahidi na baadhi ya askari kuchukua rushwa.

"Kesi zinafutwa kwa sababu watu hawajitokezi kutoa ushahidi kuna watu wanafanya kama ni fursa ya wao kujipatika kipato ili tutakufunga miaka 30 kama una hela toa, tupe milioni tano au mbili ndio kinachofanyika," alisema.

Mkuu huyo alisema kutokana na hali hiyo atahakikisha anapambana bila kujali cheo cha mtu.

"Sitajali kama ni askari au ni nani, aidha mimi niondoke au wewe uondoke, lazima tuchukue hatua ya kukomesha vitendo hivi," alisema.

Naye Mkurugenzi wa Shirika hilo, Fatuma Toufiq, alitoa rai kwa wazazi kuhakikisha watoto wajua haki zao ili anapofanyiwa ukatili ili kutoa taarifa kwenye mamlaka husika.



# HABARI ZANZIBAR

# Wataalamu kuangalia athari mazingira

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Mussa Azzan Zungu, ameahidi kuteua wataalamu maalum wa masuala ya mazingira watakaopewa jukumu la kuangalia athari za mazingira zinazoendelea kujitokeza katika maeneo ya visiwa vya Unguja na Pemba.

Alisema hatua hiyo ambayo ni jukumu la ofisi yake itatekelezwa kufuatia maeneo mengi hasa sehemu zilizo pembezoni mwa Barahi ya Hindi kukumbwa na changamoto za mazingira ikiwamo mmong'onyoko wa ardhi.

Zungu aliyasema hayo wakati akizungumza na Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Balozi Seif Ali Iddi, Mjini Zanzibar.

Alisema visiwa vikubwa na vidogo ni sehemu muhimu zinazopaswa wakati wote kushughulikiwa na kuangaliwa kwa umakini kulingana na maumbile yake ya kuzungukwa na maji sehemu zote ili kulinda mazingira yake kutokana na mabadiliko ya tabianchi yanayoikumba dunia hivi sasa.

Waziri huyo alisema atapanga ziara maalum ya kuangalia hali ya mazingira katika maeneo ya Zanzibar kwa kushirikiana na Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar inayoratibu na kusimamia mambo yote ya Muungano na Mazingira kwa upande wa Zanzibar.

Zungu aliipongeza Serikali ya Zanzibar kwa usimamizi wao makini wa kuwaletea maendeleo wananchi wa visiwa vya Unguja na Pemba.

Alisema Zanzibar imepiga hatua kubwa ya maendeleo mbayo yanaendelea kustawisha maisha ya jamii na kuongezeka kwa pato la Taifa lililoongezeka zaidi katika kipindi cha takribani miaka mitano.

Naye Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Mohamed Aboud Mohamed, alisema milango iko wazi wakati wote katika kuona jukumu alilokabidhiwa Waziri Zungu analisimamia vyema kwa upande wa Zanzibar.

Aboud alisema yapo mambo mengi yanayoendelea kushirikisha viongozi wa pande zote mbili za Muungano ambayo Zungu atapaswa kupewa ushirikiano ili kutekeleza jukumu lake hasa vikao vya wataalamu, watendaji waandamizi, mawaziri na viongozi wa juu wa pande hizo mbili wanaounda kamati ya pamoja na Muungano.

Kwa upande wake Balozi Iddi alisema zipo fursa nyingi zinazoendelea kuwafaidisha wananchi wa Zanzibar ndani ya ardhi ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania kwa upande wa Bara.

Alizitaja baadhi ya fursa hizo ni sekta ya biashara na ardhi inayowapa nafasi pana wananchi wa Zanzibar walioamua kuishi Bara kuendeleza shughuli zao za uwekezaji katika kilimo.



Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira, Mussa Hassan Zungu (kushoto), akizungumza na Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Balozi Seif Ali Iddi, alipofika kujitambulisha rasmi baada ya kuteuliwa kushika wadhifa huo. Kulia ni Mohamed Aboud Mohamed, Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, inayosimamia na kuratibu Muungano na Mazingira kwa upande wa Zanzibar. **RAHMA SULEIMANI**

# Vifungashio vya ukwaju vyazagaa mjini

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

LICHA ya Zanzibar kupiga marufuku matumizi ya mifuko ya plastiki ambayo imekuwa ikiharibu mazingira, hivi sasa Mji wa Zanzibar umezagaa vifungashio vya plastiki vya Ice-cream ya ukwaju.

Hali hiyo imekuwa ni kero kwa wananchi na wadau wa mazingira.

Kutokana na kuzagaa kwa vifungashio hivyo vinavyochafua mji, Mamlaka ya Usimamizi wa Mazingira imekaa na wafanyabiashara wa ukwaju ili kudhibiti uchafuzi wa mazingira.

Mamlaka hiyo imewataka wafanyabiashara hao kutafuta njia bora ya kuhifadhi vifungashio vya bidhaa hiyo ili visiendelee kuharibu mazingira ya Mji wa Zanzibar.

Akizungumza na wafanyabiashara wa bidhaa hiyo, Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka hiyo, Sheha Mjaja Juma, alisema kuendelea kuzagaa kunaathiri haiba ya mji kuwa mchafu na kuibua malalamiko kwa wananchi.

Alisema, mamlaka hiyo kwa kushirikiana na wadau wengine wa mazingira zimekuwa zikishirikiana kuhakikisha mji unakuwa katika hali ya usafi, ambapo ni kichocheo kikubwa cha kuingia watalii nchini.

"Tumekutana kwani tumeona vifuko hivi vimeshaanza kuleta changamoto ya kimazingira, siku moja vifungashio vya plastiki vya ukwaju 9,000 vinatupwa ovyo," alisema.

Mjaja alisema hali ya mji kwa sasa ni mchafu kutokana na kuzagaa kwa vifuko hivyo jambo ambalo halipendezi hasa kwa wageni wanaoingia nchini katika maeneo ya Mji Mkongwe.

Aliwataka wafanyabiashara hao kuhakikisha wanawaelimisha wananchi kutokutupa ovyo vifungashio hivyo baada ya kula bidhaa hiyo na kutembea na mifuko inayokubalika kimazingira.

Hata hivyo, alisema mamlaka yake inashirikiana na Baraza la Manispaa ili kuhakikisha wanatekeleza kanuni ya kudhibiti wa uchafuzi wa mazingira unaotokana na taka ili Zanzibar iweze kupata hadhi inayostahiki ya kuwa miongoni mwa nchi zinazoongoza kwa usafi wa mazingira.

Mjaja alisema wameshakutana na uongozi wa kampuni ya Bakhresa inayotengeneza bidhaa hiyo na kukubaliana kufanya utafiti wa kuona kuna vifungashio mbadala ili kutoathiri mazingira.

Naye Ofisa Uhusiano wa Baraza la Manispaa Mjini, Seif Ali Seif, alisema wanaandaa kanuni ya adhabu ya papo kwa papo ambayo mtu yeyote atakayekamatwa kutupa taka ovyo atatozwa faini ya Sh. 30,000.

Kwa upande wao wafanyabiashara wa ukwaju walisema wateja wao wanaponunua bidhaa hiyo huwa wanaondoka nayo, hivyo inakuwa vigumu kupata kifungashio baada ya kula bidhaa hiyo.

"Wateja wetu wengi wananunua bidhaa hii wakiwa katika usafiri, aidha, daladala au usafiri binafsi, hivyo inakuwa vigumu kuturejeshea vifungashio hivyo," alisema Bakari Ali.

Aidha, waliishauri serikali kuweka sheria zitakazowabana wananchi wanaotupa ovyo taka ikiwamo plastiki ili kuweka mji katika hali ya usafi.

# Wavuvi washauriwa taarifa hali ya hewa

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

OFISA Elimu kutoka Kamisheni ya Kukabiliana na Maafa Zanzibar, Haji Ame Haji, amewataka wavuvi kuzingatia taarifa zinazotolewa na Mamlaka ya Hali ya Hewa ili kujiepusha na maafa.

Akizungumza wakati wa kutoa mafunzo kwa wajumbe wa kamati za uvuvi katika kijiji cha Fumba, alisema elimu ya maafa ni muhimu kwa wajumbe wa kamati ya uvuvi ambayo yatasaidia kupata taaluma ya kujikinga na maafa na kuzingatia taarifa zinazotolewa na Mamlaka ya Hali ya Hewa.

Pia aliwataka kutumia uzoefu wa asili katika kujiandaa kukabiliana na maafa.

Alisema elimu hiyo itawajengea uwezo na mbinu za kujikinga na majanga pamoja na kupunguza athari za maafa yanapotokea.

Alieleza kuwa maafa yanaweza kutokezea kwa viwango tofauti ikiwamo ya mtu mmoja, jamii na hata taifa kwa ujumla.

Naye Ofisa Elimu Msaidizi wa Kamisheni ya Kukabiliana na Maafa Zanzibar, Aziza Ali Rajabu, alisema elimu kwa kamati za uvuvi zinasaidia katika kujiandaa kabla maafa kutokea.

Alieleza kuwa wavuvi wanatakiwa kuwa makini wanapopatwa na matatizo wakiwa bahari ili kuitumia mbinu ya kujiokoa bila ya kujali hasara watakayoipata.

Aliitaka kamati hiyo kuimarisha mawasiliano na wavuvi pamoja uokozi ili kuwapo na msaada wa haraka na tahadhari za mapema juu ya usalama wao wakiwa katika kazi zao.

Aliwashauri wavuvi kuhakikisha wanachukua zana za kujiokoa wakati wa matatizo ya bahari ikiwamo makoti ya kujiokoa.

Kwa upande wake Katibu wa Kamati ya Uvuvi ya Kijiji cha Fumba, Juma Mohamed Bakari, alisema wamekuwa wakikabiliwa na matatizo mengi katika shughuli zao za uvuvi, hali ambayo inavunja moyo utendaji wa kazi zao.

Hata hivyo, alieleza kufurahishwa na uamuzi wa kamisheni ya kukabiliana na maafa kuamua kutoa taaluma kwa kamati ya uvuvi ya kijiji hicho na kuahidi kuwa wataifikisha elimu hiyo kwa wavuvi wenzao.

# Jumuiya wanyamapori yaipa serikali gawio

**Na Stevie Chindiye,** TUNDURU

JUMUIYA ya Uhifadhi wa Wanyamapori (NALIKA) iliyopo katika Wilaya ya Tunduru mkoani Ruvuma, imekabidhi gawio kwa serikali lenye thamani ya Sh. milioni 15 kwa ajili ya kuendeleza miundombinu ya elimu katika shule tatu za sekondari.

Shule hizo ambazo zitanufaika kwa miundombimu ni za Namwinyu, Matemanga na Ligunga.

Akisoma taarifa kwa mkuu wa wilaya kabla ya kukabidhi gawio, Mwenyekiti wa Nalika, Said Masoud, alisema kuwa jumuiya hiyo imekuwa ikitoa gawio kwa serikali kila mwaka ikiwa ni kuunga mkono shughuli za serikali katika maeneo yanayozunguka jumuiya hiyo.

Masoud alifafanua kuwa katika kipindi cha mwaka huu imepanga kutoa zaidi ya Sh. milioni 30, lakini imeanza na Sh. milioni 15 kwa shule tatu kila moja utapata shilingi milioni tano kwa ajili ya shughuli za ujenzi wa hosteli katika shule zilizopo kwenye maeneo yanayozunguka jumuiya hiyo.

Mkuu wa Wilaya ya Tunduru, Julius Mtatiro, amesema serikali ina wajibu wa kushirikiana na Nalika katika kufanya doria katika maeneo ya jumuiya hiyo ili kupambana na wahalifu wanaovamia maeneo hayo na kwamba wasisite kuomba msaada kutoka kwa serikali.

Katika taarifa hiyo Mtatiro aliitaka jumuiya hiyo kuwa na ubunifu katika kupanga mikakati ya kupata mapato ya kutosha badala ya kutegemea tuu chanzo kimoja na uwindaji na ufadhili kutoka kwa wahisani.

"Jumuiya hii iliundwa mwaka 2003 ambapo mwaka 2023 itafikisha miaka 20, hivyo ni vyema kupanga mikakati endelevu ya kupata mapato nje ya shughuli ya uwindaji ikiwa ni pamoja na kujikita katika shughuli za kilimo kama kilimo cha ufuta na korosho ili kujiendesha," alisisitiza Mtatiro.

Mtatiro aliongeza kwa kusisitiza juu ya umuhimu wa kuwa na mipango ya muda mrefu ili kuepuka kuomba fedha kwa wahisani kila wakati. "Nataka kuanza kuona uwekezaji wenu mkubwa kwenye mashamba ya korosho na ufuta hata katika vijiji vingine kwa kushirikiana na ofisi ya Mkurugenzi, ili kupata ardhi kwa bei nafuu, na sitaki kuona taasisi ambayo ni tegemezi kwa wahisani na nitafanya ufuatiliaji."

Aliwaagiza wakuu wa shule za Ligunga, Namwinyu na Matemanga zilizo pata msaada huo kuunda kamati za usimamizi na ufuatiliaji wa fedha hizo na kuhakikisha kuwa zinafanya kazi iliyokusudiwa kwa kuzingatia kipaumbele cha shule husika ili kumaliza changamoto zilizopo kwa sasa.



Waziri wa Maji Prof. Makame Mbarawa, akipata maelezo ya uendeshaji wa mradi wa maji Kibamba-Kisarawe kutoka kwa mwakilishi wa Mamlaka ya Majisafi na Majitaka Dar es Salaam (Dawasa), Mhandisi Ishmael Kakwezi (kushoto), wakati wa ziara ya kutembelea mradi huo uliotekelezwa na Dawasa wenye thamani ya Sh. bilioni 10.5. Pembeni kwa waziri ni wajumbe wa Bodi ya mamlaka hiyo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wakulima wa tumbaku washauriwa

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

MWENYEKITI wa Chama Kikuu cha Ushirika wilayani Kahama (KACU), Emmanuely Charahani, amewataka viongozi wote wa ushirika kuwasihi wakulima wanaposhusha tumbaku kwa kila mchomo waunganishe na kuchambua, kufunga mabelo ili kuepuka unyevu unaotokana na mvua zinazoendelea kunyesha.

Charahani alisema kulingana na Mamlaka ya Hali ya Hewa nchini (TMA)kutabiri kuwapo kwa mvua nyingi katika baadhi ya mikoa inayolima tumbaku, viongozi wa vyama vya msingi kwa kushirikiana na mabwana shamba watembelee wakulima na kuoa elimu ya namna ya kukabiliana na unyevu.

Pia alisema kuwa kwa mwaka huu wakulima wa tumbaku wanakaribia kuzalisha kilo milioni 9.45 kiasi ambacho ni kikubwa kuliko msimu uliopita walipazalisha kilo milioni saba.

Charahani aliyabainisha hayo jana wakati akizungumza na gazeti hili na kuongeza kuwa ili kuepukana na unyevu kwenye maghala ya tumbaku, wanatakiwa kujenga vichanja vyenye urefu wa sentimita 30 hadi 45 ili kuepuka kuloa kwa tumbaku na kupoteza ubora wake.

"Mwaka huu kuna mvua nyingi sana, mabani na maghala ya tumbaku yanaanguka sana, kwa hiyo niwaombe wakulima, viongozi wote wa sekta hii, mabawana shamba na viongozi wa vyama vya ushirika kushirikiana ili kuhakikisha wanawatembea wakulima wote katika kipindi hiki na kuwapatia elimu," alisema Charahani.

Aliongeza: "Mkulima anaposhusha mchomo mmoja wa tumbaku waende sambamba na uchambuzi na uhifadhi wa tumbaku hiyo katika hali ya usafi na kutumia vifungashio vinavyokubaliwa na wanunuzi ili tumbaku ziendelee kuwa na ubora hadi zinapelekwa sokoni.

Charahani aliwataka wakulima katika ufungaji wa zao hilo, kutochanganya madaraja kwani kwa kufanya hivyo, wanapoteza faida na kuleta usumbufu na migogoro isiyokuwa na tija kwenye soko na wanunuzi pia.

# Fursa zaidi ya elimu kwa wazazi, walezi

**Na Mwandishi Wetu**

WAZAZI na walezi wenye watoto wanaosoma, wameongezewa fursa katika akiba wanayoweka benki kwa ajili ya kuwasomesha.

Katika kuhakikisha wazazi na walezi wanakuwa na uhakika wa elimu ya watoto wao, Benki ya Biashara ya DCB imeongeza fursa zaidi kupitia akaunti yake maalum ya mpango wa elimu ya DCB Skonga kwa kuongeza DCB Mini Skonga Ili kuunga mkono juhudi za serikali ya awamu ya tano katika kuboresha sekta ya elimu nchini.

Akizungumza kuhusu fursa hizo, Mkurugenzi wa Biashara wa benki hiyo, James Ngaluko, alisema tofauti na mpango wa skonga uliokuwapo awali ambapo mzazi alipaswa kuweka akiba kuanzia mwaka mmoja hadi 17, sasa kwa kupitia DCB mini skonga mzazi anaweza kuweka akiba kidogo kidogo kwa kipindi cha miezi 12 na kupata uhakika wa elimu ya mtoto wake kwa muda wa miaka mitatu.

"Mpango huu mpya wa mzazi au mlezi anakuwa na uhakika wa elimu ya mtoto kupitia akiba yake anayoweka kila mwezi, lakini pindi anapopata ulemavu wa kudumu au kupoteza maisha, mtoto atasomeshwa kwa kipindi cha miaka mitatu bure.

Mkurugenzi huyo alisema licha ya DCB kuanzisha mpango huu mpya, bado wazazi wanaweza kuendelea kuweka akiba kupitia mpango wa awali wa ambapo mzazi anapata uhakika wa elimu ya mtoto wake hadi chuo kikuu kutokana na mpango aliouchagua kuanzia mwaka mmoja hadi miaka 17.

Ngaluko alisema Watanzania wengi hasa wenye kipato cha wastani hukabiliwa na hofu nyingi mara wawazapo hatima ya elimu ya watoto wao kutokana na changamoto mbalimbali zinazoweza kutokea kiasi cha kupunguza ama kuondoa kabisa uwezo wao wa kulipa gharama za elimu na mahitaji mengineyo.

"Kwa kupitia DCB Skonga au Mini Skonga mteja anapata fursa ya kuamua kiwango cha kuwekeza kila mwezi kwa ajili ya kutimiza ndoto zake, lakini kupata uhakika wa elimu ya mtoto wake, DCB tunaondoa hofu ya mzazi kwani endapo kutatokea majanga yatakayosababisha ulemavu wa kudumu ama kifo kabla ya muda kukamilika, mtegemezi atarudishiwa kiasi cha pesa kilichowekwa tokea mwanzo na mtoto atalipiwa gharama zote za elimu pamoja na hela ya matumizi ya shule kwa kipindi chote kilichosalia cha mkataba," alisema.

Naye Mkuu wa Kitengo cha Masoko na Mawasiliani, Rahma Ngassa, aliongeza kuwa mteja anakuwa na uhakika wa usalama wa pesa zake, uhakika wa elimu ya mtoto hadi chuo kikuu, gawio nono la kila mwaka, uhakika wa mkopo wa dharura hadi asilimia 50 ya kiwango cha akiba alichowekeza, bima ya mazishi endapo mwenye akaunti/mume/mke au mtoto atakapofariki.

HABARI KIMATAIFA

## Mgomo wa mahakimu DRC washika kasi

**KINSHASA, DRC**

MGOMO wa mahakimu unaendelea nchini Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) kudai nyongeza ya mshahara na kuboreshewa mazingira ya kufanya kazi unazidi kupamba moto.

Hali hiyo inashuhudiwa licha ya hapo awali kuwapo kwa mazungumzo kati ya mahakimu hao na waziri wa sheria bila ya mafanikio.

Watumishi hao muhimu wa Idara ya Mahakama, wanataka ahadi ya nyongeza ya mshahara iliyotolewa na Rais wa zamani Joseph Kabila kutekelezwa, kabla ya wao kurudi kazi.

Mgomo huo wa nchi nzima, umesababisha kukwama kwa kesi mbalimbali katika Mahakama za nchi hiyo ya Afrika ya Kati.

"Hii serikali haisemi lolote kuhusu suala hili, ndio maana tumeamua kugoma na tutaendelea hivi labda kwa miezi kadhaa ili tujibiwe," walisema mahakimu wanaogoma.

Hatua hiyo imechelewesha na kusababisha kuahirishwa kwa kesi kadhaa, huku wafungwa wakiwa hawafahamu hatima yao kwa sababu shughuli zinaweza kurejea tu baada ya mgomo huo kuisha.

**RFI**

## FAO yatuma wataalamu kupambana na nzige

**NAIROBI, Kenya**

KENYA inaimarisha juhudi za kupambana na uvamizi wa nzige kwa kutoa mafunzo maalumu kwa kikosi cha kitaifa cha huduma ya vijana kiitwacho KNUS.

Mafunzo hayo yanatolewa na waatalamu kutoka Morocco waliopelekwa na Shirika la Chakula Duniani (FAO) kuisaidia Kenya iliokumbwa zaidi na nzige wa jangwani wanaotishia kuharibu chakula nchini humo.

Mwakilishi wa FAO nchini Kenya, Tobia Takavarasha, alisema wameamua kuisaidia Kenya kwanza kwa vile ni kitovu cha uvamizi huo wa nzige na ndiyo eneo kubwa zaidi linaloathirika, mbali na mataifa matano ya Afrika Mashariki na pembe ya Afrika yanayoizunguka nchi hiyo.

Alisema ukikabiliana na hali ya Kenya kutapunguza athari katika nchi za jirani.

Waziri wa Kilimo na Uvuvi wa Kenya, Kello Harsama, alisema nzige wanahatarisha mfumo wa chakula wa nchi nyingi za Afrika.

Alisema: "Nzige walipoanza kujitokeza Desemba walikuwa katika nchi tatu, lakini hivi sasa wameanza kuenea katika nchi 17 na hilo ni tishio kubwa katika kuzalisha chakula".

**VOA**

# Marekani kuwaokoa raia wake kwenye meli yenye corona

**WASHINGTON, Marekeni**

MAREKANI ina mpango wa kuwaondoa raia wake katika meli ya kitalii ya Diamond Princess, meli ambayo ina maambukizi makubwa ya mlipuko wa virusi vya corona.

Meli hiyo imetengwa katika bandari moja nchini Japan tangu mwanzoni mwa Februari. Kati ya abiria 3,700 waliopo ndani ya meli hiyo, 218 wamegundulika na ugonjwa huo.

Taarifa kutoka ubalozi wa Marekani mjini Tokyo zinaeleza kuwa raia wa Marekani waliopo katika meli hiyo watapatiwa viti katika ndege ya serikali Jumapili.

Takriban watu 1,500 wamefariki kutokana na virusi hivyo duniani ambavyo chanzo chake ni mji wa Wuhan uliopo China.

Tume ya Afya nchini China Jumamosi iliripoti vifo vipya 143 na kuongeza idadi ya waliofariki kufikia 1,523. Wote kutoka mji wa Wuhan isipokuwa wanne wa waathiriwa hao walitoka Mkoa wa Hubei.

Watu wengine 2,641 wamethibitishwa upya kuwa wameambukizwa virusi hivyo na kufanya idadi ya walioambukizwa na ugonjwa huo kufikia 66,492.

Nje ya China, kumekuwa na zaidi ya matukio 500 katika mataifa 24 na vifo vitatu, vikitokea Hongkong, Ufilipino na Japan.

Mlipuko huo katika meli ya Diamond Princess unasemekana kutoka kwa mzee mwenye umri wa miaka 80 ambaye alishuka mjini Hong Kong kabla ya kupatikana na ugonjwa huo.

Kwa sasa abiria na wafanyakazi wanazuiliwa katika meli hiyo mjini Yokohama hadi Jumatano. Mamia ya raia wa Marekani ni miongoni mwa wale waliokwama na takirban 24 wamepatikana na ugonjwa huo.

Lakini katika barua yake, ubalozi wa Marekani mjini Tokyo imeeleza kuwa raia wa Marekani waliopo katika meli hiyo watapimwa kabla ya kuruhusiwa kupanda ndege itakayowarudisha nyumbani Jumapili.

Ndege hiyo inatarajiwa kusafiri katika kambi ya kijeshi ya Travis mjini California ambapo baadhi ya abiria watawekwa katika karantini kwa siku nyingine 14.

Mpango wa kuwatenga zaidi waliopo katika meli hiyo unaonekana kuwakera wengi.

Tungependelea kumaliza karantini iliyowekwa katika meli kama ilivyopangwa, halafu kutusafirisha Marekani kwa mipango yetu, kuna ubaya gani na hatua hiyo? Mmoja ya abiria hao Mathew Smith alituma ujumbe kwenye akaunti ya mtandao wa Twitter.

Kambi ya kijeshi ya wanaanga wa Marekani ya Travis Airbase kwa sasa imewaweka karantini zaidi ya raia 200 wa Marekani waliotolewa mjini Wuhan.

**BBC**



Wanasayansi na wataalamu wa afya wakiwa katika mkutano nchini Geneva, Switzerland wakijadili maambukizi ya kirusi cha corona. **PICHA: REUTERS**

# Video yazima ndoto ya mbunge kuwa meya

**PARIS, Ufaransa**

VIDEO ya ngono imemaliza ndoto ya mgombea wa chama tawala cha Ufaransa, Benjamin Griveaux ya kuwa meya wa mji wa Paris.

Aliyekuwa msemaji wa serikali ya Ufaransa, Griveaus, alisema hakuna ambaye anastahili kupitia unyanyasaji huo.

Video hiyo inaonesha mwanaume akiwa katika hali tatanishi, ilisambaa kwa haraka katika mitandao ya kijamii Alhamisi jioni.

Petr Pavlensky, raia wa Urusi aliyeomba hifadhi ya ukimbizi, alisema kwamba ameweka video hiyo mtandaoni.

Wapinzani kutoka vyama mbalimbali vya kisiasa walionyesha hasira yao baada ya kuiangalia video hiyo.

Meya wa sasa Anne Hidalgo alitoa wito wa kuheshimu maisha binafsi ya watu, huku kiongozi wa chama cha mrengo wa kushoto, Jean-Luc Mélenchon akishutumu tukio hilo na kulitaja kama la kuchukiza.

Kiongozi wa mrengo wa kulia, Marine Le Pen alisema kwa sababu ya demokrasia, Griveaux hakuwa na haja ya kujiuzulu.

Waziri Mkuu, Edouard Philippe alimuunga mkono aliyekuwa mfanyakazi mwenzake na waziri wa ndani, Christophe Castaner na kuonya kwamba kuweka mtandaoni video kama hizo bila idhini ya mhusika ni kosa ambalo mtendaji anaweza kuadhibiwa na kutozwa faini kubwa na kifungo cha hadi miaka miwili jela.

Video hiyo ilionekana kwenye tovuti ambayo haifahamiki na wengi na kuandamana na wasifu wa Griveaux na malengo yake ya kisiasa pamoja na imani yake kali katika maadili ya familia.

Video hiyo ilimwonyesha Griveaux akibadilishana ujumbe wa mapenzi kwa njia ya simu na mwanamke kisha kumtumia video binafsi.

Kiunganishi cha kwenye mtandao ya kijamii kilisambazwa na mbunge ambaye alilazimika kujiuzulu kutoka chama cha Macron mwishoni mwa mwaka 2018.

Griveaux alisema katika kipindi cha mwaka mmoja uliopita, yeye na familia yake wamechafuliwa, wamesemwa kwa maneno ya uwongo, uzushi, kushambuliwa na watu wasiowafahamu na hata kupata vitisho vya kifo.

Wakili wa Griveaux alisema atawasilisha mashtaka dhidi ya video hiyo iliyowekwa mtandaoni ambayo alisema inakiuka faragha ya mtu.

**BBC**

# Watanzania wanaosoma China wapo salama, asema Majaliwa

Na Mwandishi Wetu

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amesema vijana wa Tanzania wapatao 497 wanaosoma katika vyuo mbalimbali vilivyoko kwenye mji wa Wuhan nchini China wote wapo salama.

Kwa sasa Mji wa Wuhan umewekewa zuio hakuna mtu anayeruhusiwa kutoka wala kuingia, lengo likiwa ni kuzuia kuenea kwa maambukizi ya virusi hivyo. Mlipuko wa virusi vya corona ulianzia katika mji wa Wuhan. Alitoa kauli hiyo jana kwenye Kumbukumbu ya Mazazi ya Mtume Muhammad Swalla Allahu Alayh Wasallam iliyoandaliwa na Nida Textile Mills (T) Ltd, na kufanyika katika mtaa wa Indira Ghandi jijini Dar-es-Salaam. Watu zaidi ya 1,500 wamefariki dunia kutokana na mlipuko wa virusi hivyo.

Waziri Mkuu alisema kutokana na zuio hilo, wakazi wote wa mji huo wakiwamo vijana wa Kitanzania wanapata huduma mbalimbali kupitia njia ya mtandao ukiwamo ununuzi wa bidhaa mbalimbali.

"Hakuna usafiri hata wa umma unaofanya shughuli za kusafirisha watu katika mji wa Wuhan kila mmoja anayetakiwa abakie katika makazi yake na kwamba Serikali ya China na uongozi wa vyuo unawatunza wanafunzi wote wakiwamo na Watanzania."

Waziri Mkuu alisema kwamba kwa sasa Wachina wameimarisha utoaji huduma kwa njia ya mtandao hata kama mtu anataka kununua kitu ananunua kwa njia ya mtandao. "Kama kijana ameishiwa basi atumiwe fedha kwa njia ya mtandao ili aweze kujikimu wakati huu wa zuio."

Waziri Mkuu alisema jambo la muhimu kwa sasa ni usalama wao na kujali maelekezo yaliyotolewa na Serikali ya China juu ya usalama wao pamoja na wananchi wengine walioko katika eneo hilo.

Amesema serikali imeweka mitambo ya kupima watu katika maeneo yote ya mipaka, na kwamba inawataka wananchi washirikiane nayo katika kuhakikisha watu wote wanaoingia nchini wanapita kwenye njia sahihi.

Pia Waziri Mkuu aliwataka Watanzania waendelee kuwa watulivu na kuitegemea serikali katika kupata taarifa za mara kwa mara kuhusu masuala mbalimbali zikiwamo na ya mlipuko wa virusi hivyo.



Wakulima wa kikundi cha Fukuza Njaa cha Kijiji cha Butata, Musoma Vijijini mkoani Mara wakiandaa mashamba kwa jembe la kukokotwa na ng'ombe, ambalo ni miongoni mwa majembe 20 yaliyotolewa na mbunge wao Prof, Sospeter Muhongo, kwa ajili ya kuhamasisha wananchi kuacha kilimo cha jembe mkono. **PICHA: MPIGA PICHA WETU**

# Kairuki azindua mwongozo wa uwekezaji mkoani Songwe

Na Mwandishi Wetu, SONGWE

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Uwekezaji), Angellah Kairuki amezindua kitabu cha mwongozo wa uwekezaji katika Mkoa wa Songwe na kuwahamasisha wawekezaji kuchangamkia fursa lukuki zilizopo mkoani humo.

Akimwakilisha Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, katika uzinduzi wa kitabu cha mwongozo na Kongamano la Uwekezaji la Mkoa wa Songwe jana, Kairuki alisema washiriki watapata fursa ya kujadili changamoto mbalimbali zinazokwamisha maendeleo ya uwekezaji na biashara.

"Uzinduzi wa kitabu hiki unaonyesha dhamira ya kweli na utayari wa Mkoa wa Songwe kuvutia wawekezaji katika mkoa huu. Bado ninatoa rai kwa mikoa ambayo bado haijakamilisha mwongozo wa uwekezaji kufanya hivyo," alisema.

Waziri Kairuki alisema Waziri Mkuu Majaliwa mbali ya kuwapongeza Wanasongwe wote kwa hatua waliyofikia, amesema majumuisho na taarifa ya kongamano hilo ameagiza apelekewe kwa ufuatiliaji zaidi.

"Mkoa wa Songwe una fursa nyingi sana za kiuwekezaji na hasa eneo la kilimu pamoja na kuwapo fursa nyinghine kama madini, ufugaji, utalii.

Mna mtaji mkubwa wa watu na hivyo hamna budi mkazitumia fursa hizo kubadilisha maisha," alisema.

Kairuki aliipongeza Taasisi ya Sekta Binafsi nchini (TPSF) kwa kufanya kazi bega kwa bega na uongozi wa Mkoa wa Songwe kuhakikisha kuwa fursa za kibiashara na uwekezaji zinatangazwa na pia kongamano la uwekezaji linaleta mafanikio yaliyokusudiwa.

"Nitakuwa mstari wa mbele kutangaza fursa zilizopo katika mkoa huu na pia naomba msichoke kujifunza kutoka katika mikoa mingine. Jitahidini pia kuwekeza katika miundombinu muhimu ili kuvutia wawekezaji zaidi," alisema.

Alisema tangu alipowasili mkoani Songwe hajasikia malalamiko yoyote kutoka kwa wawekezaji wala wananchi na hivyo akauomba uongozi wa mkoa kuendelea kufanya kazi karibu na wawekezaji ilikuongeza mapato na makusanyo ya serikali.

Mkurugenzi Mtendaji wa TPSF, Godfrey Simbeye, aliipongeza serikali ya ya Rais John Magufuli kwa kufanikiwa kubadilisha fikra miongoni mwa watumishi wa umma.

"Naomba niwe mkweli Mheshimiwa Rais Magufuli amebadilisha kabisa fikra za watendaji na watumishi wa umma dhidi za dhana ya uwekezaji na biashara. Waziri Kairuki amekuwa msaada mkubwa sana katika eneo la uwekezaji na biashara," alisema.

## Wakulima milioni 1 wakopeshwa NMB

Na Mwandishi Wetu

BENKI ya NMB imesema imejizatiti katika kilimo na uwezeshaji wa wajasiriamali wadogo na wa kati kwa uwezeshaji wa aina mbalimbali.

Hayo yalibainishwa na Ofisa Mkuu wa Wateja Binafsi Biashara ndogo na wa kati, Filbert Mponzi katika kongamano la uwekezaji Mkoa wa Songwe.

Mponzi alisema benki hiyo imewakopesha zaidi ya wakulima 1,000,000; kupitia kilimo cha mazao mkakati kama korosho, kahawa, tumbaku, pamba, mazao ya chakula kama mpunga, maharage, mahindi yamejumuishwa.

Aidha, alisema imewezesha wajasiriamali wadogo na wakati kwa kukopesha kiasi cha Sh. bilioni 40 kila mwezi.

Alieleza kuwa kwa kutambua suala la ujumuishaji wa wananchi walio wengi katika sekta ya fedha, NMB imepanga kufungua akaunti 300,000 kwa mwaka huu kwa wakulima, akaunti hizi zitafunguliwa bila gharama ya ufunguzi wala ya kadi.

Kwa mujibu wa Mponzi, benki hiyo imekuwa ikihudumia miradi mikubwa ya kimkakati ya serikali ukiwamo wa umeme vijijini (REA), ambapo benki imetoa dhamana zenye thamani ya Sh. bilioni 44 pamoja na kutoa mikopo mbalimbali kwa makandarasi.

Kadhalika, alisema wamewezesha Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) kununua vifaa muhimu kama mita na nguzo za umeme kwa kutumia dhamana zenye thamani ya Sh. bilioni 54.

Mponzi alieleza zaidi kwamba benki hiyo inashirikiana na kampuni za kigeni zinazo ratibu miradi mikubwa kama ujenzi wa barabara, reli ya kisasa (SGR) pamoja na miundombinu ya maji.

"Kwa kutumia mtandao wetu mpana wa zaidi ya matawi 224, NMB imefanikisha zabuni kwa makandarasi wazawa zaidi ya 400 katika ngazi ya wilaya na mkoa," alisema katika kongamano hilo ambalo mgeni rasmi alikuwa Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa.

Kuhusu huduma za kibenki kwa mkoa wa Songwe, Mponzi alisema NMB ina matawi matano ya Mbozi, Tunduma, Mlowo, Mkwajuni na Ileje, mawakala 100 na imekopesha mikopo kwa wakulima yenye thamani ya Sh. bilioni 22.

Mpinzi alimhakikishia Waziri Mkuu kwamba benki hiyo iko tayari kuendelea kuunga mkono jitihada za serikali katika uwekezaji nchini.

Aliishukuru serikali ya awamu ya tano kwa kuendelea kutoa kipaumbele kikubwa katika uwekezaji nchini na kuweka mazingira wezeshi kwa wawekezaji kwa lengo la kukuza uchumi wa nchi na kuchangia katika kukuza pato la Taifa.

"Pia kwa namna ya pekee, napenda kumpongeza Mkuu wa Mkoa wa Songwe na timu yake kwa maandalizi mazuri ya kongamano hili muhimu la uwekezaji.

## TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

### MATANGAZO MCHANGANYIKO

**NYUMBA INAUZWA MIL 70 ARUSHA NGULELO:,** SELF VYUMBA 3 KIMOJA MASTER, SITTING, JIKO NA STORE, INA UMEME âNA MAJI INAFAA KUISHI, FINISHING NA FENSI UNAIMALIZIA.MWENYE NYUMBA **0757 804 970**

**MKOPO WA HARAKA NA KUTOKA ENTERPRISE FINANCE LIMITED (EFL)** Kwa mahitaji kama kulipa ada ya shule, kodi, kuboresha biashara, kumaliza tenda etc. Kwa maelezo zaidi piga: **0758 112 332. Karibu EFL**

***NIPASHE NI JIBU LAKO***

**NJOO UTANGAZE NASI**

**BIDHAA YAKO**

**KWA BEI NAFUU SANA**

**LOSS OF CERTIFICATE OF REGISTRATION TIGER FRIENDSHIP SOCIETY**

inatangaza kupotelewa na Certificate of Registration yenye namba ya usajili 9966 iliyotolewa mwaka 1999.

Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

Control No. 9911081167784.

115630702

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**UASIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA YA 5 KANUNI 2)**
**KATIKA MAHAKAMA YA WILAYA YA DODOMA**

**USIMAMIZI WA MRATHI NO.09/2020**
**TANGAZO**

Ombi la ROSE YOHANA SENKUNDE Kuteuliwa Msimamizi wa mirathi ya Marehemu CHISHOSHA WILLIAM MBIJIMA

KWA YEYOTE ANAYEHUSIKA NA MIRATHI HII NA MWENYE PINGAMIZI LOLOTE

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya Marehemu huyo na wana nia ya kupinga ua kuthibitisha uteuzi wa mwombaji wanaalikwa kufika mahakamani na kuhudhuria kesi mnamo tarehe 04/03/2020 ili kuwasilisha mapingamizi yao kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
Imetolewa tarehe 12/2/2020

SAHIHI / SIGNATURE........................

115632402

***Kwa Habari Motomoto***

***usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku Tupigie 0782253676***




TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.



# KANTE:

## TUNATAKA USHINDI KWA MAN, SIO KISASI

**LONDON, England**

N'GOLO Kante amesema mchezo wa Chelsea nyumbani dhidi ya Manchester United leo Jumatatu sio wa 'kulipiza kisasi' cha kufungwa kwenye mchezo wa ufunguzi wa Ligi Kuu England pale Old Trafford, lakini ni wa kuweka 'pua' zao mbele kuwania kumaliza kwenye nne bora.

Chelsea bado wapo nafasi ya nne kwenye msimamo, lakini baada ya kupata ushindi mmoja kwenye mechi zao nne zilizopita za Ligi Kuu, kumewafanya kuwa na pengo kubwa na zile tatu za juu.

Wamewapita pointi mbili tu Sheffield United walipo nafasi ya tano, huku Tottenham Hotspur inaweza kupunguza pengo hadi pointi moja na Blues hao kama ilishinda mchezo wake wa jana Jumapili dhidi ya Aston Villa. United wameipita pointi sita.

"Man United tuliwaacha mbali, lakini sasa wapo karibu na wamepunguza gepu, hivyo ni nafasi kwetu kuongeza gepu zaidi au faida kwao kupunguza pengo," alisema kiungo Kante.

"Ni mchezo muhimu kwa timu zote mbili. Wote tunajua kwamba wakicheza nyumbani unakuwa mchezo mgumu, hasa kile kilichotokea kwenye mchezo wa kwanza kwa ufunguzi wa Ligi.

"Tunaangalia mbele kwa sababu tunataka kuendelea kuwa na gepu na wao na ndio maana tunataka kushinda na sio kulipa kisasi."

Ni wiki ngumu kwa Chelsea wakianza kuikabili United leo Jumatatu nyumbani na watacheza na Tottenham Jumamosi nyumbani kabla ya kwenda kuwavaa Bayern Munich kwenye mchezo wa kwanza wa Ligi ya Mabingwa Ulaya hatua ya 16 bora.

# HAALAND MCHEZAJI BORA WA MWEZI BUNDESLIGA

**DORTMUND, Ujerumani**

ERLING Haaland ametwaa tuzo ya mchezaji bora wa mwezi wa Ligi Kuu ya Ujerumani, Bundesliga, kwa Januari licha ya kucheza dakika 60 tu.

Haaland mwenye umri wa miaka 19, ambaye alijiunga na Borussia Dortmund akitokea klabu ya nchini Austria ya FC Salzburg wakati wa dirisha dogo la Januari, alicheza mara mbili mwezi huo, akifunga hat trick katika mchezo wake wa kwanza dhidi ya Augsburg na akafunga mara mbili dhidi ya Cologne.

Katika mechi zote mbili mchezaji huyo wa kimataifa wa Norway alitokea benchi kipindi cha pili.

Tangu hapo, Haaland amefunga mara nne kwenye mechi nyingine alizocheza.

"Ni mchezaji asiyezuilika," alisema kocha wa Dortmund, Lucien Favre. "Ni jambo la kuvutia kwa kocha kuwa na mchezaji kama yeye."

Miongoni mwa wachezaji waliokuwa wanawania tuzo hiyo ambayo ameitwaa, Haaland ni mchezaji mwenzake, Jadon Sancho na nyota wa Bayern Munich, Robert Lewandowski.

Dortmund iliwapiku Manchester United kupasa saini ya Haaland, licha ya Ole Gunnar Solskjaer, ambaye alimnoa mchezaji huyo pale Molde kukutana nae na kumpa ushauri Desemba mwaka jana.

# Nahodha City ahofia Guardiola kuondoka

**MANCHESTER, England**

NAHODHA wa zamani wa Manchester City, Richard Dunne, anahofu kwamba itakuwa ni vigumu kwa Pep Guardiola kuendelea kubakia pale kwenye dimba la Etihad baada ya klabu hiyo kufungiwa kutoshiriki misimu miwili mashindano yanayoandaliwa na Shirikisho la Vyama vya Soka Ulaya, UEFA.

Chombo hicho kinachosimamia soka la Ulaya kilitangaza Ijumaa kwamba, City itazuiwa kushiriki kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya na Ligi ya Europa kwa msimu wa 2020-21 na 2021-22 baada ya kuvunja sheria ya haki sawa ya matumizi ya fedha kati ya mwaka 2012 hadi 2016.

City imetoa taarifa kwamba inakata rufani kwa adhabu hiyo kwa mahakama ya usuluhishi wa michezo, wakisema kwamba "wamekatishwa tamaa" na hatua hiyo ya UEFA, ambapo pia wanatakiwa kulipa faini ya pauni milioni 25.

Guardiola alijiunga na City mwaka 2016 na ameiongoza klabu hiyo kushinda mataji matano kati ya sita ya nyumbani kwenye soka la Uingereza.

Hata hivyo, beki huyo wa kati wa zamani wa timu ya Taifa ya Ireland na City, Dunne anahisi kwamba Guardiola haweza kuendelea kubakia hapo.

"Popote anapokwenda mara zote anakuwa mshindi. Ndio maana itakuwa ngumu kumbakisha pale City," alisema akinukuliwa na Omnisport.

"Anataka kwenda na kushinda mataji na kama City watabakia kwenye hali hii, hawataweza kushindana, kwa sababu wataweza wachezaji na hawataweza kuwashawishi wengine kuja."




Mshindi wa Jackpot bonasi ya SportPesa, Ngassa Kulwa Simba (33), (kushoto) mkazi wa jijini Mwanza akikabidhiwa mfano wa hundi ya Sh. 10,814,995 na Mkurugenzi wa Uendeshaji SportPesa Tanzania, Luca Neghesti (kulia) baada ya kubashiri kwa usahihi mechi 12 kati ya 13 wiki iliyopita. Mshindi wa Jackpot wiki iliyopita alikuwa ni Yassin Ridhiwani Ally ambaye alishinda zaidi ya Sh. milioni 437 baada ya kubashiri mechi zote 13 kwa usahihi. **PICHA NA SPORTPESA**

# MWAMUZI AMCHEFUA KOCHA BARCA



**BARCELONA, Hispania**

KOCHA Quique Setien hakufurahishwa na staili ya uchezaji wa kutumia nguvu ya Getafe pamoja na mwamuzi, Guillermo Cuadra Fernandez baada ya Barcelona kuibuka na ushindi wa 2-1 kwenye mchezo wa Ligi Kuu ya Hispania, LaLiga.

Barca walijivuta kileleni mwa msimamo sawa na vinara Real Madrid, ambao jana Jumapili walikuwa wakicheza na Celta Vigo, baada ya mabao ya kipindi cha kwanza ya Antoine Griezmann na Sergi Roberto kwenye dimba la Camp Nou.

Mchezaji anayehusishwa na kutakiwa Barca, Angel Rodriguez aliifungia bao la kufutia machozi Getafe kipindi cha pili.

Kocha Setien alisema baada ya mchezo huo kuwa mwamuzi, Cuadra Fernandez alitakiwa kuchukua hatua za haraka kwenye mchezo huo dhidi ya wachezaji wa Getafe.

Alipoulizwa kama makosa hayo yalikuwa kwa mwamuzi wa nne, Setien alisema: "Nilikuwa nalalamika kwa sababu muda mwingi ilikuwa ni hatari kwa wachezaji wangu.

"Walikuwa wanatumia nguvu nyingi na mwamuzi hakuonyesha kuchukua hatua yoyote. Wakati mwingine unakuwa huna bahati."

# Tuchel akasirika wanaohoji kiwango cha PSG

**PARIS, Ufaransa**

THOMAS Tuchel alikasirishwa na maswali kuhusu kiwango cha Paris Saint-Germain baada ya kutoka sare ya kufungana 4-4 na Amiens.

Wakiwa bila ya Kylian Mbappe na Neymar, PSG walijikuta nyuma kwa mabao 3-0 kipindi cha kwanza kwenye mchezo huo wa Ligi Kuu ya Ufaransa, Ligue 1, juzi Jumamosi.

Hata hivyo, mabao mawili ya Tanguy Kouassi na mengine mawili kutoka kwa Ander Herrera na Mauro Icardi yaliwarudisha mchezoni, kabla ya Serhou Guirassy kusawazisha dakika ya 91 na kuipa sare hiyo Amiens.

Sare hiyo imewafanya PSG kucheza mechi tisa bila ushindi na kuongeza mechi ambazo hawajapoteza kufikia 23, huku wakielekea kwenye mchezo wa kwanza wa Ligi ya Mabingwa Ulaya hatua ya 16 dhidi ya Borussia Dortmund, kesho Jumanne.

Lakini Tuchel hakuwa na furaha na shaka ya kiwango cha PSG, akisema timu yake ilikuwa na wakati mbaya dhidi ya Amiens.


"Sasa nini? Mlipenda nipoteze? Ni jambo nzuri kwenu, mnaweza kusema mna shaka, shaka, shaka. Ni nzuri kwenu, lakini sio kwa upande wangu," alisema kocha huyo wa PSG akiwaambia waandishi wa habari.

"Sitarajii chochote. Mara zote natarajia timu isipoteze. Najua kwamba kwenu nyinyi na yoyote ni kawaida kutaka tuwe tunashinda, na kutoruhusu bao, na tukifanya hivyo, mara zote inaonekana kuwa rahisi kwa sababu tuna timu bora na wachezaji bora.

"Na leo tulicheza karibia nusu saa bila kuwa na malengo, ilionesha kwamba inaweza kutokea. Hii ni Ligue 1. Kuna ubora.

"Na sasa kila mmoja anahofia, tuna mambo mengi, haya ni maisha, na huu ndio mchezo wa soka."

Licha ya sare hiyo, PSG bado inaongoza msimamo wa ligi hiyo kwa tofauti ya pointi 13 kileleni.



# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# KLOPP AKUNWA KIWANGO CHA MANE AKITOKA MAJERUHI

Sasa yuko fiti kuivaa Atletico Ligi ya Mabingwa Ulaya hatua ya 16 bora...

**LIVERPOOL, England**

MFUNGAJI wa bao la ushindi la Liverpool, Sadio Mane alirudi vizuri kutoka majeruhi kwenye mchezo dhidi ya Norwich City na sasa yupo tayari kuivaa Atletico Madrid kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya hatua ya 16 bora, kwa mujibu wa kocha wake, Jurgen Klopp.

Klopp alionekana kukunwa zaidi na kiwango cha Mane, baada ya fowadi huyo wa kimataifa wa Senegal kurudi dimbani akitoka kuuguza majeruhi ya nyama za paja na kufunga bao hilo pekee pale katika dimba la Carrow Road kwenye mchezo huo wa Ligi Kuu ya England.

Ushindi huo wa 1-0 umeifanya Liverpool kuongoza ligi kwa tofauti ya pointi 25 kileleni dhidi ya Manchester City waliopo nafasi ya pili, huku wakiweka rekodi ya kupoteza pointi mbili tu kwenye Ligi Kuu hadi sasa.

Mane na James Milner waliingia wakitokea benchi na kucheza kwa ushirikiano mzuri na kufanikisha ushindi huo kwenye mchezo huo wa 26 wa Ligi Kuu msimu huu. Baada ya mchezo huo, Klopp alisema: "Inasaidia wakati ukiwa na wachezaji bora kama wale benchi na kuwaingiza ndani."

Liverpool sasa itarudi dimbani kwenye mchezo wake kwanza wa hatua ya 16 bora utakaopigwa kwenye dimba la Wanda Metropolitano dhidi ya kikosi cha kocha, Diego Simeone, Atletico.

"Sadio angeweza kuanza bila shaka yoyote," alisema Klopp, "lakini nilitaka kuwa na maamuzi huru kwa ajili ya Jumanne.

"Sifikirii mara kwa mara kuhusu mechi hizi, lakini unapokuwa na wachezaji waliorudi kutoka majeruhi kama Sadio na Fabinho, hufikiri kama watacheza mechi mbili. Usifikiri wanaweza kucheza, au wanatakiwa kucheza.

"Na ubora wa vijana hawa ni mkubwa wanaweza kuwasukuma wachezaji wengine kuwa bora zaidi.

"Lilikuwa jambo la busara kwa Sadio kucheza dakika chache. Ilionekana kama alikuwa tayari, ndio ni kweli alikuwa tayari."

## KWA UFUPI

**JUVENTUS KUMTOA RAMSEY WAMPATE POGBA**

KLABU ya Juventus inapanga kuwatoa Aaron Ramsey mwenye umri wa miaka 29 na Adrien Rabiot mwenye miaka 24 kwa Manchester United kama sehemu ya kitita cha pauni milioni 125 ili kujaribu kumrejesha mchezaji wa kimataifa wa Ufaransa, Paul Pogba mwenye miaka 26. ***(La Gazzetta dello Sport)***

**MABOSI MAN CITY WATETA NA WACHEZAJI**

WACHEZAJI wa Manchester City waliitwa katika mkutano na mkuu wa klabu hiyo, Ferran Soriano, Jumamosi, saa moja baada ya klabu hiyo kupigwa marufuku ya kushiriki kombe la Ligi ya Mabingwa Ulaya kwa misimu miwili. ***(Sunday Telegraph)***

**POCHETTINO KUMRITHI GUARDIOLA MAN CITY**

ALIYEKUWA Kocha wa Tottenham Hotspur, Mauricio Pochettino anaweza kuchukua nafasi ya kocha wa Manchester City, Pep Guardiola iwapo raia huyo wa Hispania ataamua kuondoka klabuni hapo. (Sun on Sunday)

**SPURS ILIMKATAA GREALISH**

KLABU ya Tottenham Hotspur ingekubali kumsajili mshambuliaji wa Aston Villa anayewaniwa na Manchester United Jack Grealish mwenye umri wa miaka 24, kwa pauni milioni 6 miezi 18 iliyopita, lakini mwenyekiti Daniel Levy alikata kufikia makubaliano hayo. ***(Sun)***

**SOLSKJAER HALI BADO NI TETE**

HATIMA ya kocha wa Manchester United, Ole Gunnar Solskjaer iko mashakani baada ya kushindwa kuwasajili wachezaji watatu waliokuwa wakilengwa katika kipindi cha usajili wa dirisha dogo la Januari. ***(Star Sunday)***

**CONTE AMTAKA AUBAMEYANG INTER**

KOCHA wa klabu ya Inter Milan, Antonio Conte ameonesha nia ya kutaka kumsajili mshambuliaji wa Arsenal na timu ya taifa ya Gabon, Pierre-Emerick Aubameyang mwenye umri wa miaka 30. ***(Sunday Mirror)***

**MARTINEZ KURUHUSIWA KWENDA BARCELONA**

TIMU ya Inter Milan itamruhusu mshambuliaji wake, Lautaro Martinez raia wa Argentina mwenye umri wa miaka 22, kujiunga na Barcelona iwapo itafanikiwa kumsajili mshambuliaji wa Ufaransa, Antoine Griezmann mwenye umri wa miaka 28. ***(Tuttosports)***

**LIVERPOOL BADO WAKOMAA NA WERNER**

KLABU ya Liverpool ipo katika mazungumzo ya mwisho ya kumsajili mshambuliaji wa RB Leipzig, Timo Werner raia wa Ujerumani kwa ada inayotajwa kuwa ni pauni milioni 48. (Sunday Express)

**KIERAN TIERNEY AWANIWA LEICESTER**

NYOTA wa Arsenal, Kieran Tierney anawaniwa na kocha wa Leicester City, Brendan Rodgers, ambaye aliwahi kuwa na mchezaji huyo wa Scotland mwenye umri wa miaka 22 wakati akiwa pale Celtic. ***(90min)***

**ISCO AGOMBEWA CHELSEA, ARSENAL**

KLABU za Arsenal na Chelsea zinafikiria kuwasilisha ombi la kumsajili kiungo wa kati wa Hispania mwenye thamani ya pauni milioni 63, Isco mwenye umri wa miaa, 27, huku klabu ya Real Madrid ikitafuta kuchangisha fedha kujiandaa kwa dirisha la uhamisho la mwisho wa msimu huu. ***(Sun)***

**GIROUD APEWA MKATABA LAZIO**

MSHAMBULIAJI wa Chelsea na Ufaransa, Olivier Giroud, mwenye umri wa miaka 33, amepewa mkataba na klabu ya Lazio, lakini watasubiri kufanya uamuzi huo msimu ujao baada ya ombi kutoka kwa Tottenham Hotspur katika dirisha la uhamisho la Januari. ***(Telegraph)***

## HABARI MICHEZO

# TWIGA STARS YAZIDI KUNG'ARA

**Na Somoe Ng'itu, TUNISIA**

TIMU ya Soka ya Taifa ya Wanawake (Twiga Stars) imeendelea kufanya vizuri katika mashindano ya Kombe la UNAF baada ya kupata ushindi wa mabao 3-2 dhidi ya Algeria katika mchezo uliochezwa jana kwenye Uwanja wa Kram jijini Tunis nchini hapa.

Kwa ushindi huo, Twiga Stars imefikisha pointi sita na kuongoza katika msimamo wa mashindano hayo yanayoshirikisha nchi tano za Kanda ya Kaskazini na Tanzania wakiwa waalikwa.

Bao la kwanza la Twiga Stars lilifungwa na Mwanahamisi Omary "Gaucho" katika dakika ya 11 na dakika ya 22 Algeria walisawazisha kupitia Dellidj Anissa.

Dakika ya 44 Affak Horiya aliifungia Algeria bao la pili na sekunde chache kabla ya kwenda mapumziko, Gaucho, mshambuliaji wa Simba Queens aliisawazishia Twiga Stars kwa kufunga bao la pili.

Diana Msewa aliwanyanyua mashabiki wa Twiga Stars baada ya kufunga bao la ushindi dakika ya lala salama na kuipa timu yake pointi tatu muhimu.

Kocha wa Twiga Stars, Bakari Shime amewapongeza wachezaji wake kwa kupambana kusaka ushindi katika mchezo huo wa pili mfululizo.

"Kila timu inavyocheza inazidi kuimarika, kuna makosa yapo tumeyabaini, tutayarekebisha kwa ajili ya mechi inayofuata, tunaendelea kujifunza na kuwapa uzoefu wachezaji wetu kupitia michuano kama hii, inawaimarisha kwa ajili ya mechi za mashindano," alisema Shime.

Twiga Stars itashuka tena dimbani kesho kucheza dhidi ya Morocco ambayo nayo iliwafunga Tunisia katika mchezo wa kwanza na itamaliza dhidi ya wenyeji hao Februari 22, mwaka huu.

Jana jioni Tunisia ilishuka dimbani kuwakaribisha Mauritania, timu zote zikiwa na kumbukumbu ya kufungwa katika mechi zao za kwanza.



Mkurugenzi Mkuu wa Kampuni ya Bia Tanzania (TBL), Philip Redman, akipita kwenye Kili Canvas kupiga picha ikiwa ni sehemu ya hamasa kwa Watanzania kwenda kupiga picha, kwa ajili ya maandalizi ya kilele cha mbio za Kili Marathon 2020 katika ufukwe wa Coco Beach jijini Das res Salam mwishoni mwa wiki. Kili Marathon inatarajiwa kufanyika Machi Mosi 2020 mkoani Kilimanjaro. PICHA: TBL

# Kili Canvas yawa kivutio kwa wakimbiaji Dar

**Na Mwandishi Wetu**

KILI Canvas iliyozinduliwa na Kampuni ya Bia Tanzania (TBL) kupitia bia yake ya Kilimanjaro Lager hivi karibuni jijini Dar es Salaam, imekuwa kivutio kikubwa kwa wakimbiaji mbalimbali wa jiji hilo.

Canvas hiyo ina lengo la kuhamasisha wakimbiaji wa vitongoji tofauti vya Jiji la Dar es Salaam na mji wa Moshi katika kuelekea kilele cha mbio za Kili Marathon zinazotarajiwa kufanyika Machi Mosi, 2020 mkoani Kilimanjaro.

Kili Canvas ni picha maalumu iliyochorwa kwa ukubwa ambapo mkimbiaji yeyote akipita karibu yake anapigwa picha na picha hiyo yenye muunganisho wa teknolojia ya kisasa baadaye kumtumia picha hiyo kupitia simu yake ya mkononi. Hata hivyo, mkimbiaji anatakiwa kujisajili na kupewa chip maalumu ambayo anatakiwa kuwanayo kwa maelekezo ya wahusika.

Mtangazaji wa Wasafi Redio FM, Maulid Kitenge mmoja wa wakimbiaji wa Wasafi Jogging Club ambaye amevutiwa na Canvas hiyo jijini Dar es Salaam, alisema, "Teknolojia hiyo nzuri ambayo inakupatia picha yako tena nzuri pasipo kupata taabu yoyote."

Aliongeza, "Mwaka jana alikimbia Kili Marathoni lakini mwaka huu pia lazima nishiriki kwa kuvuna rekodi yangu. Sio mimi tu bali wanafamilia wote wa Wasafi Jogging tunatarajia kushiriki Kili Marathon 2020."

Meneja wa Bia ya Kilimanjaro, Pamela Kikuli alisema kuwa, mtu yeyote anayependa mchezo wa kukimbia anaweza kupata fursa ya kupita katika Canvas hiyo na kufaidi teknolojia hiyo ya kisasa ya kupigwa picha na kisha kutumiwa katika simu yake.

Kwa mujibu wa meneja huyo, usajili bado unaendelea kwa ajili ya kujipatia chip unafanyika Mlimani City na Uwanja wa Taifa Temeke jijini Dar es Salaam.

## Azam FC yafunguka Coastal ilipowashika

**Na Saada Akida**

KOCHA Msaidizi wa Azam FC, Idd Nasso 'Cheche' amesema kutofuata maagizo kwa wachezaji wao, ni sababu kubwa ya kupoteza mchezo dhidi ya Coastal Union juzi.

Juzi Azam iliwakaribisha Coastal katika mchezo wa Ligi Kuu Tanzania Bara uliopigwa Uwanja wa Uhuru na kukubali kipigo cha mabao 2-1.

Akizungumza na Nipashe jijini Dar es Salaam jana, Cheche alisema wapinzani wao walikuwa wazuri kwa mipira mirefu na kona, walilifanyia kazi lakini wachezaji wao walishindwa kufuata maagizo.

Alisema wachezaji wao hawakufuata maagizo ambayo walitoa kabla ya kukutana na Coastal hasa wanapopata kona na kucheza mipira mirefu.

"Coastal ni wazuri kwa kona na mipira mirefu, hasa pale tunaposhambulia na wanapoupata mpira lazima umakini uwepo kwani wanakuwa hatari kwa kupiga mipira mirefu hawakosei," alisema.

Alisema baada ya mchezo huo wanaenda kukaa na kujadiliana kwa ajili ya kufanyia kazi upungufu wao na kujipanga kwa mchezo ujao.

## Straika Twiga Stars atamani 'hat trick'

**Na Somoe Ng'itu, TUNISIA**

MSHAMBULIAJI anayekuja kasi wa timu ya soka ya Taifa ya Wanawake (Twiga Stars), Aisha Masaka, amesema anatamani kuona anafunga hat trick katika mashindano ya Kanda ya Kaskazini (UNAF), yanayoendelea nchini hapa.

Hata hivyo, Masaka ambaye alianzia benchi katika mchezo wa kwanza ambao Twiga Stars ilipata ushindi mnono wa mabao 7-0 dhidi ya Mauritania, hakufunga bao hata moja.

Akizungumza na gazeti hili jana, Masaka alisema kuwa kitendo cha kukaa benchi katika mchezo wa kwanza kilimsaidia kuwasoma wapinzani wao na anaamini ndoto zake zitatimia bila wasiwasi.

Masaka alisema amejipanga kucheza katika kiwango cha juu ili kujihakikishia namba katika, kikosi cha kwanza cha Twiga Stars lakini muhimu ni kuifanya timu yao irejee nyumbani na ubingwa wa michuano hii inayoshirikisha mataifa matano.

"Malengo yangu ni kufunga hat trick, ninaamini sitatoka patupu katika mashindano haya, tena mechi ya mwisho ndio itakuwa yangu, nitawashangaza wote, nataka kutengeneza jina langu, kwa hiyo ni lazima nionyeshe ubora wangu," alisema Masaka.

Twiga Stars itashuka uwanjani tena kesho kucheza dhidi ya Morocco wakati Mauritania watawakabili Algeria na itamaliza michuano hii kwa kuwavaa wenyeji Tunisia.

# Michezo

Jumatatu Februari 17, 2020

Nipashe




Twiga Stars yazidi kung'ara

HABARI UK 31



Mshambuliaji wa Azam FC, Obrey Chirwa (kulia), akiwania mpira na mchezaji wa Coastal Union, Bakari Nondo, katika mchezo wa Ligi Kuu uliopigwa Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam juzi, Jumamosi. Coastal ilishinda mabao 2-1. **PICHA NA JUMANNE JUMA**

# SVEN ATOA MKAKATI WA UBINGWA SIMBA

●●●Makali ya kikosi yampagawisha akiokota tatu ugenini, huku wakielekea kuivaa Kagera Sugar kesho asema...

**Na Isaac Kijoti, IRINGA**

BAADA ya kupata ushindi wa pili mfululizo ugenini kwenye mbio za ubingwa wa Ligi Kuu, Kocha Mkuu wa Simba, Mbelgiji Sven Vandenbroeck ametoa siri ya kuepuka presha ya kutwaa taji hilo.

Juzi Simba ikiwa katika Uwanja wa Kumbukumbu ya Samora mjini Iringa iliibuka na ushindi wa bao 1-0 dhidi ya wenyeji wao, Lipuli FC, shukrani kwa bao la dakika ya 23 kupitia kwa nahodha John Bocco.

Ushindi huo unaifanya Simba kuendelea kung'ang'ania kileleni mwa msimamo wa ligi hiyo ikiwa na pointi 56, na 12 zaidi ya washika nafasi ya pili, Azam FC wakati huu zote zikishuka dimbani mara 22.

Hata hivyo, watani wao wa jadi, Yanga wenye mechi mbili mkononi za viporo, wapo nafasi ya tatu wakiwa na alama 39 baada ya juzi kulazimishwa sare tasa na Tanzania Prisons katika Uwanja wa Taifa wakati Azam mapema siku hiyo ikikubali kipigo cha mabao 2-1 dhidi ya Coastal Union kwenye dimba la Uhuru.

Kesho Simba ikitarajia kushuka katika Uwanja wa Taifa majira ya saa moja usiku kuikaribisha Kagera Sugar, Sven ametoa siri ya kutwaa ubingwa huo bila presha.

Sven mbali ya kuwasifu wachezaji wake kwa ari waliyoonyesha dhidi ya Mtibwa Sugar wakiichapa 3-0 kabla ya juzi kuibanjua Lipuli FC 1-0, alisema wanachokitazama kwa sasa ni alama tatu tu.

Alisema wakati huu wapinzani wao wakiendelea kupoteza pointi tatu huku wengine wakiondoka na pointi moja, wao wanatazama mbele kwa kujizatiti kileleni.

Alisema ushindani ni mkubwa katika ligi hiyo, hivyo kuvuna alama tatu kutawasaidia pindi wapinzani wao watakaposhtuka watawakuta wamewaacha kwa pengo kubwa.

"Natarajia ari hii itaendelea pia katika mechi ijayo, tunataka kuendelea kuvuna pointi tatu ili kujizatiti kileleni.

"Nimefurahishwa na morali wa kikosi changu, tumepata alama tatu, sasa tunatazama mechi ijayo," alisema.

Baada ya mechi hiyo ya juzi, Simba iliondoka Iringa usiku na kulala mjini Morogoro na jana ilitarajiwa kurejea jijini Dar es Salaam tayari kwa maandalizi ya kuivaa Kagera Sugar kesho kwenye mwendelezo wa ligi hiyo.

## Eymael ataja tatizo Yanga

***

**Na Saada Akida**

PAMOJA na ugumu wa ratiba yao, Kocha Mkuu wa Yanga, Mbelgiji Luc Eymael amesema tayari amebaini udhaifu ulipo katika kikosi chake hasa safu ya ushambuliaji.

Juzi katika Uwanja wa Taifa, Yanga ililazimishwa sare tasa na Tanzania Prisons, hivyo kujikuta ikiendelea kubaki katika nafasi ya tatu ikiwa na alama 39, tano nyuma ya Azam FC inayoshika nafasi ya pili na 17 nyuma ya vinara Simba zilizopo mbele kwa michezo miwili.

Akizungumza na Nipashe jijini jana, Eymael alisema bado ana kazi ya kufanya kwa washambuliaji wake ili kuweza kutumia vema nafasi wanazopata kwa kufunga mabao mengi.

"Washambuliaji wangu wote wana kazi moja tu kufunga na ikibidi kuwatengenezea wengine, lakini bado tunapoteza nafasi nyingi," alisema Eymael.

Alisema kwa kuwa tayari amegundua tatizo hilo ataendelea kulifanyia kazi ili waweze kuipa timu matokeo katika mechi zijazo.

Eymael alisema uwapo wa David Molinga ndani ya Yanga ni moja ya silaha kwake itakayompa ushindi kwenye mechi zao, na kwamba anaamini atamtengeneza vema ili kuzidi kuwa msaada kwa timu.

Alisema amezungumza na Molinga kuhusu tatizo lake la kukosa utulivu jambo litakalompa nafasi ya kufunga mabao mengi.

**"Tuna kazi kubwa ya kufanya kwa kuwa wapinzani wetu wanazidi kujipanga, hilo tunalitambua na tunalifanyia kazi, kwa uwezo ambao anaouonyesha Molinga atafunga mabao mengi, jambo litakalofanya mashabiki wafurahi," alisema kocha huyo.**

Molinga hadi sasa ndiye kinara wa mabao Yanga akiwa na mabao saba akifuatiwa na Patrick Sibomana aliyecheka na nyavu mara nne hadi sasa.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >